**Rufiji Environment Management Project**[1]

## Environmental Management and Biodiversity Conservation of Forests, Woodlands, and Wetlands of the Rufiji Delta and Floodplain

# Usimamizi wa Wanyamapori Wilaya ya Rufiji
# Ripoti ya ushauri kwa vijiji vinne

**Donasian O. Shayo**



**Ripoti nambari 39**

**January 2003**

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na**
Meneja Mradi
Mradi wa Usimamizi wa Mazingira Rufiji
S. L. P. 13513
Dar es Salaam, Tanzania
Simu 023 2402972 Rufiji 022 2666088 Dar 0741 322366
Email: rempute1@bushmail.net iucndar@epiq.or.tz

[1] The Rufiji District Council implements Rufiji Environment Management Project with technical assistance from IUCN – The World Conservation Union, and funding from the Royal Netherlands Embassy.

# Rufiji Environment Management Project – REMP

**Project Goal:** To promote the long-term conservation through 'wise use' of the lower Rufiji forests, woodlands and wetlands, such that biodiversity is conserved, critical ecological functions are maintained, renewable natural resources are used sustainably and the livelihoods of the area's inhabitants are secured and enhanced**.**

**Objectives**

- To promote the integration of environmental conservation and sustainable development through environmental planning within the Rufiji Delta and Floodplain.
- To promote the sustainable use of natural resources and enhance the livelihoods of local communities by implementing sustainable pilot development activities based on wise use principles.
- To promote awareness of the values of forests, woodlands and wetlands and the importance of wise use at village, district, regional and central government levels, and to influence national policies on natural resource management.

**Project Area**

The project area is within Rufiji District in the ecosystems affected by the flooding of the river (floodplain and delta), downstream of the Selous Game Reserve and also including several upland forests of special importance.

**Project Implementation**

The project is run from the district Headquarters in Utete by the Rufiji District Administration through a district Environmental Management Team coordinated by the District Executive Director. The Project Manager is employed by the project and two Technical Advisers are employed by IUCN.

Project partners, particularly NEMC, the Coast Region, RUBADA, The Royal Netherlands Embassy and the Ministry of Natural Resources and Tourism, collaborate formally through their participation in the Project Steering Committee and also informally.

**Project Outputs**

At the end of the first five –year phase (1998-2003) of the project the expected outputs are:

An Environmental Management Plan: an integrated plan for the management of the ecosystems (forests, woodlands and wetlands) and natural resources of the project area that has been tested and revised so that it can be assured of success - especially through development hand-in-hand with the District council and the people of Rufiji.

Village (or community) Natural Resource Management Plans: These will be produced in pilot villages to facilitate village planning for natural resource management. The project will support the implementation of these plans by researching the legislation, providing training and some support for zoning, mapping and gazettement of reserves.

Established Wise Use Activities: These will consist of the successful sustainable development activities that are being tried and tested with pilot village and communities and are shown to be sustainable

Key forests will be conserved: Forests in Rufiji District that have shown high levels of plant biodiversity, endemism or other valuable biodiversity characteristics will be conserved by gazettement, forest management for conservation, and /or awareness-raising with their traditional owners.

# Muhtasari

**Historia ya shughuli hii ya ushauri**
Mradi wa Usimamizi wa Mazingira Rufiji (MUMARU) ni ushirikiano kati ya serikali ya Tanzania, serikali ya Uholanzi na Muungano wa Uhifadhi Ulimwenguni (IUCN). Makao makuu ya MUMARU ni Utete ambapo pia ndiyo makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji. Lengo la MUMARU ni kudumisha maliasili za misitu, mbuga na maeneo chepechepe kwa kuzitumia kwa 'njia ya busara'. Hivyo bioanuwai itahifadhiwa, ikolojia itadumu na watu watakuwa na uhakika wa maisha. MUMARU inahamasisha usimamizi mzuri wa mazingira katika maeneo ya tambarare ya mafuriko na visiwani pamoja na uthibiti wa uvunaji wa wanyamapori. Mradi unafanya kazi zake katika ngazi ya kiwilaya, kimkoa na kitaifa. Sehemu kubwa katika kazi hii ni kutayarisha mpango wa usimamizi wa mazingira ya tambarare ya mafuriko na visiwani.

Sehemu kubwa ya eneo la mradi ni tambarare ya mafuriko, misitu ya pwani, misitu ya kingo za mito, maeneo chepechepe na maeneo yenye miti na vichaka. Eneo hili pia linapakana na pori la akiba la Selous na hivyo huwa na wanyamapori wengi ambao wakazi wa maeneo haya wanadhani ndio chanzo kikubwa cha ufukara kutokana na uharibifu unaofanywa kwa mazao mashambani, mifugo, na tisho kwa maisha yao. Ndani ya eneo la mradi kuna vijiji 52 vinavyokisiwa kuwa na wakazi 150,000 ambao hutegemea kilimo cha mazao ya chakula na uvuvi wa samaki.

Ili kuwezesha uteketezaji wa lengo lake, mradi unawezesha vijiji vya mfano vinne katika usimamizi wa mazingira kwa kufuata mpango wa upangaji wa usimamizi na matumizi bora ya ardhi. Hii ni moja katika mikakati ya sera ya mazingira na juhudi za wanavijiji kufanya matumizi ya busara na endelevu ya rasilimali kwenye ardhi ya vijiji vyao. Ili kuharakisha utekelezaji katika sekta ya wanyampori, MUMARU ilifunga mkataba na mshauri wa fani ya wanyamapori kwa lengo la kutoa ushauri wa kiufundi kwa watumishi waliopewa jukumu la kuwezesha vijiji katika mchakato wa usimamizi wa mazingira na kujipatia kipato kutokana na rasilimali ya wanyamapori.

**Shughuli za mshauri**
Mshauri alipangiwa kufanya shughuli zifuatazo:

- Kupata picha kamili ya hali halisi kwa kila kijiji kwa kusoma taarifa za MUMARU na kwenye majalada ya vijiji husika. Kujadili kwa pamoja kazi iliyokwishafanyika na watumishi wanaohusika katika uwezeshaji wa utekelezaji wa mchakato wa mpango wa usimamizi wa mazingira katika vijiji vya mfano, hasa wawezeshaji wa vijiji, washauri wa misitu na udhibiti wa wanyamapori waharibifu.
- Kutembelea vijiji na kupata maelezo ya maendeleo na mtizamo wa wanavijiji
- Kukubaliana mikakati na mipango ya utekelezaji na wanakijiji, watumishi husika Wilayani na katika mradi wa usimamizi wa mikoko. Hii ni pamoja na kupanga ratiba ya utekelezaji kuwezesha kupata usimamizi wa kisheria kwa maeneo ya usimamizi wa wanyamapori ama taratibu nyingine zinazokubalika.
- Kutekeleza mikakati kwa pamoja na kamati za usimamizi wa mazingira za vijiji, watumishi wilayani na kwenye mradi wa usimamizi wa mikoko na katika ngazi za kitaifa.

**Mbinu ya utekelezaji**
Mbinu ya ushirikishwaji ilitumika katika njia mbalimbali mchanganyiko zilizojumuisha mikutano, matembezi kwenye maeneo ya vijiji, doria, mafunzo kwa vitendo na kuchunguza. Sehemu kubwa ya ushauri imefuata mfumo wa mahojiano (rasmi na isiyo rasmi) na majadiliano ya pamoja. Hata hivyo katika kijiji kimoja, tathmini shirikishi ilitumika kuchambua chanzo cha mfarakano kati ya viongozi wa Halmashauri ya Kijiji, Kamati ya Usimamizi wa Mazingira na Askari wa usimamizi wa maliasili kijijini. Pia nyakati nyingine shughuli ya ushauri ilibadilika kuwa kuamsha na kuhuisha hisia za wanakijiji hasa wakati masuala ya kisheria kuhusu ardhi na rasilimali ya maliasili yalipojadiliwa.

**Mipaka ya kiutendaji ya kijiji**

MUMARU imewezesha wanavijiji kujijengea uwezo kwenye nyanja mbalimbali ikiwemo upangaji wa usimamizi na matumizi bora ya ardhi. Ni budi kuyaendeleza haya na mapendekezo ya mshauri ni kama ifuatavyo:

- Afisa Ardhi wa Wilaya na Mpima Wilaya wasaidie kukamilisha majadiliano na kufikia muafaka kwa vijiiji vya mfano vilivyoshindwa kufikia muafaka kwenye mipaka ya pamoja na vijiji jirani katika vikao vya kawaida vya ujirani mwema. Kwa mfano mipaka ya kiutendaji ya Halmashauri za Wilaya za Rufiji na Kisarawe na pia Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji na Pori la Akiba la Selous ambapo kijiji cha Mtanza/Msona kinahusika. Ni wajibu wa Halmashauri za Wilaya husika kusaidia ukamilishaji wa maelewano kwenye mipaka hiyo ya kiutendaji. Hii ni kufuatana na maelekezo ya sheria ya vijiji namba 5 ya mwaka 1999 kifungu cha 7 (2).
- Afisa Ardhi wa Wilaya na Mpima Wilaya wawezeshe uchoraji wa ramani za msingi (ramani za mipaka ya vijiji) kwa vijiji vya mfano, na kuviandikisha kama ilivyoelekezwa na sheria namba 5 ya 1999 kifungu cha 7 (7). Ramani hii ni muhimu kijiji kitakapohitaji hati ya kuandikikishwa.
- Endapo ni lazima usimamizi wa pamoja wa ardhi unaweza kupangwa kati ya vijiji kama ilivyoelekezwa katika sheria ya ardhi ya kijiji namba 5 ya mwaka 1999 kifungu cha 11.

**Migongano kati ya binadamu na wanyamapori**

MUMARU na watumishi wa Sekta ya Wanyamapori Wilayani wametoa mafunzo mbalimbali kwa askari wa vijiji vya mfano. Haya ni mafanikio makubwa katika uthibiti wa wanyampori waharibifu kwani sheria ya bunduki na risasi ya mwaka 1991 pamoja na sheria ya kuhifadhi wanyampori namba 12 ya mwaka 1974 zinaruhusu ulinzi binafsi wa kujihami kwa mali na maisha ya binadamu. Inashauriwa kuwatumia wanavijiji hawa wenye ujuzi kupunguza matatizo ya usumbufu wa wanyampori hasa kwenye maeneo ya mashambani.

- Hivyo inashauriwa, Vijiji visaidiwe katika kufuata taratibu za kujinunulia bunduki na nyavu na shughuli ya uzuiaji wa wanyamapori waharibifu ikitwe kwenye Halmashauri za vijiji husika.
- Kupata uwezo na kutumia uwezo uliopatikana ni vitu viwili tofauti. Hivi sasa ni vyema kutizama uwezekano wa kutumia uwezo ulioko kwenye vijiji vya mfano katika suala zima la uthibiti wa uharibifu kutokana na wanyamapori vijijini hasa kwa kuzingatia uwezo mdogo uliopo katika Halmashauri ya Wilaya. Kijiji cha Ngarambe kimekuwa mfano mzuri katika kupunguza tatizo la usumbufu wa wanyampori kijijini kwa kutumia askari wake na silaha za kijiji.
- Kwa sasa Halmashauri ya Wilaya inawajibika kutumia ruzuku ya uwindaji wa kitalii kununua risasi kwa ajili ya askari wanyamapori kwenye vituo vya Kata na Tarafa.
- Taratibu za kuboresha mbinu za asili za kujihami na wanyampori waharibifu kwa mfano matumizi ya ndoana kwa kutegea mamba, matumizi ya moto na nyavu kwa wanyamapori wengine zinatakiwa kupangwa na kutekelezwa. Uboreshaji huu unaweza kupangwa na Afisa Wanyamapori akishirikiana na Afisa Maendeleo ya Kilimo na Mifugo wilayani.

**Uwindaji wa wanyamapori kwenye ardhi ya kijiji**

Sambamba na sera ya kukasimu mamlaka ya usimamizi na haki ya matumizi ya rasilimali ya maliasili, MUMARU imejenga uwezo kwa wanavijiji katika nyanja mbalimbali. Hizi ni pamoja na haki za msingi, majukumu ya watendaji, mafunzo rasmi kwa askari na viongozi katika usimamizi wa maliasili, usimamizi wa mazingira na kukita shughuli za usimamizi wa mazingira katika Halmashauri za Vijiji husika. Uwezo huu uliojengeka ni budi ukatumiwa kuharakisha mchakato wa kupata haki ya matumizi kwa rasilimali ya wanyamapori.

Ili kuharakisha haya mshauri anapendekeza yafuatayo:

- Ni vyema Halmashauri ya wilaya hususani Idara ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ikatambua juhudi za wanakijiji katika vijiji vya mfano na kuwasaidia ili kuweza kupata haki ya matumizi ya rasilimali ya wanyampori. Ili kuweza kuharakisha maamuzi, ushauri na msaada, ni vyema Halmashauri ya wilaya ikampa Afisa Mwanandamizi kutoka Idara ya Ardhi, Maliasili na

Mazingira kazi ya uwezeshaji katika mipango wa usimamizi wa mazingira kwenye vijiji vya mfano. Afisa huyu atatakiwa kuwa na uwezo wa kutafsiri sera na sheria za maliasili ama awe na uwezo wa kujifunza kutoka kwa washauri wa nje.

- Ujangili kijijini unaweza tu kuthibitiwa endapo wanakijiji husika watashiriki kikamilifu kadri inavyofaa. Halmashauri ya Wilaya inashauriwa kuwatumia askari wa usimamizi wa maliasili vijijini kwani wana ujuzi wa kutosha na hivyo kuiga mfano wa wilaya nyingine zilizowahi kutumia Askari wa vijiji. Mfano wa wilaya ngingine kama vile Songea, Ruvuma na hata utawala wa Pori la Akiba Selous ambao huwatumia askari wa vijiji hata kwenye shughuli rasmi ambazo kwa kawaida zingefanywa na askari wanyamapori wa serikali.
- Kuna haja ya kujenga ushirikiano katika doria na mafunzo kati ya Askari Wanyamapori wa Pori la Akiba Selous, Halmashauri ya Wilaya na Askari wa Vijiji ili kuweza kudhibiti ujangiri.

**Ufuatiliaji wa wanyamapori**

Ufuatiliaji ni tathmini ya kudumu ya utendaji na hivyo ni sehemu ya ndani katika utekelezaji wa kila siku. Shughuli ya ufuatiliaji wa wanyamapori inajumuisha uchunguzi wa mabadiliko katika mambo muhimu kwa muda maalumu ili kuweza kuelewa hali halisi ya mazingira na kuweza kutabiri mwelekeo na hali tarajiwa kwa baadaye. MUMARU umewezesha kujenga uwezo wa kufanya ufuatiliaji na kila kijiji kina Askari, Viongozi na Watambuzi wa mimea waliofunzwa kwa ajili hii. Kinachotakiwa sasa ni kuandaa mfumo wa ufuatiliaji utakaoelekeza nini cha kufanya, wakati wa kufanya na kifanywe na nani. Mfumo huu pia utamtaka Afisa Wanyamapori wa Wilaya aendelee na taratibu zake za kawaida za ufuatiliaji katika wilayani nzima, na siyo vijiji vya mfano tu utendaji wake wa kazi.

Uandaaji wa mfumo mzuri wa ufuatiliaji unahitaji kufanya warsha ya wadau wote kijijini kwa vijiji vyote vyenye uwezekano mkubwa wa kuanzishwa maeneo ya hifadhi ya wanyamapori ya jamii - WMA's ambapo malengo ya utekelezaji yatachambuliwa na viashiria kuwekwa. Ili kuweza kutekeleza haya inashauriwa:

- Kuendesha warsha ya wadau wote kijijini kujadili na kuandaa mfumo wa ufuatiliaji.
- Kwa sasa itumike fomu ya ufuatiliaji yenye sehemu za kujaza pamoja na matumizi ya daftari wakati wa doria.
- Kuandaa orodha ya rasilimali za kijiji pamoja na matumizi yake (tathmini ya hali halisi, matumizi ya wanyamapori na makazi yake) kama ilivyopendekezwa na Turpie, (2000) katika taarifa yake ya utafiti wa matumizi na thamani ya maliasili za tambarare ya mafuriko na visiwani wilayani Rufiji.
- Kutoa mafunzo zaidi ya usomaji na tafsiri ya namba za chombo cha GPS kwenda kwenye ramani kwa wanavijiji. Pia mafunzo zaidi katika kuandaa na kuhifadhi nyaraka mbalimbali kijijini.

**Utekelezaji wa doria**

Ushiriki wa wadau wote katika upandaji wa mpango kijijini ni muhimu katika kuweka mikakati mizuri inayokubalika kushughulikia masuala muhimu katika mradi wa kijiji. Askari wa Kijiji na Viongozi watokapo mafunzoni wanahitaji msaada kutoka kwa Afisa Wanyamapori/Afisa Ardhi, Maliasili na Mazingira. Hivyo inashauriwa:

- Mahitaji ya msaada wanaohitaji wanakijiji ili kuweza kutekeleza vyema majukumu yao katika doria ni vyema yakabainishwa kwenye warsha ya wadau wote ambapo wataweka mikakati ya pamoja na kugawana majukumu.
- Maswala kama nguo rasmi za doria, vitambulisho na bunduki ni vyema yakaangaliwa kwa karibu.
- Mafunzo kwa vitendo katika utekelezaji wa sheria ndogo, kuwakamata wahalifu na namna ya kuwashughulikia pamoja na mafunzo ya ukusanyaji wa taarifa mbalimbali na utoaji wa taarifa kwa sasa itatosheleza utekelezaji katika ngazi ya kijiji. Mafunzo haya yanaweza kutolewa na Askari yeyote aliyepitia mafunzo ya Askari Wanyamapori katika Taasisi ya Wanyamapori Pasiansi.
- Askari watarajiwa wapewe mafunzo ili kuongeza uwezo wa kufanya kazi kama wenzao waliopitia mafunzo rasmi ya Askari wanyampori wa kijiji.

**Fungamano la wadau**

Utambuzi wa wadau umekuwa ukifanyika katika ngazi ya Wilaya kwenye vikao vya upangaji wa mipango. Warsha za upangaji kwa kawaida ni fupi lakini muhimu sana katika uendelevu wa mradi na hivyo ni muhimu kurejea Mipango ya Usimamizi wa Mazingira ya Vijiji vya mfano kila mwaka na kuhakikisha kuwa wadau wote muhimu wanashiriki kikamilifu. Hivyo inashuriwa:

- Kuandaa orodha ya wadau wote wanaojulikana na wale watakaotegemewa kujitokeza na kuchambua umuhimu na uwezo wa kila mmoja katika kuathiri utekelezaji wa mradi wa kijiji.
- Hakikisha wadau wote muhimu wanashiriki katika mchakato wa upangaji wa mradi kijijini.

**Umaarufu wa pekee na ufanyaji wa biashara ya wanyampori.**

Vijiji vyote vya mfano vina uwezo wa kufanya shughuli za kujipatia kipato kutokana na wanyamapori japo kwa kuendelezwa ili kuwezesha kuinua hadhi ya eneo. Ili kuweza kuboresha hadhi ya wanyamapori na makazi yake ni lazima kufahamu zaidi kuhusu jamii za wanyamapori na mfumo wa kiikolojia katika maeneo yao ya makazi. Uwezo wa kuchunguza haya upo kwa kila kijiji cha mfano na hasa kwenye sekta ya wanyampori. Hivyo inashauriwa:

- Kufanya ufuatiliaji wa idadi ya wanyamapori na mizunuko yake
- Vijiji vya mfano kuhamasisha vijiji jirani kuanzisha uhifadhi kwenye vijiji vyao
- Halmashauri ya Wilaya kushirikiana na wanavijiji kwenye Tambarare la Magharibi kudhibiti ujangili wa wanyamapori na kuagiza vijiji vyote kuiga usimamizi wa mazingira unaofanywa na vijiji vya mfano

**Utekelezaji wa maelekezo ya kuanzisha maeneo ya usimamizi wa wanyampori.**

Vijiji vya mfano chini ya ufadhili na uwezeshaji wa MUMARU vinawajibika kufuata masharti na taratibu ngumu na zilizofungwa kwa uanzishaji wa maeneo ya usimamizi ya wanyampori tofauti na vijiji vya mfano chini ya ufadhili wa programu ua uhifadhi ya Selous kama Ngarambe. Wakati masuala ya maeneo ya kiutawala yanashughulikiwa kama ilivyopendekezwa, inashauriwa:

- Kuwasilisha nia ya kutaka kuhifadhi wanyampori ndani ya eneo la Kijiji kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori. Taratibu zinazotakiwa kufuatwa ni kwa Halmashauri ya Kijiji kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyampori kwa barua baada ya makubaliano kufanyika kwenye kikao cha baraza la kijiji kufuatana na sheria ya ardhi ya kijiji namba 5 ya mwaka 1999. Barua hiyo inatakiwa kuambatana na muhtasari wa kikao cha baraza la kijiji ambacho kimepitisha mpango huo. Ni vema nia hii ikapitia kwenye ngazi rasmi za mawasiliano (Kata na Halmashauri ya Wilaya).
- Vijiji vya mfano vinashauriwa kuangalisha matumizi na thamani ya wanyamapori kwa wakazi wa vijiji jirani kupitia vikao vya ujirani mwema kama njia mojawapo ya kuhamasisha usimamizi wa pamoja wa rasilimali ya wanyamapori. Masuala haya yanaweza pia kujadiliwa kwenye vikao vya kamati ya maendeleo ya kata.

**Rasilimali za majini**

Ni vyema utafiti wa jumla ukafanyika kwenye maji baridi katika vijiji vya Mtanza/Msona, Mbunju/Mvuleni na Twasalie, kwa lengo la kutambua thamani ya mamba na kobe walioko. Utafiti huu utahitaji boti maalumu lenye kuruhusu mtafiti kuona, kutambua na kuwahesabu wanyama hao ndani ya maji. Endapo utafiti utaonyesha kuwepo kwa thamani kubwa, basi taratibu za usimamizi zinaweza kubadilika kadri itakavyofaa. Hivyo inashauriwa:

- Kujadiliana na vijiji husika kuona mtizamo wao na kuamua kwa pamoja kabla ya utafiti kufanyika.
- Kijiji cha Mbunju/Mvuleni kinatakiwa kuiga mfano wa usimamizi na uthibiti wa rasilimali ya samaki, mbinu/vifaa vinavyotumika na namna ya kupata mapato kutokana na shughuli za uvuvi kutoka kwa vijiji vya Mtanza/Msona, Jaja na Twasalie.

**Hifadhi za misitu za Vijiji**

MUMARU na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji imejenga uwezo wa usimamizi wa maliasili katika ngazi za vijiji na wilaya. Hivi sasa Halmashauri ya Wilaya inatakiwa kutumia na kuendeleza uwezo huu na hivyo inashauriwa:

- Halmashauri ya Wilaya itambue hifadhi za misitu za vijiji na ifungue daftari la kuandikisha misitu ya hifadhi wilayani kama ilivyoelekezwa kwenye sheria ya misitu ya mwaka 2002 kifungu cha 40.
- Halmashauri ya Wilaya inawajibika kutoa ushauri wa kitaalamu katika usimamizi wa rasilimali ya misitu vijijini.
- Halmashauri ya Wilaya iweke kumbukumbu ya ufuatiliaji wa bioanuwai (mimea na wanyama jamii zote) katika mfumo wa kurasa za komputa. Hivyo Halmashauri ya Wilaya, hususani Idara ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Wilayani inawajibika kumfunza Afisa mmoja ufundi wa kutumia komputa kwa ajili ya kupokea, kuweka pamoja, kuhifadhi na kutoa taarifa kwa Kamati na Halmashauri ya Wilaya.



# Executive Summary


**Background to the consultancy**
Rufiji Environment Management Project (REMP) based in Utete, the headquarters of Rufiji District, is an environment management project working with the Rufiji District Council of Coast Region with technical assistance from The World Conservation Union (IUCN) and funding from the Royal Netherlands Embassy. The overall goal of REMP is 'to promote the long term conservation through ''wise use'' of the lower Rufiji forests, woodland and wetland such that biodiversity is conserved, critical ecological functions are maintained, renewable natural resources are used sustainably and the livelihoods of the area's inhabitants are secured and enhanced'. REMP is working at District, Regional and National level to promote better management of the environment of the floodplain and delta including better control of the wildlife harvest. A major part of this work is the production of a workable environment management plan for the flood plain and delta.

A big portion of the project area is low lying floodplain and contains mangrove and coastal forests, riparian, swamps, fringing woodlands and thickets. Being adjacent to Selous Game Reserve is blessed with large concentrations of wildlife. These animals are charged with being the main cause of poverty in the area because of their damage to crops, livestock and threats to human lives. There are 52 villages in the project area with an estimated population of 150,000 people who are almost entirely dependent on subsistence agriculture and fishing.

In fulfilling the above role, REMP is currently assisting four pilot villages in the project area to adopt better environment management through land use planning and management. This is in line with the national environment policy and the villagers' efforts towards "wise use" of the natural resources on their village land. This consultancy was contracted by REMP to provide technical backstopping to District Staff from the line departments who play a facilitating role in the village environment management process to enhance and accelerate the process of empowering villagers to take greater control and make greater profit from the wildlife resource.

**Tasks of the consultant**
The detailed tasks envisaged for the consultancy were outlined as follows:

- Gain a clear understanding of present situation in each village by studying REMP reports and files, discussing the REMP work done so far with District staff who have been involved in facilitation of the village environment management planning process, particularly the two VEMP facilitators and the forest and vermin- control advisers.
- Make familiarisation visits to the villages and listen to their descriptions of progress and their aspirations.
- Agree strategies and plans of action with villagers and co-operating district and mangrove management staff and lay out a schedule of tasks for achieving legal and operative village wild animal management areas or other management arrangements as applicable.
- Implement the strategy together with the village environment committees, the district and Mangrove Management Project personnel and national level bodies concerned.

**Methodology**
The approach used was mainly participatory, with a mix of methodologies, which include meetings, field visits, patrols, practical training and observations. Semi - structured interviews (formal and informal) and participatory discussion were the main approach used throughout the consultancy. In one village, however a participatory self-evaluation was used to explore the source of mis-understanding among the village leaders, environment management committee and natural resources management scouts. In some instances the consultancy turned into animation and mediation especially when issues such as legal aspects over village land and resources were being discussed.

**Village boundary issues**
Facilitation by REMP has raised the capacity of the villagers in several areas including local land use planning. These achievements need to be consolidated and efforts continued to strengthen them. These are the consultant's recommendations.

- It is recommended that the District Land Officer and the District Surveyor assist the pilot villages to finalise discussions on boundary dispute as provided by the Village Land Act No. 5 of 1999 section 7 (2). This is specifically in areas where the villages on their own initiatives have failed to resolve the boundary issue in neighbourhood meetings.
- It is also recommended that the same facilitate drawing of a Village Base Map i.e. Village Boundary Map and register the pilot villages as provided in the Village Land Act No. 5 of 1999 section 7 (7). The map will be required when applying for the village certificate.
- In some case, the option of a Joint Land Management may be necessary as provided by the Village Land Act No. 5 of 1999 section 11

**Human - wildlife conflict**
REMP has trained village scouts and others have learnt from them and from DGO personnel. This is a great achievement in problem animal control and the Arms and Ammunition Act of 1991 as well as the Wildlife Conservation Act no. 12 of 1974 permits self-defence to property and life's. It is recommended to use these skilled villagers to reduce the menace at least on farm level.

- It is therefore recommended that, the villages be assisted to acquire fire arms and nets and institutionalise vermin control in the village council
- Capacity raising is one thing and the utilisation of the raised capacity is another. Given the low capacity of the district council to combat problem animals, it is now necessary for the District Council to utilise the trained village scouts in problem animal control. The District can simulate the example of Ngarambe village, where trained village scouts have taken away the District Council nightmare in trying to solve problem animal on their village land.
- As an interim measure, the District should use the 25% revenue accrued from tourist hunting to purchase and supply ammunitions to scout based at Ward/Division headquarters.
- Arrangements should be made to improve the villagers' traditional self-defence methods such as use of hooks for crocodiles, use of fire, noise and nets for other animals. The District Council/Game Officer and Agriculture and livestock officer can arrange for this.

**Wild animal hunting on village land**
REMP has helped to raise the capacity of the villages in terms of their knowledge of legal rights and responsibilities, formal natural resources scouts and leaders training, environment management and has institutionalised environment management in the village council. This is in line with the national policy of decentralisation and devolution of management and user rights of the vast natural resources estate. Capacity acquired needs to be tapped to accelerate the process towards acquiring legal user rights of the wildlife resource for the pilot villages.

The following recommendations are proposed to accelerate the process:
District Council and specifically the Department of Natural Resources needs to acknowledge the efforts of the villagers and assist them to acquire legal user rights to the wildlife resource. To speed up decisions, advice and support from the Department of Natural Resources, there is a need for the District Council to assign a facilitator role to a Senior Officer from the Department of Natural Resources. This officer needs to be able to interpret natural resources policies and laws or learn the same from part time consultants.

- Poaching on village land can only be controlled by appropriate participation of the villagers themselves. The villages have trained scouts and the District Council is advised to utilise this capacity thus imitating other Districts like Songea, Ruvuma and even the Selous Game Reserve

who are utilising trained village scouts on official tasks that otherwise were supposed to be done by government scouts.
- Collaboration for patrolling/training between SGR, District scouts and village scouts need to be established in order to deter poaching in the area.

**Wild animal monitoring**
Generally monitoring is a continuous assessment of functioning and thus it is an internal part of the day-to-day management. When we come to wild animal monitoring we would like to make systematic observations of changes in all relevant issues for the better understanding of the existing environment and anticipation on new expected situations. REMP has raised the capacity to do this and each village has trained village scouts, village leaders and plant identifiers among the villagers. What is required now is to set up a monitoring system, which will tell them what and when to do it by whom. This will also specifically require the District Game Officer to conduct external monitoring as part of his routine activity.

Formation of a good monitoring system requires a stakeholder workshop where an overview of objectives and formulation of indicators can be facilitated. It is therefore recommended to:
- Run a stakeholder workshop to discuss and develop a monitoring system in each village.
- Currently use a monitoring sheet with spaces to fill to supplement the need of a notebook in patrol.
- Deliberately attempt to establish a village baseline data (situation analysis and basic functions of the wildlife resources and its habitat) as earlier recommended by Jane K. Turpie, (2000) on use and values of natural resources of the Rufiji floodplain and Delta.
- More practical exposure to the villagers on interpretation of GPS readings into map readings as well as training on data organisation and storage

**Patrol implementation**
Stakeholder participation in village level planning is very important in devising ways to tackle all project issues. Newly trained village scouts and leaders need support from the District Game Officer and/or District Lands, Natural Resources and Environment Officer. It is recommended that:
- The support the villagers need to facilitate their responsibilities in patrol need to be identified in a stakeholder workshop where all important stakeholders will be required to discuss and agree on a common action plan with clear roles and responsibilities for each spelled out and agreed upon.
- Issues like patrol uniform, identification cards and the need to acquire a firearm cannot be neglected.
- Local training on practical implementation of by-laws, arresting defaulters and legal aspects thereof as well as training on patrol data collection and reporting is considered to be sufficient for current implementation in the village. And can be conducted by any scout who has formerly attended a Game Assistant Course at Pasiansi.
- The scout appointees need to get an elaborate training to match their counterparts.

**Stakeholder co-ordination**
Stakeholder identification has always been done during management planning at District level. Planning workshops are normally short but of crucial importance to sustainability of a project. It is therefore important to review VEMP plans at village level annually and make sure all stakeholders especially the most important ones i.e. those that can have an effect to VEMP implementation, attend and participate fully.
It is therefore recommended to:
- Short-list all known and expected stakeholders and an analysis conducted to establish the importance and influence of each to the village plan.

- Include all key stakeholders in the village level planning process.

**Village significance and wild animal enterprising**
All the pilot villages have a potential to wildlife enterprising but this needs further development to enhance area significance. In order to be able to do this the need to have a clear knowledge on the wild animal populations and ecosystem aspects cannot be skipped. Capacity exists to do this at village level at least in the wild animal aspect.
It is therefore recommended:

- To monitor the animal numbers and their movements
- The pilot villages lure neighbours to start conservation on their village lands
- District council collaborate with villagers in the so-called "Mloka Open Area" to control wild animal poaching and request the rest of the villages to emulate the pilot villages

**Implementation of basic Wildlife Management Area guidelines.**
The villages are bound to follow the current draft Wildlife Management Area guidelines, unlike the pilot villages of the Selous Conservation Programme like Ngarambe. While other issues like the village land jurisdiction are being dealt with as proposed in 6.1, it is recommended that:

- Formal expression of interest be forwarded to the Director of Wildlife. The procedure is the Village Assembly to agree in accordance to the Village Land Act No. 5 of 1999 and through the Village Council informs Director of Wildlife. The intent shall be in the form of a letter accompanied by the minutes of the Village Assembly meeting that endorsed the plan. The information may conveniently be channelled through the normal channels i.e. the Ward and District Council.
- The villages are advised to establish neighbourhood contact meetings with adjacent villages and raise awareness on uses and values of the wildlife resource as a step towards collaborative management of the wild animal resources. This can also be discussed in Ward Development Committee meetings.

**Village Aquatic resources**
A general survey needs to be done to establish the potentiality of the crocodiles and terrapins in Mtanza/Msona, Mbunju/Mvuleni and Twasalie village fresh waters. This survey requires a special boat with a glass pane so that the surveyor can identify and count the water resources in the village waters especially in the lakes. However if potential is established then, a management arrangement other than the existing may be required.

It is therefore recommended to:

- Discuss the matter with the villages responsible to find out their consent on the matter pre-hand
- The success of Mtanza/Msona, Jaja and Twasalie in the control of fishing gear and getting revenue from the fishery resource need to be emulated by their counterparts in Mbunju/Mvuleni and other villages in the district.

**Village forest resource**
REMP working with the Rufiji District Council has built capacity at village and District levels in natural resources management. It is now the turn of the District Council to tap the acquired capacity. It is therefore recommended that:

- The District Council assists the villages by opening up a District Forest Reserve register and acknowledge the Village Forest Reserve as required by law. Section 40 of the Forest act 2002 provides for this.
- On part of expertise the District Council is obliged to give professional advice to the village concerning the management of the forest estate.

# Table of Contents

**Muhtasari** .......... i

**Executive Summary** .......... vi

**1 Vijiji** .......... 1

1.1 Mtanza Msona .......... 1
1.2 Kijiji cha Mbunju/ Mvuleni .......... 4
1.3 Kijiji cha Twasalie .......... 8
1.4 Jaja Village .......... 11
1.5 Maoni ya jumla .......... 15

**2 Warsha ya kuitaarifu EMT matokeo ya kazi** .......... 26

**3 Hitimisho** .......... 27

3.1 Suala la mipaka ya kijiji .......... 27
3.2 Migogoro ya binadamu na wanyamapori .......... 27
3.3 Uwindaji wa wanyamapori kwenye ardhi za kijiji .......... 28
3.4 Ufuatiliaji wa wanyamapori .......... 28
3.5 Utekelezaji wa Doria .......... 28
3.6 Uratibu wa wadau .......... 29
3.7 Kufanya biashara ya wanyamapori vijijini .......... 29
3.8 Utekelezaji wa miongozo ya maeneo ya usimamizi wa wanyamapori .......... 30
3.9 Rasilimali za maji za kijiji .......... 31
3.10 Rasilimali ya misitu ya vijiji .......... 31

**4 Mapendekezo** .......... 33

4.1 Suala la mipaka ya kijiji .......... 33
4.2 Migogoro ya wanyamapori na binaadamu .......... 33
4.3 Uwindaji wa wanyamapori kwenye ardhi ya kijiji .......... 34
4.4 Ufuatiliaji wa wanyamapori .......... 34
4.5 Utekelezaji wa doria .......... 34
4.6 Uratibu wa wadau .......... 35
4.7 Umuhimu wanyamapori kwa vijiji na biashara ya wanyamapori .......... 35
4.8 Utekelezaji wa miongozo ya maeneo ya usimamizi wa wanyamapori. .......... 35
4.9 Rasilimali za kwenye maji vijijini .......... 36
4.10 Rasilimali ya misitu ya kijiji .......... 36

**5 Viambatisho** .......... 37

5.1 KIAMBATISHO 1: Madhumuni na Majukumu ya Ushauri Kulingana na Hadidu Rejea .......... 37
5.2 Kiambatisho 2: Utaratibu wa Safari ya Kwanza .......... 40
5.3 Kiambatisho 3: Utaratibu wa Safari ya Pili .......... 42
5.4 Kiambatisho 4:Mpato yatokanayo na Uwindaji wa Kujkimu Katika Kijiji Cha Ngarambe .......... 44
5.5 Kiambatisho 5: Mfano wa Formu ya Kutunzia Taarifa ya Ufuatiliaji wa Wanyamapori .......... 45
5.6 Kiambatisho 6: Orodha ya Watu Tuliokutana Nao/Waliotoa .......... 46
5.7 Kiambatisho 7: Maombi Ya .......... 59
5.8 Kiambatisho 8: Madaraja Ya Wafanya Biashara Ya Nyara .......... 62
5.9 Kiambatisho 9: Mfano wa Kamati ya Ushauri ya Ardhi Maliasili na Mazingira, Washiriki na Majukumu Yao 63
5.10 Kiambatisho 10: Utarabiu wa Mafunzo ya Walinzi Wa Wanyamapori Wa Kijiji .......... 64

# 1 Vijiji

## 1.1 Mtanza Msona

Kijiji cha Mtanza/Msona ni mojawapo ya vijiji vilivyoko upande wa magharibi wa tambarare ya mafuriko la Mto Rufiji. Makazi ya watu kwenye kijiji hiki yapo upande wa kaskazini mwa Mto Rufiji, lakini maeneo ya kilimo yapo kusini wa mto. Eneo la makazi ni sehemu ndogo tu, na kwa kawaida eneo hili huwa haliathiriwi na mafuriko. Kwa hiyo wanakijiji huwa wanamiliki nyumba mbili, moja ni katika eneo la makazi na nyingine kwenye eneo la mashamba. Kwa mujibu wa takwimu za halmashauri ya wilaya inakisiwa kwamba kijiji kina kaya 343 na zinaongezeka kwa kasi ya asilimia 1.3 kwa mwaka. Kijiji kimegaiwa katika maeneo kadhaa ya usimamizi, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa mazingira wa kijiji. Kwa hivyo kijiji kina maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya misitu ya hifadhi, misitu ya matumizi, maeneo ya kilimo, maeneo ya makazi, maeneo ya maji na maeneo ya wanyama pori.

Inakisiwa kwamba kijiji kina upana wa kilomita 12 kutoka kusini ambako kinapakana na Hifadhi ya Wanyamapori ya Selous hadi kaskazini kinakopakana na wilaya ya Kisarawe. Kijiji bado hakijapimwa lakini kina eneo kubwa, ambalo linakisiwa kuwa na ukubwa wa 300 $km^2$. Kijiji pia kinapakana na kijiji cha Nyaminywili kwa upande wa mashariki na upande wa magharibi kinapakana na kijiji cha Mibuyu Saba. Pamoja na kwamba mikutano ya uhusiano mwema imefanyika, kijiji cha Mtanza/Msona bado hakijaupatia ufumbuzi mgogoro wa mpaka wake na kijiji cha Nyaminywili. Pia hawajafanikiwa kusawazisha matatizo kama ya mpaka wa kaskazini na Kijiji cha Vikumburu kilichopo wilaya ya Kisarawe. Vilevile mpaka baina ya kijiji na Hifadhi ya Wanyamapori ya Selous bado unamatatizo.

Kuanzia mwezi Agosti hadi Disemba ya kila mwaka kijiji cha Mtanza/Msona huwa na wanyama pori wengi. Wanyama hawa huvutiwa na kuwepo kwa mabwawa na madimbwi yenye maji pamoja na malisho katika ardhi ya kijiji. Wanyama wanaokuwepo kijijini kwa wakati huo huwa ni, tembo, simba, nyati, viboko, mamba, chui, nyumbu, twiga, pundamilia, swala, tohe, digidigi, mbawala, sungura, fisi, mbweha, ngawa, kudu, pofu, kongoni, kuro, nungunungu, vicheche, chindi, nguruwe mwitu, ngiri, nyani, kima weusi, tumbili, mbega, makobe, kenge, pakamwitu, na aina mbalimbali za nyoka na ndege. Kwa kuwa kuna wanyama wengi basi uwindaji ni shughuli ya kawaida kwenye kijiji hiki. Si wawindaji wote wanaoripoti kwenye ofisi za kijiji na kwa hiyo inadhaniwa kwamba uwindaji wao si halali. Wawindaji kutoka Kisarawe na Dar es Salaam huwinda upande wa kaskazini wa kijiji na watalii huwinda kwenye upande wa kusini wa kijiji.

Isipokuwa kwa vijana wachache ambao ni wavuvi, wanakijiji waliobakia wanamashamba na wanachukulia kwamba kilimo ndio shughuli yao muhimu ya kiuchumi. Kwa wanakijiji wengi uvuvi ni shughuli ya ziada. Samaki hupatikana kwa wingi zaidi mara baada ya mafuriko, pengine ni kwa sababu ya kuongezeka kwa maji. Maliasili nyingine ambazo ni za umuhimu kwa wanakijiji ni pamoja na nguzo kwa ajili ya ujenzi, miti ya mbao, kuni, magogo ya kutengeneza mitumbwi na ukindu. Wanakijiji pia huvuna mazao ya porini ambayo hutumika kama chakula. Haya ni pamoja na nafaka, mizizi, majani na matunda. Mazao haya ni muhimu kwa wanakijiji hasa baada ya mafuriko kwa vile yanakuwa ni sehemu muhimu ya chakula.

Wanakijiji hulima mazao mbalimbali kwenye mashamba yao. Haya ni pamoja na mpunga, mahindi, korosho, embe, maboga, miwa, ndizi na mboga mboga. Msimu wa kilimo unaanza Oktoba/Novemba na huishia mwezi Mei ambao ni wakati wa mavuno. Wakulima, haswa wanawake, hutumia muda mrefu kwenye mashamba yao kuliko kwenye nyumba zao zilizoko kwenye eneo la makaazi. Kwenye miaka ya mafuriko wakulima hutumia kilimo cha mlao ambacho ni kilimo kinachofanyika mara tu baada ya mafuriko kumalizika, na aina ya mazao yanayolimwa ni mahindi, maboga na mbogamboga. Eneo la kaskazini, ambalo lina rutuba kidogo na huzalisha mazao kidogo, wakulima hulima mpunga kwenye maeneo chepechepe.

Wakati wa kutembelea mashamba, mshauri aliona kwamba, mashamba ya wanakijiji yanaukubwa wa kati ya hekta 0.4 hadi 1.2. Matokeo haya yanafanana na yale ya Turpie (2000) ambaye alisema kwamba kwa wastani mashamba yana ukubwa wa hekta 0.77 hadi 1.2 kwa kila kaya. Wakulima wengi walieleza kwamba wanaongeza ukubwa wa mashamba yao kufuatana na kuongezeka kwa idadi ya wake walionao. Kufuatana na desturi za wakulima wa Mtanza/Msona kila mke alieko kwenye kaya huwa anahudumia shamba lake. Mashamba haya huwa na ukubwa wa kati ya hekta 0.4 hadi 0.6. Udogo wa mashamba haya na uzalishaji mdogo – magunia 10 hadi 20 ya mpunga kwa hekta – hautoshelezi mahitaji ya chakula kwa kaya kwa mwaka.

Usalama wa chakula kijijini hapa ni dhaifu, kwa sababu, pamoja na uzalishaji mdogo kilimo chake kinatumia teknolojia duni na kinaathiriwa sana na kiwango cha mafuriko kwa mwaka. Mafuriko yakiwa mengi sana au kidogo sana huwa yanaathiri uzalishaji kwa kiwango kikubwa. Juu ya hayo wanyamapori, hususan tembo na nyati hufanya uharibifu mkubwa, kiasi cha kuzifanya familia zinazoathirika kukosa mazao na kutegemea samaki na vyakula vya porini. Mamba ni tatzo jenginne zito, hasa kwa sababu wanakijiji wanautegemea mto na maziwa kwa maji ya kunywa, uvuvi na usafiri.

### 1.1.1 Kutambulishwa kijijini

Ikiwa ni sehemu ya kujizoeza na maeneo ya mradi, mshauri, Bw. Haji Mkungura na viongozi wa kijiji walitembelea kituo cha Mtemere kilichomo kwenye eneo la Matambwe la Hifadhi ya Wanyamapori la Selous na kukutana na mkuu wa kituo Bw. Fadhili Seif. Eneo la Matambwe ndipo pia yalipo makao makuu ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Selous. Kulifanywa mazungumzo kuhusu ushirikiano baina ya wanavijiji na maafisa wa kituo. Mjadala ulihusu uendeshaji wa doria ya pamoja kati ya wanavijiji na walinzi wa hifadhi, na pia kulijadiliwa suala la mawasiliano baina ya kijiji na Hifadhi ya Wanyamapori ya Selous.

Baadae msafara wa mshauri na viongozi wa kijiji ulirudi kijijini. Ramani ya kijiji ilifunguliwa na mwanakijiji mmoja aliongoza utambuzi wa rasilimali za kijiji kwenye ramani. Takribani kila mwanakijiji alionekana kufahamu thamani ya rasilimali mbalimbali zilizopo kijijini. Karibu kila mwanakijiji alikuwa anaouelewa wa matatizo wanayo pambana nayo. Tatizo kuu likiwa ni wawindaji wenye vyombo vya moto na migogoro ya mipaka ya vijiji. Wanakijiji wamekuwa wakijitahidi kutatua migogoro ya mipaka. Kwenye mkutano huo wanakijiji walisema kwamba, pamoja na kutumia mikutano ya ujirani mwema, pia wameomba msaada kutoka ofisi ya ardhi ya halmashauri ya wilaya.

Halmashauri ya kijiji inakutana mara kwa mara lakini mahesabu ya fedha za kijiji huwa hayazungumzwi pamoja na kwamba wanakijiji wamepatiwa mafunzo ya uongozi uendeshaji wa serikali. Baadhi ya wanakijiji wanahisi kwamba viongozi wa kijiji hawafanyi kazi zao sawasawa na kwa hiyo wamefungua kesi ambayo inahoji matumizi na udhibit wa fedha za kijiji. Kesi hii imefunguliwa kwenye ofisi ya Kata. Walinzi (skauti) wa maliasili wa kijiji wamepewa jukumu la kutekeleza sheria ndogo za kijiji zinazohusu maliasili, majukumu hayo yanajumuisha ukusanyaji mapato na kufanya doria kwenye ardhi ya kijiji.

Makadirio ya mahitaji ya mafunzo kwa wanakijiji yalifanyika na mpango wa utekelezaji wa kazi za kijiji uliandaliwa. Baadae kulifanyika mikutano miwili ya kujadili matokeo ya kazi ya utafiti huu. Mikutano hi ilitarajiwa kuwakutanisha wanakijiji wote na maazimio yatokanayo na mkutano huo yalipangwa kuwa yawasilishwe kwenye halmashauri ya kijijini hapo siku za usoni.

### 1.1.2 Kutembelea mashamba

Jioni ya siku ya kwanza mshauri akifuatana na Bw Juma Mkungura, Bw. Mbonde – Afisa Wanyamapori Msaidizi, pamoja na kundi la wanakijiji, walivuka mto na kwenda upande wa kusini ambako walilala kwenye eneo la mashamba. Usiku wa siku hiyo, nyati walivamia mashamba. Watu walijaribu kuwafukuza kwa kuwapigia kelele. Asubuhi yake walitembea

kwenye eneo la Mchangini hadi kwenye mpaka wa sasa wa pori la Hifadhi ya Wanyamapori ya Selous. Wakati wa matembezi hayo, kulitolewa mafunzo juu ya uendeshaji na nidhamu ya doria pamoja na ukusanyaji wa taarifa muhimu kwa ajili ya ufuatiliaji na kuweka kumbukumbu.

### 1.1.3 Ziara na doria kwenye msitu wa kijiji

Mshauri na wenzake walizuru msitu wa hifadhi wa kijiji pamoja na maeneo yanayodaiwa kuwa yanamilikiwa kiasili na kijiji. Eneo la Msigani lilionekana kuwa linatumiwa sana kwa shughuli za uwindaji, ambao huenda ukawa unafanywa na wasasi wa mwisho wa wiki, kwa kuwa siku ya ziara ilikuwa ni jioni ya Jumatatu. Haikuwezekana kufanya shughuli ya kuhesabu wanyama, ambayo ilipangwa kufanyika wakati wa ziara hii, kwa sababu wanyama walikuwa bado hawajahamia kwenye maeneo yaliyotembelewa. Mikuatano kadhaa ya dharura ilifanyika ili kuweza kupima uwezo wa maeneo ya kijiji kuhuisha wanyama pori.

### 1.1.4 Mikutano ya Hadhara

Mikutano miwili ya hadhara ilifanyika kujadili matokeo ya shughuli za ziara na mijadala iliyofanyika kijijini. Kwenye kijiji cha Mtanza/Msona wananchi hawakushiriki sana kwenye kazi za ziara, na Mwenyekiti wa Kijiji alikubali kuitisha mikutano ili kujadili na kuamua masuala mahususi kama vile utumiaji wa fedha za vijiji kununulia silaha. Mkutano wa kwanza ulijadili matokeo ya shughuli za mshauri kuanzia siku ya mwanzo alipofika kijijini hadi siku ya kutembelea mashamba. Siku ya pili mkutano ulijadili shughuli nzima ikiwemo kuzungumzia ziara kwenye maeneo ya misitu na doria. Ufuatao ni muhtasari wa mijadala na maoni ya washiriki. Majina ya washiriki hao yapo kama Kiambatisho Nambari 6.

### 1.1.5 Suala la Mipaka ya kijiji

Ilikubaliwa kwamba suala la ufafanuzi wa mipaka ya vijiji ni lazima liendelee sambamba na utekelezaji wa shughuli nyingine. Kwa mfano, mpaka wa kaskazini, ambao hauna matatizo usizuwie utekelezaji wa shughuli nyingine kama vile mipango ya kutumia wanyama pori walioko walioko kwenye ardhi au misitu ya kijiji.

Mikutano ya ujirani mwema baina ya kijiji cha Mtanza/Msona na vijiji vya Vikumburu na Nyaminywili ingefaa ikaendelea kufanyika ili kurahisisha na kuimarisha ushirikiano baina ya vijiji.

### 1.1.6 Kusajiliwa kwa misitu ya hifadhi ya kijiji

Utaratibu unatayarishwa ili kusajili Msitu wa Hifadhi wa Kijiji wenye eneo la mita za mraba 107.3 ambao uko kaskazini mwa mto. Jambo linalochelewesha shughuli hii ni kwamba Afisa Misitu wa Wilaya analipa suala hili uzito mdogo, na kwamba baadhi ya madiwani wanadai kwamba msitu huo ni msitu wa halmashauri ijapokuwa hausimamiwi ipasavyo kama ambavyo inahitajiwa na sera ya taifa ya misitu. Hata hivyo urasimu huu unaochelewesha usajili usisababishe kupuuzwa utekelezaji wa shughuli nyingine za kusimamia msitu wa kijiji, kama vile doria na ulinzi wa misitu. Hasa ikichukuliwa kwamba Sheria ya Misitu ya mwaka 2002 inasema kwamba msitu utahifadhiwa ikiwa baraza la kijiji litaazimia kutenga sehemu ya ardhi ya kijiji kuwa msitu wa hifadhi.

### 1.1.7 Doria za kuzuia ujangili

Kijiji kimeamua kuweka utaratibu wa kuanzisha mawasiliano na kituo cha Mtemere kwa ajili ya kupata msaada, hasa pale ambapo kutakuwepo majangili wenye bunduki au pale itakapoonekana kwamba uvamizi wa wanyamapori unazidi nguvu za kijiji. Mkuu wa kituo cha Mtemere Bw. Fadhili Sefu, aliahidi kusaidia moja kwa moja au kwa kufanya mawasiliano na Kitengo cha Kuzuia Ujangili

kilichopo Dar es Salaam au kwa kuwasiliana na Afisa Wanyamapori aliepo Utete. Hata hivyo mipango ya kina ya kutekeleza maamuzi ya ushirikiano bado haijatayarishwa.

### 1.1.8 Udhibiti wa wanyama waharibifu

Washiriki wa mikutano ya hadhara iliyojadili kazi ya mshauri waliamua kwamba inunuliwe bunduki ya kijiji, kwa sababu kijiji kinao walinzi wanne waliofunzwa, na sheria inawaruhusu kutumia silaha. Wamesema kwamba kutafuta fedha za kufanyia shughuli hii halitokuwa tatizo hasa ikichukuliwa kwamba, kijiji kinaidai halmashauri ya wilaya kiasi cha shilingi laki tatu. Wakitambua kwamba kiasi hiki hakitotosha kununua silaha hiyo, wanafikiria kuongeza fedha hizo kwa kutumia mapato yanayokusanywa kutokana na vibali vya uvuvi. Mwezeshaji wa mpango wa mazingira wa kijiji, Bi. Pili Mwambeso, alisema kwamba halmashauri ya wilaya imeahidi kulilipa deni la kijiji wakati wowote mwaka huu. Wanakijiji wanafahamu pia kwamba wanahitaji kupata ruhusa kutoka kwenye Baraza la Kijiji ili kuweza kutumia fedha za kijiji kununua silaha hiyo.

### 1.1.9 Kueleza msimamo wa kuvuna wanyama pori waliopo kwenye ardhi ya kijiji

Moja ya shughuli zilizopangwa kwenye mpango wa usimamizi wa mazingira wa kijiji ni matumizi ya busara ya rasilimali ya wanyama pori. Mpango huu umekubaliwa na baraza la kijiji na umo katika utekelezaji. Wanakijiji wanafahamu kwamba, miongozo ya usimamizi wa maeneo ya wanyamapori au utumiaji wa rasilimali ya wanyamapori waliopo kwenye ardhi/msitu wa kijiji inapendekeza kwamba maamuzi ya kijiji hayana budi kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori. Vile vile wanakijiji wanafahamu kwamba ni lazima waandike barua ya kuelezea utashi wao na kwamba barua hiyo ni lazima iambatanishwe na kumbukumbu za mkutano. Pia wanafahamu kwamba ni jambo la busara kuiwasilisha barua hiyo kwa kupitia ofisi za kata na halmashauri ya wilaya.

## 1.2 Kijiji cha Mbunju/ Mvuleni

Mshauri alikitembelea kijiji cha Mbunju/Mvuleni akifuatana na Bw. Eddy Kilapilo (Afisa Wanyamapori Msaidizi) na Bw. Nandi R. X. (Mwezeshaji wa mpango wa usimamizi mazingira vijijini). Kijiji hiki kipo kwenye eneo la kati la bonde la tambarare, kiasi cha kilomita 70 kwa kutoka makao makuu ya wilaya, Utete. Barabara inayofika kijijini hapa kutoka Utete inajumuisha kuvuka mto kwa kutumia pantoni liliopo kijiji cha Ndundu. Kijiji hiki pia kinafikika kwa kutumia boti au mtumbwi kupitia Mto Rufiji. Hata hivyo, kijiji kipo kiasi cha kilomita 10 kutoka mtoni.

### 1.2.1 Kuhusu kijiji Cha Mbunju/Mvuleni

Mbunju Mvuleni ni moja ya vijiji vilivyopo katika eneo la kati la bonde la tambarare la Mto Rufiji, maeneo ya makazi yapo kiasi cha kilomita 10 kaskazini ya mto. Maeneo haya ya makaazi yamegawika kwenye maeneo mawili Mbunju na Mvuleni ambayo yapo kwenye barabara itokayo Ikwiriri kwenda Mkongo. Mvuleni ipo meta chache kutoka Ziwa Ruwe vilevile eneo la Mbunju lipo meta chache kutoka Ziwa Uba, ambalo linatumiwa kwa pamoja na kijiji cha Mpima. Kwa kawaida wanakijiji wanakuwa na nyumba mbili mbili, moja ikiwa ni nyumba ya kdumu inayokuwa kwenye maeneo ya makaazi na nyingine hujengwa mashambani. Kutokana na takwimu za wilaya za mwaka 1997 kijiji cha mbunju kinakisiwa kuwa na kaya 123, na idadi ya watu inaongezeka kwa kiasi cha asilimia 1.3 kwa mwaka. Ardhi ya kijiji imegaiwa katika maeneo mbalimbali ya matumizi, hii ni moja ya mikakati iliyomo kwenye mpango wa usimamizi wa mazingira wa kijiji. Kwa hiyo kijiji kina maeneo ya misitu ya hifadhi, misitu ya matumizi, maeneo ya kilimo, maeneo ya makazi na maeneo ya maji.

Kijiji hakijapimwa rasmi lakini kina eneo dogo ikilinganishwa na vijiji vingine kama vile Mtanza/Msona. Eneo la kijiji lipo pande zote za mto, upande wa kusini mwa Mto Rufiji, kijiji kinapakana na kijiji cha Utunge/Nyanda na upande wa kaskazini-magharibi kijiji kinapakana na kijiji cha Mng’aru. Tangu kijiji cha Mbunju/Mvuleni kianze kuchukua hatua za kusimamia maliasili zake, migogoro ya mipaka imefumka. Migogoro ipo kwenye mpaka wa magharibi ambako kijiji kinapakana na kijiji cha Ruwe na mashariki ambako kinapakana na kijiji cha Mgomba Kaskazini. Majadiliano ya

kusawazisha migogoro hii yanafanyika na Katibu Mtendaji wa Kata anasaidia katika kutatua matatizo haya.

Kijiji kimebarikiwa kwa kuwa na kiasi kikubwa cha wanyamapori, hasa kwenye miezi ya Agosti hadi Desemba. Idadi kubwa ya wanyama hawa hutoka Hifadhi ya Wanyamapori ya Selous, wakiufuata mto Ruhoi. Misafara hii ya wanyama huendelea kukipita kijiji kuelekea kaskazini kwenda kwenye kijiji cha Mng'aru. Wanyama huvutiwa na kuwepo kwa maji na pengine malisho. Aina za wanyama wanaopatikana ni tembo, simba, nyati, kiboko, mamba, chui, twiga, punda milia, tohe, digidigi, na mbawala. Wingineo ni Sungura, Fisi, Mbweha, Ngawa, Kudu, Kuro, Nungunungu, Cheche, Chindi, Nguruwe mwitu, Ngiri, Nyani, Kima, Ngedere, Mbega, Makobe, Mbalapi, Kenge, Paka mwitu, na aina mbali mbali za ndege na nyoka. Uwindaji ni moja ya shughuli ya kawaida kijijini, lakini kwa kiasi kikubwa unafanyika kinyume cha sheria kwa sababu wawindaji huwa hawaripoti kwenye halmashauri ya kijiji na huwa hawana leseni. Na kwa kuwa kijiji kipo karibu na mji wa Ikwiriri soko la nyamapori huwa ni rahisi kupatikana.

Wanakijiji wengi wanayo mashamba na wanaona kwamba kilimo ndiyo shughuli yao kuu ya kiuchumi. Uvuvi unachukuliwa kuwa ni shughuli ya ziada lakini muhimu, hasa wakati wa vipindi vya njaa. Maliasili nyingine yenye umuhimu kwa wanakijiji ni misitu ambayo hutoa nguzo, mbao, kuni, magogo ya kutengenezea mitumbwi, na ukindu. Pia wanakijiji wamezoea kuvuna vyakula vya porini, ambavyo vinajumuisha nafaka, mazao ya mizizi, majani na matunda. Matunda yanao umuhimu mkubwa pale yanapotokea mafuriko kwa sababu yanakuwa ndio chakula kikuu.

Kijiji kina misitu iliyofunga vyema hasa upande wa kaskazini, magharibi na sehemu za upande wa kaskazini-mashariki. Wakati wa kufanya doria kwenye misitu iliyopo kijijini tuliona wanyama kama vile Mbawala, Mbega na Kima. Uvunaji wa misitu kwenye maeneo ambayo hayakuhifadhiwa ni jambo la kawaida kwenye kijiji hiki. Kijiji kinatoza kodi ya shilingi 2000/= kwa kila mti uvunwao na Shilingi 100/= kwa kila kipande cha ubao. Malipo haya ni juu ya gharama za leseni ambayo hutolewa na Afisa Misitu wa Wilaya. Wanakijiji wamekuwa wakitumia maeneo haya kwa muda mrefu na wanajua mipaka ya asili ya misitu ndani ya kijiji chao. Sasa hivi wanakijiji wanathibitisha ufahamu wa mipaka yao na uwezo wa usimamizi wa rasilimali za misitu. Wanavijiji wameigawa misitu yao kwenye maeneo mawili, misitu ya hifadhi na ile ya matumizi na wanayo nia ya kudhibiti kisheria matumizi ya maeneo hayo.

Maeneo ya kilimo yapo kwenye tambarare la mafuriko kwenye bonde upande wa kaskazini mwa Mto Rufiji ambako mazao makuu yanayolimwa ni mpunga, korosho, embe, maboga, miwa, ndizi na mboga mboga. Msimu wa kilimo unaanza mnamo mwezi wa Oktoba/Novemba na upandaji huendelea hadi mwezi Januari. Msimu huendelea hadi mwezi wa Mei ambapo uvunaji hufanyika. Wakulima, hususan wanawake hutumia muda mwingi  (kiasi cha 2/3 ya mwaka) kwenye mashamba kuliko kwenye makazi yao ya kudumu. Kwenye miaka ya mafuriko, wakulima huwa wanalima kilimo cha mlao, mazao yanayolimwa ni, mahindi, maboga, na mboga mboga.

Wakati wa kutembelea mashamba, mshauri aliona kwamba ukubwa wa mashamba kwa familia ni wastani wa hekta 0.4 hadi hekta 1.2. Matokeo haya yanafanana sana na matokeo ya utafiti wa Turpie (2000), ambaye aliona kwamba kwa wastani mashamba ya familia yana ukubwa wa hekta 0.77 hadi hekta 1.2. Hata hivyo mkulima mmoja aitwae Bw. Saidi Yusufu Ngubege alikuwa na shamba la mahindi lililotunzwa vyema na lenye ukubwa wa hekta 4.8. Ijapokuwa ana wake watatu, lakini umiliki wa bunduki unaweza kuwa ndio sababu kuu iliyomfanya aweze kuwa na shamba lilotunzwa vyema. Mahindi yalikuwa yamepandwa vizuri kwenye mistari iliyonyooka. Wakulima wengi walieleza kwamba huongeza ukubwa wa mashamba yao kufuatana na idadi ya wake walionao. Kufuatana na mila za wakulima wa kijiji hiki, kila mke huwa anaendesha shamba, ambalo huwa na ukubwa wa hekta 0.4 hadi 0.6. Udogo wa mashamba haya na uzalishaji mdogo – magunia 10 – 20 ya mpunga kwa hekta – hauwezi kutosheleza familia kwa mwaka mzima.

Pamoja na uzalishaji mdogo, hali ya upatikanaji wa chakula kijijini hapo pia ni ya wasiwasi, kwa sababu mafuriko makubwa sana au kidogo mno huathiri mfumo wa kilimo, ambacho hufanyika kwa kutumia teknolojia duni. Mbali na mafuriko wanyamapori, hasa tembo, viboko, kima na nyani huharibu mashamba na baadhi ya wakati huwafanya wanakijiji wategemee samaki na vyakula vya porini. Mamba ni tatizo jengine, kwa sababu wanakijiji wanatumia mto na maziwa kwa matumizi mbalimbali yakiwemo usafiri, maji ya kunywa, na uvuvi. Kwa mfano, Mwezi wa Sita mwaka huu, mamba aliua mwanakijiji mmoja kwenye eneo la kijiji cha mvuleni.

### 1.2.2 Kutambua kijiji na uzoefu

Tarehe 28/7/2002 mshauri na Eddy Kilapilo walifika kijijini na kukutana na mwenyekiti wa kijiji ili kujitambulisha na kuelezea lengo la ziara yao. Mwenyekiti alikuwepo na aliona kwamba ingekuwa vigumu kufanya mkutano siku hiyo hiyo kwa kuwa wengi wa watu ambao wangetarajiwa kushiriki walikuwa wakihami mashamba yao dhidi ya wanyamapori. Siku ya pili ilipangwa kuwa ni siku ya mkutano. Mkutano ulipoanza tulijadili mpango wa utekelezaji kazi iliyotupeleka kijijini pale, mijadala ilijumuisha kupanga wakati wa kufanya doria na kutembelea mashamba na washiriki waliombwa kuandika matarajio yao juu ya ziara yetu. Matarajio haya yalijadiliwa na kueleweka na wote. Wakati wa jioni ramani tatu za kijiji zililetwa na wanakijiji walizifasiri ramani na maliasili ziliomo.

### 1.2.3 Ziara za mashambani

Tukiwa kijijini tulizuru maeneo ya Mtumbini na Nyalwala ambako familia 7 za mashambani zilitembelewa. Wakati wa ziara kulifanyika mijadala kuhusu matatizo ya wanyama waharibifu, njia zinazotumika kupunguza hasara na katika kujitetea, mbinu za kilimo zinazotumika na mapendekezo ya jinsi ya kupunguza tatizo la wanyama waharibifu.

### 1.2.4 Ziara na doria kwenye msitu wa kijiji

Kulifanyika ziara kwenye msitu wa kijiji na doria kwenye eneo la Mbundi. Kwenye eno la Mbundi miti kadhaa ilikuwa imeangushwa na mapande ya magogo yalikuwa yameachwa. Miti yote iliyoangushwa haikuwa imepigwa nyundo (muhuri) ya afisa misitu na hakukuwa na mtu wa kumhoji kama alikuwa na leseni au la. Hata hivyo, inawezekana eneo lenyewe lilikuwa nje ya mipaka ya kijiji, kama ambavyo walinzi wa msitu walivyosema, lakini mwenyekiti wa kijiji alidai kwamba eneo hilo lilikuwa ndani ya mipaka ya kijiji. Wakati wa ziara, ambayo ilichukuwa siku mbili, wanyama walihesabiwa, mipango na nidhamu ya doria ilifanyika. Pia ilifanyika mijadala kadhaa ili kusaidia kutambua na kuainisha uwezo wa uzalishaji wa maeneo ya kijiji.

### 1.2.5 Mikutano ya Hadhara

Kulifanyika mikutano miwili ya hadhara ili kujadili utekelezaji wa shughuli yote. Mkutano wa kwanza ulijadili matokeo ya ziara kuanzia siku ya utambulisho hadi siku ya ziara ya mashambani, na mkutano wa pili ulihitimisha safari yote ikijumlisha ziara za na doria kwenye msitu wa kijiji. Yafuatayo ni muhtasari wa majadiliano na maoni ya wanakijiji walioshiriki kwenye mikutano ya hadhara.

### 1.2.6 Suala la mipaka ya kijiji

Mwenyekiti wa kijiji alieleza kwamba msaada zaidi unahitajika kutoka ofisi ya ardhi ya kijiji ili kuondosha migogoro ya mipaka. Alisema kwamba, wamewasilisha tatizo hili kwenye kamati ya mazingira ya wilaya (EMT), pia alieleza kuwa mikutano ya ujirani mwema ambayo itakuwa ikiwezeshwa na afisa ardhi wa wilaya imepangwa kufanyika mnamo mwaka 2003. Hata hivyo, wengi wa washiriki walikuwa na maoni kwamba, migogoro ni kikwazo kikubwa kwenye usimamizi wa maliasili za kijiji. Kwa hiyo walipendekeza na kukubaliana kuwa na mkutano wa ujirani mwema na kijiji cha Utunge nyanda. Wakati huo huo, wataendelea kufuatilia maombi yao yaliyopelekwa kwenye ofisi ya Katibu Mtendaji Kata, ya kutafutia ufumbuzi tatizo la mipaka ya magharibi na mashariki.

### 1.2.7 Uwezekano wa kurekebisha misitu ya hifadhi ya kijiji

Kijiji kimetenga rasmi eneo la kilometa za mraba 12.22 kuwa ni msitu wa hifadhi wa kijiji. Ijapokuwa kijiji kilishiriki kikamilifu kwenye upimaji wa msitu wa kijiji, baadhi ya wanakijiji wanahisi kwamba mpaka wa kaskazini mashariki si sahihi. Kwa hiyo wangependa kufanyike marekebisho na kujumuisha maeneo ya matumizi ya msitu kiasi kwamba kwenye mpango wa usimamizi maeneo haya mawili yanakuwa tofauti. Wanakijiji walifikiri kwamba kwa njia hii watakuwa na hakika ya kuhibiti misitu iliyomo kwenye ardhi yao, tofauti na hali ya sasa ambapo wanahisi kwamba inawabidi wagawane faida zitokanazo na misitu ambayo haimo kwenye maeneo ya misitu ya hifadhi lakini inapendekezwa kusajiliwa. Wanakijiji wanaona kwamba mara tu msitu utakaposajiliwa kama ni msitu wa hifadhi wa kijiji utakuwa chini ya miliki yao kama ilivyokuwa hapo siku za nyuma chini ya usimamizi wa machifu. Sasa hivi, magogo na mbao zinazovunwa nje ya msitu wa hifadhi zinalipiwa ushuru wa shilingi 2000/= kwa gogo na Sh 100/= kwa kipande cha ubao. Inafahamika kwamba Afisa Misitu wa Wilaya hulipwa pesa nyingi zaidi kwa kila leseni anayotoa kwa wavunaji. Mti mmoja hutoa magogo mawili hadi matatu lakini unaweza kuwa na meta za ujazo kadhaa. Leseni ya kuangusha miti inagharimu kati ya shillingi 30000/= hadi 80000/= kutegemeana na aina (kabila) ya miti.

### 1.2.8 Doria za kuzuia uwindaji haramu

Wanakijiji wanahisi kwamba, walinzi wa wanyama pori wa kijiji wanahitaji bunduki ili waweze kupambana na wawindaji wenye silaha. Katika hali ya sasa hivi ambapo hawana bunduki, huwa wanategemea msaada wa afisa wa wanyama pori wa wilaya ambaye yuko mbali na hana vifaa vya kutosha. Kwa hiyo, wanahisi kwamba kuna haja ya kuwa na bunduki ili kuweza kupambana na wawindaji wenye silaha.

### 1.2.9 Kupambana na wanyama waharibifu

Wanakijiji waliamua kwamba walau kungenunuliwa wavu wa kuwakamata wanyama waharibifu, hasa nguruwe mwitu, nyani, na kima ili kupunguza idadi yao. Tatizo ni jinsi ya kupata fedha za kwa ajili ya kununua wavu huo ambao unagharimu kiasi cha Shilingi 200,000 kwa wavu wenye meta 150. Kuhusu mamba na viboko kuna haja ya kuwa na bunduki, kwa hiyo wana mipango ya kununua bunduki ili waweze kupunguza kutegemea msaada wa afisa wa wanyama pori wa wilaya. Wanapanga kutumia rasilimali ya samaki ili kuweza kupata fedha za kununulia bunduki hiyo.

### 1.2.10 Uvunaji wa wanyama pori

Wanakijiji wameelezea kupendezewa kwao na kutumia wanyama pori waliomo kwenye msitu wao wa hifadhi. Ijapokuwa wamezungumzia suala hili mara kadhaa, bado hawajaomba ruhusa rasmi. Kwa hiyo wameamua kuandika maombi rasmi kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori ili kuelezea utashi wao. Vilevile wanafahamu kwamba maombi yao inabidi yapitie kwa halmashauri ya kata na halmashauri ya wilaya ili kurahisisha utekelezaji.

### 1.2.11 Kuboresha mawasiliano na uongozi

Kwa muda mrefu sasa utekelezaji wa kazi wa walinzi wa maliasili wa kijiji umevurugika na kwa hiyo umepunguza mshikamano na ufanisi baina yao. Hili lilielezwa mnamo siku ya mwanzo ya mafunzo wakati kamati ya mazingira ya kijiji ilipoeleza wasi wasi kwamba, rekodi za doria si za ukweli. Pamoja na kwamba walinzi walimchagua kiongozi wao rasmi, doria hazifanyiki ipasavyo na mipango ya doria imeghairishwa mara kadhaa kwakuwa baadhi ya washiriki hawakuwa wakifika kwenye malindo kwa siku na wakati uliopangwa.

Wakati wa ziara mapungufu haya yalijionyesha kwa walinzi kushindwa kuutambua mpaka wa kaskazini wa msitu wa hifadhi wa kijiji na badala yake mabishano yakazuka. Baadae wakati wa mkutano ilionekana kwamba ni vyema kulitafutia ufumbizi tatizo la uongozi. Kwa hiyo mshauri aliamua kufanya upembuzi wa haraka kwa kutumia tathmini shirikishi na kuona kwamba tatizo kubwa ni kukosekana kwa mawasiliano. Kwa hiyo mkutano ukaiomba kamati ya mazingira ya kijiji

kulifuatilia suala hili kwa kumteua kiongozi wa walinzi atakae hakikisha kwamba ratiba za doria zinafuatwa na ripoti zinaandikwa. Hii itaupa nguvu utekelezaji wa kanuni zote, zikiwemo za uvuvi, ambazo zipo lakini hazitekelezwi. Katika hali hiyo hiyo vifaa vya mradi, pamoja na ukusanyaji na usimamizi wa mapato utafanikiwa ikiwa tu kila mwanakijiji atashiriki.

Kulikuwa na utaratibu wa kuweka rekodi, lakini kwa muda mrefu sasa umekuwa haufuatwi. Wanakijiji walitaka walinzi wote wawajibike na wabadili nyendo zao. Pia walitaka utaratibu utakaohakikisha ufuatiliaji wa kamati ya mazingira ya kijiji na halmashauri ya kijiji kuwa tayari na kufuatilia utekelezaji. Vilevile walifikiri kuwa na karatasi ya ufuatiliaji, ambayo juu ya kuandika matokeo ya doria pia itahakikisha taarifa mahsusi kadhaa zinarekodiwa ili kuwezesha ufuatiliaji. Pamoja na kuzisajili taarifa kwenye kitabu cha rekodi, ile karatasi ya ufuatiliaji ijazwe na ripoti iandikwe.

### 1.2.12 Utaratibu wa kutekeleza mipango ya mazingira ya kijiji

Wanakamati wa kamati ya mazingira ya kijiji walisema, kanuni za udhibiti wa maliasili zimewekwa lakini hakuna sheria za kuwashughulia wanaokataa kutekeleza mipango iliyowekwa, kama vile kufanya doria. Wanakijiji walikubali kutayarisha na kutekeleza utaratibu huo baada ya kupitishwa na baraza la kijiji.

### 1.2.13 Usimamizi wa moto.

Moto wa misitu na nyika unasemekana kuwa ni suala la kawaida na wanakijiji waliokuwa kwenye mkutano wa hadhara wanahisi kwamba kuchoma moto mwanzoni mwa majira ya kiangazi na kuudhibiti kunaweza kusaidia kuleta uoto ambao ni muhimu kwa malisho ya wanyama pori. Hili, hatahivyo, halijaingizwa kwenye mpango wa mazingira wa kijiji. Shughuli hii itasaidia kupunguza hatari za moto mkali unaoweza kuwaka wakati wa majira ya kiangazi, ambao huwaka kila mwaka kijijini hapo. Wanapanga kuanza kuitumia mbinu hii kwenye mipaka ya msitu wa kijiji, lakini baadae wataitumia kama ilivyolezwa hapo juu.

### 1.2.14 Kuweka alama za mipaka ya misitu ya hifadhi ya kijiji

Kwenye baadhi ya maeneo ambako mipaka ilikuwa haijapakwa rangi, itabidi kazi hii lazima imalizike na alama ziwekwe na kuonyesha mipaka ya msitu wa kijiji ili iweze kutambuliwa vyema na wageni. Kwa kuwa hii ni shughuli iliyopangwa lakini haikutekelezwa, mwenyekiti wa kijiji alitaka kwamba kamati ya mazingira ya kijiji kupeleka maombi rasmi kwenye serikali ya kijiji ili iweze kupata msaada wa fedha.

### 1.2.15 Kuleta mwamko wa uhifadhi kwenye vijiji vya jirani

Kwakuwa inafahamika kwamba mipaka ya kijiji haijumuishi mfumo mzima wa ki-ikolojia ilipendekezwa kwamba kijiji kingevishawishi vijiji vyengine vya jirani kuanzisha juhudi za kuhifadhi kwenye vijiji vyao. Mwenyekiti alisema, vijiji kama Ruwe na Mng'aru vilikuwa vimepanga kuanza shughuli kama hiyo kwenye vijiji vyao.

## 1.3 Kijiji cha Twasalie

Kijiji cha Twasalie kipo upande wa kaskazini wa delta. Inachukuwa kiasi cha masaa manane kufika kijijini hapo kuoka Utete ikiwa utasafiri kwa boti yenye hosipawa 40 kutoka Utete. Safari hiyo inaweza kuchukua muda mrefu zaidi kwa kuwa inategemea kina cha maji kwenye mto. Baadhi ya wakati inabidi kuweka kambi kwa usiku mzima njiani ili kusubiri maji yajae. Mshauri akifuatana na Bw. Juma Mkungura (Afisa wanyama pori msaidizi) walikitembelea kijiji hicho mnamo tarehe 10/11/2002. Safari ya boti inakufikisha hadi bandari ya Tarachu, baada ya hapo inabidi kutembea kwenye mashamba ya mpunga ili kufika kwenye makazi ya watu kijijini.

### 1.3.1 Utangulizi

Kijiji cha Twasalie kina eneo la makazi katikati ya kisiwa cha Twasalie. Kijiji hiki kinapakana na kijiji cha Msala kwa upande wa mashariki, kijiji cha Maparoni kwa upande wa kusini, na kwa upande wa magharibi kinapakana na vijiji vya Mtunda, Mchinga na Mfisini. Kwa upande wa kaskazini magharibi, kijiji kinapakana na kata ya Salale na kwa upande wa kaskazini mashariki kinapakana na bahari ya Hindi, kijiji cha Kiomboni na kijiji cha Kiasi. Mikutano kadhaa ya ujirani mwema imefanyika ili kuweza kukubaliana mipaka ya vijiji. Mafanikio yamepatikana kwenye mipaka na baadhi ya vijiji lakini bado kuna matatizo kwenye mipaka na vijiji vya Msala, Mtunda, Kiomboni, Mchinga na Mfisini. Kijiji hiki kina vitongoji vitano ambavyo ni Poroti, Domwe, Kisimba, Tarachu na Nyahimba. Kutokana na takwimu za halmashauri ya wilaya za mwaka 1997 kijiji kina watu 1955, kwenye kaya 325 na idadi inaongezeka kwa kasi ya asilimia 1.3 kwa mwaka.

Moja ya mikakati utekelezaji wa mpango wa mazingira wa kijiji inajumuisha kukigawa kijiji kwenye maeneo ya usimamizi. Kwa hiyo kijiji kimeigawa ardhi ya kijiji kwenye misitu ya hifadhi ya kijiji, misitu ya matumizi, maeneo ya kilimo na maeneo ya makazi, maeneo yenye maji, na maeneo ya wanyama pori. Misitu ya kijijini hapo ni misitu ya mikoko ambayo imehifadhiwa kisheria. Kijiji kinaingia kwenye makubaliano na idara ya misitu na nyuki kuwa kwenye usimamizi wa pamoja wa misitu hiyo.

Wanyama pori wanopatikana kijijini hapo ni pamoja na simba, viboko, mamba, tohe na mbawala. Wingineo ni sungura, cheche, chindi, nguruwe mwitu, ngiri, nyani, kima, tumbili, kenge, paka mwitu, na aina mbalimbali za nyoka na ndege. Kwa sababu ya kuwepo wanyama hawa kwenye ardhi ya kijiji na pamoja na nyati kwenye baadhi ya miaka, uwindaji wa wanyama pori kwenye kijiji ni jambo la kawaida. Mara kwa mara viboko wanawindwa kwenye kitongoji cha Domwe na nyama huuzwa kijijini au hupelekwa Mtunda ambako ndiko wanakotoka wawindaji wa viboko. Halmashauri ya kijiji haina desturi ya kudhibiti uwindaji wa wanyama pori kijijini na kwa hiyo nyama huuzwa kijijini mbele ya walinzi (skauti) wa maliasili wa kijiji. Wakati wa mkutano mwanakijiji mmoja alisema kwamba nyumba ya mlinzi mmoja huwa inatumika kama soko la kuuzia nyama ya wanyama pori, na katika hali ya kushangaza mlinzi huyo alisema kwamba hakujua kwamba alikuwa anavunja sheria kwa kufanya hivyo.

Shughuli kuu za kiuchumi kijijini hapo ni kilimo na uvuvi. Wakulima wengi wanachukulia kuwa kilimo ni shughuli ya msingi na uvuvi ni shughuli ya ziada. Sehemu kuu za kilimo ni maeneo yalioko mabondeni karibu na maeneo ya makazi na kitongoji cha Domwe. Eneo kuu la makazi pia hutumika kwa kilimo. Mazao muhimu ya kilimo kwenye kijiji yanatofautiana kufuatana na eneo, kwa mfano, kwenye eneo la makazi mazao yanayolimwa ni minazi, miembe, na mikorosho. Kwenye kitongoji cha Domwe, mikoko ilikuwa imekatwa ili kuweza kulimwa mpunga, mahindi na miwa. Mabonde yaliyopo karibu na makazi ya watu kijijini ni maeneo muhimu kwa kilimo cha mpunga. Uvuvi hufanyika kwenye Mto Tarachu na Mto Bomba ijapokuwa wavuvi wachache huvua kwenye Bahari ya Hindi. Kiwango cha chumvi kwenye maji kinabadilika kufuatana na masafa kutoka baharini na majira ya mwaka, kipindi cha mvua huwa na chumvi kidogo kulinganisha na msimu wa kiangazi. Hii ina maana, kwenye baadhi ya maeneo maji yanakuwa si ya chumvi na hivyo huwa ni nmakazi ya viboko, mamba na samaki wa maji baridi. Kwenye baadhi ya maeneo maji yamechanganyika na hivyo kuweka aina ya viumbe wanaoweza kuhimili hali hiyo. Kibanju, ambayo ni sehemu inayopakana na kijiji ni kambi ya uvuvi na inajulikana sana kwa uvuvi wa kamba.

Wakulima wa kijiji hiki, kwa kawaida, hulima maeneo madogo yenye eneo la kiasi cha eka moja (0.4ha) na kilimo chenyewe huwa kinatumia teknolojia duni. Mashamba mengi ya mikorosho yameachwa kuota vichaka, ni wakulima wachache tu wanaojali mikorosho yao. Ilielezwa kwamba sababu kubwa inayopelekea hali hii, ni uharibifu unaofanywa na kima na nyani. Kilimo cha minazi vilevile kina matatizo kwa kuwa miti mingi inakufa kutokana na maradhi, ambayo labda husabishwa na virusi, lakini pia uharibifu wa kima na nyani unaweza kuwa ni sababu.

Wanyamapori wanalaumiwa kuharibu kiasi cha robo ya kila eka inayopandwa mpunga. Na kama isingekuwa kulindwa kwa mashamba hayo basi mazao yote yange kuwa yanaharibiwa na wanyama mwanzoni mwa msimu. Uharibifu wa minazi ni mbaya zaidi kwani kuharibiwa na kima na nyani hupelekea kupoteza mazao yote. Kwa mfano Ngedere wanakula usiku na mchana na kwa hiyo inakuwa vigumu kuwadhibiti wakati wa kiza na kwa kuwa wao wanaishi juu ya minazi. Kwa wastani Mazao muruwa kutoka kwenye mnazi mmoja ni nazi hamsini (50) kwa kila miezi mitatu (3), hii ina maana kwamba mkulima anaweza kuvuna nazi 200 au zaidi kutoka kila mnazi kwa mwaka.

### 1.3.2 Kutambulishwa na kukielewa kijiji

Walipofika Tarachu, siku ya tarehe 9/12/2002 mshauri na Bw Juma Mkungura, wakifuatana na wanavijiji pamoja na Bw. Mpili ambaye ni baharia wa boti, walikwenda kijijini na kumtafuta mwenyekiti wa kijiji. Baada ya mazungumzo mafupi kulifanyika mkutano na wanavijiji waliokuja kusikiliza tulichokuwanacho. Baada ya kujitambulisha, ramani mbili za kijiji zilifunguliwa na wanakijiji wakaongoza shughuli ya kuzifasiri ramani na kuonyesha rasilimali zilizopo. Baadae tulijadili utaratibu wa kutekeleza kazi iliyotupeleka na washiriki waliombwa kuandika matarajio yao kuotakana na ziara yetu. Matarajio yalijadiliwa na kueleweka na wote.

### 1.3.3 Ziara za mashambani

Matembezi yalifanyika kwenye kitongoji cha Domwe wakati tukirudi kutoka kwenye Doria. Kaya tano (5) zilitembelewa. Majadiliano yalifanyika kuhusu matatizo ya wanyama waharibifu, mbinu zinazotumika kupunguza hasara na katika kujitetea, mbinu za kilimo na mapendekezo ya kupunguza au kuondosha tatizo la wanyama waharibifu.

### 1.3.4 Ziara na Doria kwenye msitu wa kijiji

Ziara zilifanyika kwenye msitu wa hifadhi wa kijiji na pia doria zilifanyika kwenye maneo ya Mbalanyimbo na Ngatola. Jumla ya nguzo 1,520 za mikoko (Korija 76) zilikamatwa kwenye matukio matatu (Mbalanyimbo zilikamatwa nguzo 280, na Ngatola zilikamatwa nguzo 1,200 na eneo la Kijamundu zilikamatwa nguzo 40). Wenye nguzo hizo hawakukamatwa, isipokuwa wale wa Mbalanyimbo. Taarifa hizi zilipelekwa kwa afisa wa mikoko wa wilaya huko Nyamisati kwa hatua zaidi. Wanakijiji bado hawajapewa jukumu la kuwaadhibu wahalifu pale wanapowakamata. Wanakijiji wamefundishwa jinsi ya kufanya doria na kuwakamata kihalali watu wanaovunja sheria. Hii ni pamoja na kukagua maeneo husika, kuweka kumbukumbu za hali, rasilimali na yote waliyoyaona kwenye eneo walilolitembelea.

### 1.3.5 Mikutano ya Hadhara

Mkutano mmoja wa hadhara ulifanyika ili kujadili masuala yatokanayo na utekelezaji. Mkutano huu ulifanyika siku ya mwisho ya ziara na ilikuwa na lengo la kuhitimisha kazi yote iliyofanyika. Yafuatayo hapo chini ni muhtasari wa majadiliano na maoni ya washiriki wa mkutano.

### 1.3.6 Suala la mipaka ya kijiji

Washiriki walihisi haja ya kufuatilia suala la mipaka ya magharibi ambako kinapakana na vijiji vya Mtunda, Kiomboni, na mashariki ambako kinapakana na kijiji cha Msala. Zaidi ya hayo ilikubaliwa kwamba mikutano ya ujirani mwema ni lazima ipangwe na kufanyika haraka. Kwa hiyo ufuatiliaji wa baraza la kijiji linatakiwa kufuatilia, kwa kupitia ofisi ya katibu kata wa Maparoni, upangaji wa mkutano mwingine wa ujirani mwema.

### 1.3.7 Msitu wa hifadhi wa kijiji

Msitu wa hifadhi wa kijiji una eneo la kilomita za mraba 169.87 (16,987 ha) ambazo sehemu kubwa ni msitu wa mikoko. Utaratibu unatengenezwa ili kuwezesha mpango wa usimamizi wa pamoja baina ya vijiji na idara ya misitu na nyuki. Wanakijiji wanahisi kwamba utaratibu huu unachukua muda mrefu na hadi sasa hawajakubaliana mipaka ya usimamizi (uendeshaji). Hata hivyo Bw. F. Sima (Afisa

Mikoko wa Wilaya) alieleza kwamba mapendekezo ya mpango huo yapo ofisini kwa mkurugenzi wa idara ya misitu na nyuki ili kuidhinishwa kabla ya hatua nyingine hazijachukuliwa.

### 1.3.8 Doria za kuzuia ujangili

Washiriki wa mkutano walisema kwamba, doria hazifanyiki kama inavyotarajiwa. Zaidi ya hayo wanahisi kwamba halmashauri ya kijiji, kamati ya mazingira ya kijiji, na walinzi wa maliasili hawajaona kwamba uwindaji haramu kuwa ni tatizo. Kwa hiyo wakawataka walinzi na kamati ya mazingira ya kuchukua jukumu na kujitolea zaidi na kuongeza idadi ya doria hadi kiasi cha walau mara mbili kwa mwezi. Vilevile, ilikubaliwa kwamba walinzi lazima wapewe chakula siku wanapofanya doria, pia walinzi ambao hawajafunzwa ni lazima washirkishwe kwenye kazi za doria ili kuongeza nguvu za doria.

Zaidi ya hayo walitaka kwamba kila mwanakijiji ashiriki kikamilifu katika kuwakamata majangili, jambo hili ni lazima lihusishe ubadilishanaji taarifa baina ya vijiji. Doria kama hizo zitasaidia kudhibiti uvunaji usio halali wa msitu wa hifadhi wa kijiji na hata katika maeneo ya misitu ya matumizi. Hali hii itahakikisha ukusanyaji wa mapato kutokana na ukataji miti kutoka msitu wa matumizi wa maeneo ya Mtomboro na Khembwa.

### 1.3.9 Udhibiti wa wanyama waharibifu

Washiriki walitaka kwamba mpango wao wa kununua nyavu ya kutega wanyama waharibifu utekelezwe. Hata hivyo, halmashauri ya kijiji haikijaweza kupata fedha zinazotakiwa kwa shughuli hiyo. Wakasema kwamba halmashauri ya kijiji inabidi ionyeshe matumizi ya michango iliyofanyika kwa kipindi cha miaka mitatu kabla hawajaanza kuchangia tena. Akijibu hoja hii, mwenyekiti wa kijiji alisema kwamba tayari kuna mpango wa kuwasilisha hesabu za kijiji kwenye baraza la kijiji litakalofanyika tarehe 16/11/2002.

Kuhusu tatizo la mamba, washiriki walifikiri kwamba ikiwa watapatiwa marisao wangeweza kutumia bunduki zao binafsi kusaidia kudhibiti tatizo la wanyama waharibifu. Marisao waliyonunua mwaka jana kutoka idara ya kilimo na mifugo ya wilaya yalikuwa sio mazuri na mengi yao hayakufanya kazi.

## 1.4 Jaja Village

Kijiji cha cha Jaja kipo kusini mwa delta, kiasi cha kilometa 60 ukisafiri kwa mto kutoka Utete makao makuu ya halmashauri ya wilaya ya Rufiji. Mshauri pamoja na Juma Mkungura (Msaidizi Afisa Wanyamapori) walikitembelea kijiji cha Jaja wakitokea Twasalie mnamo tarehe 15/11/02. Safari ilichukua masaa sita (6) kwa sababu maji yalikuwa yamejaa na hivyo kusafiri bila ya kusimama. Barabara ya karibu inafika hadi Muhoro. Mnamo siku ya tarehe 18/11/02 waliongezeka Bw. R. X. Nandi (mwezeshaji wa mipango ya mazingira ya kijiji), Bw. Haji Mkungura (Msaidi afisa wanayama pori) na Bi Rose Hogan (Mshauri wa kiufundi – Maendeleo ya Jamii) ambao walikuja kwa gari hadi kwa kupitia njia mpya inayotengenezwa kuelekea kijiji cha Ruma. Wakati mshauri akirudi kutoka ziara ya mashambani huko King'ongo aliwachukua kutoka Ruma, ambapo ilikuwa safari ya chini ya nusu saa hadi Jaja. Wakati barabara hii itakapokwisha itakuwa maendeleo makubwa yatakayorahisiha mawasiliano baina ya Jaja na makao makuu ya wilaya, Utete.

### 1.4.1 Utangulizi

Kijiji cha Jaja kimeundwa na visiwa vitatu, yaani Jaja, Ulaya na Bedeni. Makazi mengi yapo kwenye visiwa vya Jaja na Ulaya. Kisiwa cha Bedeni hakina watu wanaoishi, lakini ni muhimu kwa makazi ya ndege (hasa Yangeyange) na tondo, ambao wanatumika kutengenezea choka na chambo cha samaki. Kijiji kinapakana na Bahari ya Hindi kwa upande wa mashariki, Kijiji cha Pombwe kwa upande wa kusini, kijiji cha Kiongoroni kwa upande wa magharibi na kijiji cha Mbwera kwa upande wa kaskazini.

Kutokana na takwimu za mwaka 1997 za halmashauri ya wilaya za mwaka kijiji kina watu 1,376 walio kwenye kaya 206 na idadi inaongezeka kwa kasi ya asilimia 1.3 kwa mwaka.

Moja ya mikakati ya utekelezaji ya mpango wa mazingira wa kijiji inajumuisha ugawaji wa maeneo ya kijiji. Kwa hiyo kijiji kimeigawa ardhi ya kijiji kwenye maeneo mbalimbali ya usimamizi (uendeshaji). Kuna maeneo yaliyoainishwa kama ni maeneo ya hifadhi, yakiwemo misitu ya mikoko ya Kilobani, matumbawe na kisiwa cha Bedeni. Msitu wa mikoko ni makaazi ya kima ambao ni wanyama pori waliopo kijijini. Maeneo ya kilimo yapo Mpendeni na King'ongo kwenye Kisiwa cha Ruma na baadhi ya maeneo ya Visiwa vya Jaja na Ulaya ambako pia kuna makazi. Maeneo mingine yaliyogaiwa ni maeneo ya maji, hasa Mto Mkongo na eneo la Pwani.

Wanyamapori muhimu wanaopatikana kijijini ni pamoja na kima, ngedere, nguruwe mwitu, ngiri, na tohe. Wingineo ni sungura, cheche, chindi, nyani, paka mwitu, kenge, na aina mbalimbali za nyoka na ndege. Kuna ujangili unaofanyika, hasa kwenye maeneo ya mashamba watu huwinda tohe. Simba, viboko na fisi huonekana mara chache kwenye kijiji cha Ruma. Ruma ni eneo kuu la kilimo kwa wakulima wote wa Kiongoroni. Visiwa vya Jaja na Ulaya havifai sana kwa uzalishaji wa chakula kwa sababu ardhi yake ni ya kichanga na udongo wake una kiwango kikubwa cha chumvi chumvi. Mazao makuu yanayolimwa Jaja ni Minazi, Miembe, mikorosho, mboga mboga na viazi vitamu. Ng'ombe, mbuzi, na kondoo pia hufugwa kwenye visiwa hivi.

Wanakijiji wanaona kwamba kilimo ndiyo shughuli yao kuu ya kiuchumi na eneo kuu la kilimo ni King'ongo na Mpendeni yaliyoko kwenye kijiji cha Ruma. Maeneo haya ya kilimo yapo mbali na makazi ya watu na inabidi watumie mitumbwi kuyafikia. Wakulima kwenye maeneo haya wanalima mpunga, mahindi, mboga mboga na viazi vitamu. Mashamba mengi yaliyotembelewa yalikuwa ni madogo na wastani wa hekta 0.4 kwa kaya yenye mwanamke mmoja, mumewe na watoto. Mwanaume mwenye zaidi ya mke mmoja, kwa kawaida, anakuwa na shamba kubwa kwa sababu kila mwanamke huwa analima kipande chake. Ijapokuwa kilimo kinaweza kutumia mashine, lakini watu hawatumii mbolea na wakulima wengi wanahama mashamba baada ya kulima kwa muda wa miaka mitatu hadi mitano, ambapo uzalishaji unapungua na magugu huongezeka.

Kulinda mashamba dhidi ya wanyama waharibifu ni kazi inayochosha na ijapokuwa wakulima wengi wana nyumba za kudumu kisiwani Jaja na/au Ulaya, lakini huwa wanatumia zaidi ya 2/3 ya muda wao kwa mwaka wakiwa kwenye maeneo ya mashamba. Wanyama waharibifu kwenye kijiji hiki ni mbawala, kima, ngedere. Nyani, Tohe, Ngiri na Nguruwe mwitu. Baadhi ya wakati wanyama waharibifu huwa ni pamoja na viboko, simba na fisi ambao baadhi ya miaka huvamia mashamba.
Wanakijiji wengi wanaziona shughuli za utengenezaji chumvi na uvuvi kama ni shughuli za ziada. Hata hivyo, kuna wakulima wachache, hususan wavuvi vijana, ambao huchukulia uvuvi kama ni shughuli kuu na ya msingi kwa maisha yao. Utengenezaji chumvi hufanyika sana kwenye Kisiwa cha Ulaya kwenye majangwa ya chumvi. Chumvi huuzwa kwa fedha taslimu au kwa kubadilishwa na mazao kama mahindi au mpunga. Vilevile, pamoja na umuhimu wa uvuvi kwa baadhi ya wakazi lakini wavuvi wengi hawaendi kuvua kwenye bahari kuu kwa sababu hawana nyenzo sahihi kwa shughuli hii, kama vile majahazi. Ni kawaida kwa meli za kigeni zinazofanya uvuvi wa kokoro kuvua ndani ya mipaka ya kijiji.

Kijiji kimebarikiwa na maeneo makubwa ya mikoko. Vilevile kuna baadhi ya miti ya mivinje inayoota kwenye baadhi ya maeneo ya kijiji. Kwa kuwa kijiji kinafahamu kwamba misitu ya mikoko imehifadhiwa kisheria, basi kimeanza utaratibu kushiriki kwenye usimamizi wake chini ya mpango usimamizi wa pamoja kwa kushirikiana na idara ya misitu na nyuki, chini ya mpango wa uendeshaji shirikishi wa misitu. Utaratibu unafanyika kukamilisha jambo hili na ramani ya msitu wa hifadhi wa kijiji imechorwa na maeneo ya misitu ya matumizi yametengwa na mistu hiyo huvunwa kwa ruhusa itolewayo kwa kupatiwa leseni na kibali kutoka kijijini. Miti mingi inayovunwa husafirishwa hadi Dar es Salaam na Zanzibar.

### 1.4.2 Kutambulishwa na kuzowea kijiji

Walipofika Jaja siku ya tarehe 15/11/2002, mshauri na Bw. Juma Mkungura wakifuatana na Bw. Mpili walikwenda ofisi ya mazingira kujaribu kukutana na katibu wa kamati ya mazingira ya kijiji. Wakati katibu wa kamati ya mazingira anafika ili kuitikia wito wetu tayari kulikuwa na kundi la uongozi wa kijiji na wanakamati ya mazingira ambao walikusanyika kutusalimu. Baada ya kujitambulisha, mshauri na Bw. Juma Mkungura pamoja na watu wingine waliokuwepo walipanga kufanya mkutano wa kufahamiana kwa siku inayofuata tarehe 16/11/2002. Mijadala isiyo rasmi kuhusu mpango wa mazingira wa kijiji na mahitaji ya mafunzo ilifanyika. Katika hali ambayo si ya kushangaza, wakati wa mijadala hiyo ilifahamika kwamba wanakijiji walikuwa wanajitayarisha kwa mafunzo ya utawala ambayo yalikuwa yamepangwa. Baadhi ya wanakijiji walikuwa na duku duku la kutaka kujua ni lini mafunzo haya yatafanyika.

Siku ya tarehe 16/11/02, mwenyekiti wa kamati ya mazingira ya kijiji Bw. R. Mng'ombe na msaidizi katibu wa kamati walileta ramani ya kijiji. Baada ya kujitambulisha kwa mshauri na Bw. Juma Mkungura na wanakijiji walioshiriki kwenye mkutano, Bw. Mng'ombe aliongoza ufasiri wa ramani na kuonyesha rasilimali zilizomo. Wanavijiji wengi wanaweza kufasiri ramani na kutambua rasilimali zao, lakini hawakuweza kuandika maelezo marefu kuhusu rasilimali hizo.

Mjadala wa kina ulifanyika kuhusu rasilimali za kijiji, thamani ya rasilimali hizo na matatizo ambayo wankijiji wanakutana nayo kwenye utekelezaji wa mpango wa mazingira wa kijiji. Msisitizo maalum uliwekwa kwenye suala la wanyamapori pamoja na makazi yao. Thamani ya rasilimali za kijiji kama vile matumbawe ya Kipwa Mtumbuka na Kisiwa cha Bedeni yalizungumzwa kwa undani. Baada ya kuzipitia juhudi za wananchi katika kuondoa au kupunguza matatizo wanayokumbana nayo, mpango wa shughuli zitakazofanyika wakati wa ziara ulitengenezwa. Siku ya tatu ilipangwa kuwa ni siku ya ziara na doria kwenye msitu wa Kilobani, Makao na Kisiwa cha Bedeni. Siku ya nne ilipangwa kuwa ni ya ziara za mashambani huko maeneo ya King'ongo na Mpendeni kwenye kijiji cha Ruma. Siku ya tano na ya sita zilipangwa kuwa ni siku za mafunzo kijijini na siku ya saba ilikuwa ni mkutano wa hadhara. Baadae, mpango uliongezwa na siku ya nane ili kufanya ziara ya Mpendeni, ambayo haikuweza kufanyika kwenye wakati uliopangwa na siku ya tisa ilikuwa ni ya kufanya safari kurudi Utete.

### 1.4.3 Ziara za mashambani

Siku mbili zilitumika kuzuru maeneo ya kilimo ya kijiji cha Ruma. Siku moja ilitumika kutembelea King'ongo na siku moja kutembelea eneo la Mpendeni. Familia kumi zilitembelewa. Mijadala ilifanyika kuhusu matatizo ya wanyama waharibifu, hasara zinazotokana na uharibifu, mbinu zinazotumika kupunguza hasara na kujilinda, aina ya kilimo, na mapendekezo ya kuondoa au kupunguza matatizo ya wanyama waharibifu. Mshauri na wakulima walibadilishana mawazo ili kuwa kama ni mafunzo zaidi kuhusu udhibiti wa wanyama waharibifu.

### 1.4.4 Ziara na doria kwenye msitu wa kijiji na maeneo mingine yaliyohifadhiwa kijijini

Mshauri na Bw. Juma Mkungura wakifuatana na wanavijiji sita walitembelea msitu wa hifadhi wa kijiji na kufanya doria kwenye maeneo ya Makao na Kilobani. Vilevile ilifanyika ziara kwenda Kisiwa cha Bedeni, ambacho kimehifadhiwa. Maeneo ya Kipwa Mtumbuka ambayo pia yamehifadhiwa, hayakutembelewa, ijapokuwa Bi. Rose Hogan aliyatembelea maeneo hayo siku ya tarehe 21/11/02 wakati mshauri alipokuwa anaendesha mkutano wa kuwasilisha matokeo ya shughuli nzima kwa wanakijiji.

Kwenye eneo la msitu uliofungwa wa Kilobani, mtu mmoja Bw. Rajabu Saidi Mnema wa kijiji cha Kiongoroni alikutwa akikata fito za mikoko na alikuwa ameshakusanya fito 161. Baada ya kukamatwa, yeye na mtumbwi wake na fito zilizokamatwa, zilipelekwa kijijini ambako sheria ndogo zingetumika kulishughulikia suala hilo. Wakati wa doria, kikundi cha doria kilifunzwa jinsi ya kufanya doria, kumkamata na jinsi ya kumshughulikia muhalifu. Hii ikiwa ni pamoja na kuweka kumbukumbu za jinsi mtu alivyokamatwa. Mafunzo ya jinsi ya kutathmini maliasili pia yalifanyika.

### 1.4.5 Mikutano ya hadhara

Mkutano mmoja wa hadhara ulifanyika ili kujadili masuala yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji. Mkutano ulifanyika siku moja kabla ya siku ya mwisho ya ziara, kwa lengo la kupata matokeo ya kazi yetu na kuhitimisha ziara nzima. Yafuatayo ni muhtasari wa mijadala na maoni ya washiriki wa mkutano.

### 1.4.6 Suala la mipaka ya kijiji

Washiriki walihisi kwamba kuna haja ya kufanya mikutano ya ziada ya ujirani mwema, ili kulitafutia ufumbuzi suala la mpaka wa pamoja na kijiji cha Pombwe na Kiongoroni ambao una utata. Vilevile ilikubaliwa kwamba, mipaka ya kijiji iliyopo baharini iainishwe na ioneshwe kwenye ramani ili kuweza kulinda matumbawe ya Kipwa Mtumbuka ambayo yamehifadhiwa kwa ajili ya utalii huko siku za usoni.

### 1.4.7 Msitu wa hifadhi wa kijiji

Msitu wa hifadhi wa kijiji una eneo la kilometa za mraba 13.18 (1318 ha) ambazo nyingi zao ni mikoko. Kunatayarishwa utaratibu wa kuingia kwenye usimamizi wa pamoja na Idara ya Misitu na Nyuki katika misingi ya usimamizi shirikishi. Uamuzi wa kuwa na msitu wa hifadhi wa kijiji ni wazo lililoletwa na mkurugenzi wa misitu na nyuki kwa kupitia mradi wa mikoko na kupokelewa na kijiji. Ilikubaliwa kwamba juhudi za makusudi zifanyike kwa ajili ya kuongeza uwelewa wa sera mpya na faida zitakazopatikana baada ya utekelezaji. Pamoja na kuongeza uwelewa mipaka inabidi iwekewe alama na mabango yawekwe ili kuonyesha mambo gani yanaruhusiwa na mambo gani hayaruhusiwi kufanyika ndani ya msitu uliohifadhiwa.

### 1.4.8 Doria za kuzuia ujangili

Washiriki wa mkutano walikuwa na maoni kwamba doria zilikuwa hazifanyiki na wakosefu walikuwa hawashughulikiwi kama ilivyokubaliwa na wanakijiji. Wanahisi kwamba serikali ya kijiji haina nguvu na kwamba kijijini kuna upendeleo. Zaidi ya hayo walisema kwamba hakuna mahusiano mema na ushirikiano kati ya kamati ya mazingira ya kijiji na halmashauri ya kijiji. Hali hii, walisema wanakijiji, inapelekea uvunaji haramu wa nguzo na fito za mikoko, hivyo kukikosesha kijiji mapato. Vilevile kukosa kuletewa boti ambayo waliahidiwa, kumewafanya kushindwa kufanya doria kwenye maeneo ya mbali kama vile kwenye eneo la matumbawe la Kipwa Mtumbuka. Hali hii imesababisha eneo hili kuendelea kuvamiwa na kutumika na wavuvi kutoka nje ya kijiji. Mwezeshaji wa mpango wa usimamizi mazingira wa kijiji Bw. R. X. Nandi aliwaeleza kwamba, kwakuwa boti iko tayari basi injini italetwa kijijini kwenye ziara nyingine ambayo imepangwa kufanyika tarehe 16/12/02. Washiriki walisema kuwa, ikiwa ni hivyo basi doria itabidi iongezwe nguvu na serikali ya kijiji ijirekebishe na iwe na maadili mema ya utendaji.

### 1.4.9 Kudhibiti wanyama waharibifu

Wanakijiji amabo walishiriki kwenye mkutano wa hadhara wa marejesho walitaka juhudi za kuwasaka wanyama waharibifu kwenye eneo la mashamba ni lazima ziendelee. Pia walihisi kwamba kuna haja ya kufanya shughuli hiyo kwenye visiwa vya Jaja na Ulaya, kwanza kwa kufanya sensa ya wanyama na halafu kuamua kima wangapi wapunguzwe. Hii ni kwa ajili ya kulinda thamani ya kuwepo kwa wanyama pori kwenye ardhi ya kijiji.

### 1.4.10 Kuongeza uwelewa wa faida za kuhifadhi mazingira kwa wanakijiji wa Jaja na vijiji vya jirani

Washiriki walikuwa na maoni kwamba bado kuna baadhi ya wanakijiji na wananchi wingine kutoka vijiji vya jirani ambao wanahisi kwamba mradi unawasukuma kukubali kujibana kwenye matumizi ya maliasili ambazo zamani walikuwa wakizipata bure. Kwa hiyo iliamuliwa kwamba, juhudi za kuongeza uwelewa wa wanakijiji kuhusu mipangilio mipya ni lazima ufanyike kwenye kijiji.

## 1.5 Maoni ya jumla

Wanyamapori ni moja kati ya rasilimali za kibaiolojia na hivyo usimamizi wa wanyama pori ni usimamizi wa rasilimali za kibaiolojia ikiwa ni sehemu ya usimamizi wa mzingira. Usimamizi wa mazingira ni jambo linalochukua muda mrefu kuonyesha matunda yake. Moja ya kikwazo kikubwa tunachokumbana nacho kwa sasa ni jinsi ya kupata fedha za kuendeshea shughuli hii na kubadilisha mawazo ya watu kutoka kuwa watumizi wa maliasili hadi kuwa wahifadhi wa mazingira. Hali hii inatuweka njia panda katika historia ya ustaarabu wa binadamu. Hii ina maana kwamba matendo yetu ya miaka michache ijayo yataamua kwamba tunaelekea kwenye matatizo na uharibifu wa maliasili au kuchukua njia mbadala ambayo itatupelekea kuwa na bioanuwai na matumizi endelevu ya rasilimali za kibaiolojia. Sasa hivi Tanzania ipo katika kipindi cha mpito na mageuzi ya jinsi ya kusimamia rasilimali pamoja na majukumu na haki za kutumia rasilimali mbalimbali. Sera zinazoongoza mabadiliko haya ni mpya na watu wengi wanaotarajiwa kuzitekeleza wanahitaji kupatiwa mafunzo ya jinzi ya kuzitumia ili kufikia hali enedelevu.

Kwa kufuatana na sera mpya, matarajio ya MUMARU yanalenga kufikia matumizi ya busara ya maliasili pamoja na uendelevu wa mazingira, hii inajumuisha usimamizi bora wa wanyamapori. Hili ndilo lililopelekea kufanyika kazi hii ya ushauri. Wakati akiwa vijijini mshauri alikaguwa mambo kadhaa yanayohusu usimamizi bora wa wanyama pori. Mada zifuatazo zinatowa muhtasari wa jumla ya mambo yaliyoangaliwa na kupimwa.

### 1.5.1 Masuala ya mipaka ya vijiji

Katika kuweka mipaka ya vijiji vyao ikiwa ni sehemu ya utayarishaji wa mpango wa usimamizi wa mazingira ya vijiji, vijiji vya mfano vimejikuta vikikumbana na matatizo na migogoro kadhaa. Lakini kwa kusaidiwa na MUMARU vijiji hivi vimepata mafanikio makubwa kwenye kutatua migogoro hiyo, hata hivyo bado kuna migogoro inayoendelea. Migogoro ambayo haijapatiwa ufumbiuzi ni kama ifuatavyo

**Kijiji cha Mtanza/Msona.** Kijiji hiki kina migogoro kwa mipaka yake iliyo upande wa kusini na upande wa mashariki. Kijiji hiki kinapakana na Hifadhi ya Wanyamapori ya Selous. Wanakijiji wanahisi kwamba kuna mgogoro kwenye mpaka wao wa kusini ambao unapakana na Hifadhi ya Wanyamapori ya Selous. Mpaka huu upo kiasi cha kilometa 4 kusini mwa Mto Rufiji. Wanakijiji wanalalamika kwamba, hawakushirikishwa wakati mpaka huo ulipokuwa unawekwa mnamo mwaka 1997/98. Kabla ya hapo wao walikuwa wanaujua mpaka mwingine ambao upo kusini zaidi. Mpaka mpya umewafanya wao kutoweza kuzifikia maliasili ambazo zamani walikuwa wakizipata bure, kwa mfano maziwa na magogo ya kutengenezea mitumbwi.

Tangu mpaka mpya uwekwe kumekuwa na migongano kati ya wanakijiji na walinzi wa hifadhi ya Selous, hususan kwenye eneo lilochukuliwa na mpaka mpya lijulikanalo kama Mchangini. Suala hili la tatizo la mpaka lilijadiliwa mnamo mwaka 1997/98 wakati wa mkutano wa kata za Mkwaseni na Ngorongo ambao uliitishwa na madiwani na kuhudhuriwa na viongozi wa serikali wakiwemo wale wa hifadhi ya Selous. Ajenda kuu kwenye mkutano huo ilikuwa kupanga mbinu za ushirikiano kwa ajili ya usimamizi wa wanyamapori kwa vijiji vyote vinavyopakana na hifadhi ya Selous. Baada ya mkutano huo, kulifanyika ufuatiliaji kwa wanakijiji wa Mtanza/Msona kwenda Dar es Salaam kwenye ofisi ndogo ya hifadhi ya Selous baada ya hapo kulifanyika mkutano mwingine na pia kufanya ziara kwa kuruka na ndege ili kulikaguwa eneo lenye mgogoro kutoka angani.

Wanakijiji bado hawajaridhika na matokeo ya mikutano hiyo na wanahisi kwamba ni vyema wangeambiwa tangu mwanzo kwamba eneo lile ni mpaka mpya na si barabara kama ilivyoelezwa wakati mpaka huu unawekwa. Sasa hivi walinzi (skauti) maliasili wa kijiji hawawezi kufanya doria kwenye eneo hilo kwa sababu wanawaogopa walinzi wa serikali. Suala lilifuatiliwa na mshauri kwa kuzungumza na Bw. Foya J. wa ofisi hifadhi ya Selous iliopo Dar es Salaam. Kwenye mazungumzo hayo iligundulika kwamba kuna mpaka mpya wa hifadhi ya Selous na ni katika maeneo machache tu, kama vile Mtanza/Msona, ambako nguzo zinazoonyesha alama ya mpaka bado hazijawekwa. Maelezo haya yalithibitisha maelezo yaliyopatikana kwenye mjadala usio rasmi uliofanyika kati ya mshauri na

msimamizi wa upande wa mashariki wa hifadhi ya Selous na mkuu wa kituo cha Mtemere. Viongozi hawa walisema kwamba hifadhi ya Selous inaongeza nguvu kwenye usimamizi, ikiwa ni pamoja na kuweka mipaka. Vilevile ushirikiano na vijiji vya jirani utaimarishwa.
Kijiji cha Nyaminywili kinashirikiana mpaka wa mashariki na kijiji cha Mtanza/Msona.Vijiji hivi viwili havijakubaliana maeneo unamopita mpaka huo. Kuna madai kwamba baadhi ya wanakijiji wa Mtanza/Msona walihamisha moja ya Nguzo zinazoweka alama ya mpaka huo. Jambo hili halijathibitishwa.
Mpaka wa kaskazini wa kijiji hiki vilevile mpaka wa wilaya ya Rufiji na Kisarawe. Hata hivyo utaratibu ni kwa vijiji kukutana na kukubaliana mpaka wao wa pamoja, ambao mara nyingi ni mpaka wa asili bila kujali mipaka ya kiutawala ya wilaya. Ijapokuwa hakuna mgogoro kuhusu mpaka huo wa kaskazini.

**Kijiji cha Mbunju/Mvuleni.** Kijiji hiki kina mgogoro kwenye mipaka yake ya Mashariki, Magharibi, na Kusini. Kwenye baadhi ya maeneo migogoro hii ni maneno tu, kwa mfano mpaka wa kusini ambako kijiji hakikuchukuwa hatua yoyote kwakuwa kinajua eneo linalozungumzwa ni lake tangu asili. Kijiji kinapakana na kijiji cha Utunge/Nyanda kwa upande wa kusini. Wanakijiji wanasema kwamba watu Utunge/Nyanda wanaolima kwenye eneo la kusini wanadai kwamba eneo hilo limo kwenye eneo la kijiji chao. Lakini wanakijiji wa Mbunju/Mvuleni hawajapeleka madai rasmi na serikali ya kijiji cha Mbunju/Mvuleni imeahidi kuifuatilia minong'ono hii na watalijadili suala hili kwenye mikutano ya ujirani mwema na kijiji cha Utunge/Nyanda.
Pia watu kutoka mji wa Ikwiriri huwa wanalitumia eneo hilo kwa kilimo. Zipo kiasi cha kaya 150, baadhi yao ziko kwenye eneo la Mupi tangu miaka ya 80. Wakazi hao hawajasajiliwa kijijini, lakini kwa kuwa wapo hapo muda mrefu na wanatumia ardhi na maliasili nyinginezo wamekuwa na haki ya maeneo haya.
Kijiji cha Mbunju/Mvuleni kinapakana na Kijiji cha Ruwe kwa upande wa Magharibi na mpaka wao bado haujaainishwa. Kwenye mwaka 2001, serikali za vijiji hivi viwili zilifanya mkutano wa pamoja na walikubaliana kuhusu mipaka, ambao baadae ulipingwa na baadhi watu ambao zamani waliishi Mbunju/Mvuleni. Watu hawa waliishi wakati wa "Operesheni Vijiji" na ni dhahiri kwamba wanayo mashamba ambayo yapo Mbunju/Mvuleni na wangependa kuendelea kuyamiliki. Tatizo lao ni kwamba wanaogopa wanaweza kupoteza mashamba yao ikiwa hawakudai kwamba sehemu hiyo ya ardhi ipo kwenye kijiji cha Umwe. Wasiwasi huu unapingana na miongozo ya sera na sheria ya ardhi, pengine wananchi hawa bado hawajafahamishwa. Mtu anayo haki ya kuishi popote na ardhi yote iliyopatikana wakati wa operesheni vijiji huwa inamilikiwa na kijiji kilichofaidika na ardhi hiyo. Wanakijiji wanasema kwamba katibu kata wa Mkongo aliitwa ili kusuluhisha mgogoro huu lakini hakuweza kuutatua.
Upande wa mashariki kijiji kinapakana na kijiji cha Mgomba kaskazini. Mpaka wa kiasili baina ya vijiji hivi unasemekana kuwa kwenye bonde ambako kulikuwa mtii unaoitwa Mgache na nguzo ya mpaka ilikuwa kwenye sehemu inayoitwa Mwenda. Mpaka huu wa asili unadaiwa kuwa ndio mpaka wa sasa wa kata, lakini bado haujathibitishwa na watendaji wa kata mbili zinazopakana.
Mpaka huu unasemekana kukiwacha kitongoji cha Mpima kuwa chini ya utawala wa kijiji cha Mbunju/Mvuleni. Pamoja na hali hiyo kitongoji cha Mpima kinatumia uongozi wa kijiji cha Mgomba/Kaskazini. Ijapokuwa kijiji cha Mgomba kaskazini kinakubaliana na mpaka wa kiasili, lakini bado kitongoji cha Mpima kinadai kuwa ni sehemu ya Mgomba kaskazini na si Mbunju /Mvuleni. Hata hivyo tangu kuwezeshwa na mradi wa MUMARU ili kuwa na usimamizi bora wa Ziwa, kumekuwa na maendeleo makubwa katika kudumisha mahusiano baina ya kitongoji cha Mpima na vitongoji vya Mbunju na Mvuleni. Kitongoji cha Mpima kilishiriki kikamilifu kwenye kuamua wapi unapita mpaka wa msitu wa hifadhi wa kijiji cha Mbunju Mvuleni.

**Kijiji cha Twasalie.** Kijiji bado kina matatizo ya mipaka na vijiji vinne vilivyoko upande wa magharibi mwa kata ya Mtunda. Kama ilivyo kwa vijiji vyengine vya mfano, migogoro imeanza baada ya kijiji kuanza utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa mazingira. Maoni ya wanakijiji kuwa mpaka wa tarafa za Mbwera na Kikale kama mpaka wa asili ndio yamesababisha matatizo. Katibu kata wa

Mtunda alishiriki kwenye mikutano ya ujirani mwema katika kujaribu kutafuta ufumbuzi wa tatizo la mpaka wa kijiji, lakini hawakufikia muafaka. Vilevile mkutano wa ujirani mwema uliofanyika Agosti 2002, haukuleta na makubaliano juu ya mpaka na kijiji cha Salale kilichoko kwenye kata ya Salale. Katibu kata pia alishiriki kwenye mkutano lakini muafaka haukupatikana.

**Kijiji cha Jaja.** Kijiji bado hakijawa na makubaliano kuhusu mpaka wake wa pamoja na kijiji cha Pombwe ambao uko upande wa kusini. Wanakijiji wa Pombwe wanadai sehemu ya kisiwa cha Bedeni. Mkutano wa ujirani mwema ulioitishwa kujadili suala hili haukufanyika. Kijiji pia hakijakubaliana na kijiji cha Kiongoroni kuhusu mpaka wao. Inasemekana kwamba mgogoro ulianza baada ya kijiji cha Jaja kuufunga Mto Mkongo na kudhibiti matumizi yake na baadae kuufungua na kuweka utaratibu wa kuwa na kibali kabla ya mtu hajavua samaki kwenye kwenye mto huo.

Kuhusu mpaka wa mashariki ambao uko ndani ya Bahari ya Hindi, meli za uvuvi zimekuwa zikivua kwenye maeneo ya kijij bila ya wananchi kukubali. Hadi sasa, haieleweki sawa sawa masafa ya mpaka wa kijiji kutoka pwani hadi baharini. Inadaiwa kuwa mpaka wa baharani wa taifa ni kilometa 12 kutoka pwani. Hata hivyo bado kuna maswali yanayohitaji majibu, kwa mfano kuelezea masafa ya mpaka kutoka pwani, na je ni sawa kwa kijiji kutumia mpaka wa taifa kama ni mpaka wao? Je meli zilizopewa leseni na serikali kuu zinatakiwa kuripoti kijijini zikiwa kwenye maeneo ya bahari ya kijiji? Meli za uvuvi hazipendwi na takriban na wanakijiji wote, ijapokuwa kuna baadhi ya wanakijiji wanaouza mazao yao kwa mabaharia wanaotoka kwenye meli hizo, na wingine hununua samaki wanaovuliwa na meli hizo ambao wana pengine wangetupwa na kuachwa waoze. Haya yamwefikiwa baada ya majadiliano ya muda mrefu, lakini bado inadaiwa kwamba faida wanayopata wanakijiji ni ndogo ikilinganishwa na uharibifu mkubwa wa mazingira unaosababishwa na meli za uvuvi.

### 1.5.2 Migogoro ya watu na wanyama pori

Ijapokuwa idadi ya wanyama pori haijulikani na wala hakuna takwimu za wanyama wanaotoweka, lakini tangu MUMARU uanze kazi vijijini humo, kwa ujumla idadi ya wanyama pori kwenye vijiji vya mfano imeongezeka. Kuongezeka kwa idadi ya wanyamapori huwa inachangia kuongezeka kwa mashambulizi ya wanyama waharibifu kwenye mashamba na mali nyingine.

Kwa mfano kijijini Mtanza/Msona, wanakijiji wanadai kwamba, tangu waanze uhifadhi kwenye maeneo yaliyokuwa yanawindwa kinyume cha sheria wamekuwa wakishuhudia kuongezeka kwa uharibifu wa mazao kadiri miaka inavyokwenda. Kuongezeka kwa juhudi za kijiji kwenye uhifadhi, na kuongezeka kwa udhibiti kwenye hifadhi ya Selous ni sababu ya wazi kabisa ya kuongezeka idadi ya wanyama pori kwenye kijiji cha Mtanza/Msona. Kwenye hifadhi ya Selous, kazi kubwa ni uhamasishaji, kufanya doria, kukata mipaka na kuweka mabango ya maelezo.

Kwenye vijiji hivi kuna wanyama wanaotishia maisha ya binadamu kama vile nyati, tembo, kiboko, na chui. Mamba wanapatikana kwenye Mto Rufiji na sehemu nyingine zenye maji kama vile vijito na maziwa Mtanza, Uba, Ruwe na mingine madogo madogo. Wanyama hawa ni wawindaji hatari na wasiotosheka na kila mwaka huwauwa watu kadhaa. Chuo wapo kwenye misitu ya pembezoni mwa maeneo ya maji pamoja na kwenye misitu ya kijiji. Mbali na hali ya kuogopwa na kuwa wanaishi karibu na watu bado hawajasababisha hatari yoyote. Nyati na tembo wanafika Mbunju/Mvuleni wakati wa msimu wa kuhama, lakini huwa wanapatikana kwenye kijiji cha Mtanza/Msona kwa mwaka mzima.

Wakati tulipozuru mashamba kwenye kijiji cha Mtanza/Msona watu walisikika wakipiga kelele za kufukuza wanyama na kuhami mashamba yao. Kwa upande mwingine, tulipotembelea mashamba ya Mbunju/Mvuleni tulishuhudia kuvamiwa kwa mashamba, ambapo baadhi ya maeneo yalikuwa yameharibiwa kabisa na nguruwe mwitu, kima na nyani. Hii ilithibitisha woga ulioelezwa na watu wa Mbunju/Mvuleni kwenye mkutano wa utambulisho wakati wa kujadili mpango wa utekelezaji shughuli za ziara yetu. Kwa hiyo walipanga kuwa doria zifanyike mapema ili kuweza kupata muda wa kulinda mashamba yao. Jambo hili linaelezea kwa nini hawakushiriki kwa wingi kwenye mafunzo na kazi zilizofanyika wakati wa ziara.

Kijiji cha Mbunju/Mvuleni kinasumbuliwa sana na wanyama wadogo wadogo na baadhi ya wakati huwakodi watu kutoka Ikwiriri ili kusaidia kuwatega wanyama hao. Vilevile kuna madai kwamba baadhi ya wanakijiji huwa wanatumia sumu kuwauwa wanyama wanaovamia kwenye mashamba yao, hususan nyani, kima na nguruwe mwitu. Baadhi ya maduka ya Ikwiriri huwauzia wakulima sumu hiyo. Hadi sasa aina au jina la sumu halijatambulika.

Kuna baadhi ya wakati mashamba yenye mazao huharibiwa kabisa na wanyama ambao kwa kijiji cha Mtanza/Msona huwa ni nyati na tembo na kwa kijiji cha Mbunju/Mvuleni ni nyani, nguruwe mwitu na kima. Kijiji cha Mtanza/Msona kinae askari mmoja wa wanyama pori, lakini mara nyingi huwa hawezi kusaidia chochote kwa kuwa wilaya hainunui marisao au risasi za kuwashughulikia wanyama wanaovamia mashamba. Afisa wa Wanyamapori wa Wilaya alisema kwamba mwaka jana idara yake haikupata fedha za kununua hata risasi moja, pamoja na kilio cha wananchi na kwamba halmashauri huwa inapokea asilimia 25% ya malipo yatokanayo na uwindaji wa kitalii na inachukua maduhuli yote yatokanayo na wawindaji wenyeji.

Wanakijiji wa Mtanza/Msona wapo karibu zaidi na hifadhi ya Selous, lakini walinzi wa wanyama pori wa Selous huwa hawawasaidii wananchi, kwa sababu ni kiutaratibu wanakijiji wanatakiwa kutoa taarifa kwa afisa wa wanyama pori wa wilaya ambaye ndiye mwenye mamlaka kwenye eneo hilo. Wakati mambo yanakuwa magumu sana wanakijiji huomba msaada kwa afisa wa wanyama pori wa wilaya, ambaye kwa kawaida msaada wake si wa kutarajiwa.

Migogoro kati ya wanyama pori na binadamu kwenye vijiji vya Twasalie na Jaja ina sura tofauti na wanyama waharibifu kwenye maeneo haya huwa zaidi ni jamii ya kima (nyani, tumbili na ngedere). Kima huwa wanakula minazi, miembe, na mahindi. Inafahamika kuwa kima huharibu mazao mingine kama vile viazi vitamu na maboga. Kazi ya kulinda minazi isishambuliwe na kima ni kazi ngumu kwa sababu kima huwa wanakula wakati wowote wa siku, iwe usiku au mchana. Hali hii inawafanya baadhi ya wakulima tuliowatembelea kufikiria kutumia sumu, na hili limekwishwahi kufanyika katika kupunguza tatizo la wanyama waharibifu. Haikuwezekana kupata jina la afisa wa kilimo mstaafu aliyekuwa akiwauzia sumu hiyo na wala jina la hiyo sumu halikupatikana.

Hasara inayosababishwa na wanyama hawa ni kubwa hususan kwenye minazi kwa sababu baadhi ya minazi huwa haitoi nazi kwa mwaka mzima. Wakati mshauri alipozuru Jaja na Twasalie, waislamu walikuwa wanafunga Ramadhani, bei za nazi kwa ujumla zilikuwa zimepanda kutoka bei ya kawaida ya baina ya Shilingi 30/= na 40/= hadi Shilingi 100/= kwa nazi moja huko Twasalie, na hadi Shilingi 70/= huko Jaja. Uvamizi wa wanyama waharibifu na ugonjwa unaosababishwa na virusi ambao umetapakaa kwenye vijiji hivi viwili, zinaonekana kuwa ndio sababu kubwa za kupanda kwa bei za nazi. Kwa mfano mkulima wa kisiwa cha Ulaya kijijini Jaja alidai kwamba havuni hata nazi moja kutoka kwenye shamba lake lenye minazi 150 kwa kuwa hawezi kulilinda shamba lake kutokana na kima. Ukichukulia wastani wa uzalishaji wa nazi miambili kwa mnazi, kwa mwaka na bei ya Shilingi 70/= kwa nazi, basi mkulima huyu mwenye minazi 150 hupoteza nazi 30,000 ambazo zingeweza kuzalisha Shilingi 2,100,000/= kwa mwaka.

Wanyama waharibifu wingine ambao ni muhimu kwa Twasalie na Jaja ni pamoja na kiboko, nguruwe, na ngiri kwenye mashamba ya mpunga, miwa na mahindi. Hesabu za mfano zinaweza kufanywa kwenye mashamba ya mpunga ambako hasara ilionekana ni kiasi ch a asilimia 25% kwenye mashamba yanayolindwa na asilimia 100% kwenye mashamba yasiyokuwa na ulinzi. Kwenye utafiti wake wa juu ya matumizi na thamani ya maliasili wilayani, Turpie (2000) alieleza kwamba wastani wa hasara ni asilimia 42% za uzalishaji wote. Ili kuweza kuwadhibiti wanyama waharibifu kwenye maeneo ya mashamba, wakulima wa Jaja waliunganisha nguvu na wanakijiji vijana kuwasaka na kuwafukuza wanyama waharibifu, kama vile nyani, ngiri, kima na nguruwe mwitu.

Mamba ni wananyama wanaosemekana kusabisha vifo kwenye kijiji cha Twasalie. Wanakijiji wanasema kwamba baadhi ya mamba huwa wanawatoa watu kutoka kwenye mitumbwi, baadhi ya wakati huwakamata waendesha mitumbwi ambao hutumbukiza kafi chini sana kwenye maji. Mamba hukamata mkono wa mtu, wakati anasukuma kafi, na kumvuta. Mamba ni tatizo kwenye maeneo ya Tarachu na mto Bomba. Mashambulizi ya mamba ni tatizo linalojitokeza mara kwa mara kila mwaka. Kwenye mwaka 2002 watu watano waliuwawa na saba kujeruhiwa. Mara chache hutokezea mashambulio ya chui, fisi, na simba. Wakati matatizo haya yanapokithiri wananchi huomba msaada kutoka kwa Afisa wa Wanyamapori wa Wilaya kama wafanyavyo wananchi wa Mtanza/Msona na Mbunju/Mvuleni.

Sasa hivi wanavijiji wengi wa vijiji vya mfano, hukaa kutwa kucha wakilinda mashamba yao. Wanasema, mtu asiekuwa na mke hawezi kulima na kwa hiyo wengi wao wameoa wake wawili au zaidi. Mahudhirio ya wanafunzi shuleni ni mabaya kwa sababu wanahitajika kulinda mashamba yasivamiwe na wanyama waharibifu.

### 1.5.3 Usasi wa wanyama waharibifu kwenye ardhi ya kijiji

Ujangili wa wanyamapori kwenye ardhi za vijiji vya Mbunju/Mvuleni na Mtanza/Msona ni jambo linaloendelea, lakini jambo hili huzidi wakati wanyamapori wanapohama kutoka Hifadhi ya Wanyamapori ya Selous. Kwa upande mwingine kijiji cha Mbunju/Mvuleni kipo kwenye ushoroba ambao unaanzia kutoka hifadhi ya Selous kwa upande wa magharibi na kufuata mto Ruhoi, ambao wanyamapori huutumia kwa kunywa maji wakati wa kiangazi. Kijiji cha Mbunju/Mvuleni kipo karibu na mji wa Ikwiriri na kwa hiyo hupata wawindaji, tatizo hawajui kama wawindaji hao ni halali au la. Hata hivyo Afisa Wanyamapori wa Wilaya alithibitisha kwamba, kwa muda mrefu sasa hajatoa leseni ya uwindaji kwenye eneo la Mbunju/Mvuleni. Inasemekana kwamba wasasi huja kwenye eneo kwa baiskeli au kwa miguu na baada ya kuwinda hutafuta gari kuja kuchukua nyama ambayo mara nyingi huuzwa Ikwiriri.

Wawindaji wengi wa Mtanza/Msona huwa wanavyombo vya moto na kwa kawaida huja siku za mwisho wa wiki na kuwinda upande wa kaskazini wa kijiji, kwenye eneo linalotambuliwa kama eneo wazi la Mloka. Inasemekana kwamba baadhi ya wawindaji ni maafisa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), ambao wanafahamika kwa uwindaji wao mbaya kwa sababu huwa hawachagui wanyama wa kupiga, aina ya silaha wanazotumia na hujiona kuwa hawapaswi kuulizwa juu ya wanachokifanya. Wawindaji hawa, inasemekana, wanatoka Kisarawe na jijini Dar es Salaam. Inadaiwa kwamba wanapata leseni kutoka wilaya ya Kisarawe.Vilevile inaaminika kwamba, wawindaji hawa walikuwa zamani wakiwinda kwenye eneo la wazi la Viaraka lililopo Kisarawe. Wakati wa ziara yetu iliyofanyika Jumatatu ya tarehe 22/07/2002, tuliona alama za uwindaji uliofanyika mwishoni mwa juma lilotangulia.

Kwenye upande wa kaskazini wa kijiji cha Mtanza/Msona, kuna mabango yanayoonyesha kambi ya Msigani. Halmashauri ya kijiji haijui nani anamiliki kambi hiyo, Afisa wa Wanyamapori wa Wilaya alipoulizwa kuhusu suala hili alikuwa hana hakika. Hata hivyo, ni kweli kwamba mpaka wa kaskazini wa kijiji cha Mtanza/Msona bado haujahakikishwa lakini afisa ardhi wa kijiji kambi hiyo imo ndani ya eneo la kijiji cha Mtanza/Msona.

Halmashauri za wilaya zinaruhusiwa kudhibiti uwindaji na kuzuia matumizi ya ardhi ya wilaya kwa kutumia sheria za serikali za mitaa (mamlaka za wilaya) ya mwaka 1967. Kifungu cha 114, kifungu kidogo 2 (b) cha sheria za serikali za mitaa (mamlaka ya wilaya) ya 1982, serikali za mitaa zimepewa uwezo wa kutumia sheria nambari 47 ya kumiliki ardhi ya mwaka 1967. Hii ina maana kuwa ‘Kumuomba rais kutumia nguvu zake alizopewa na sheria ya ardhi kufuta haki ya kumiliki ardhi husika’. Kwenye sheria hiyo hiyo wanaweza ‘Kuzuia ua kurekebisha kuwinda, kukamata, kuua au kuuza wanyama au ndege’ chini ya kifungu cha 118 kifungu kidogo 2(o).

Hakuna mfumo wa kuangalia uhalali wa leseni za wawindaji hao kwa sababu huwa hawafuatani na mlinzi wa wanyamapori wa serikali na kwakuwa hawataki kujibu masuala, uhalali wa shughuli zao unakuwa mashakani. Upande wa kusini wa kijiji cha Mtanza/Msona huwa unatumiwa na kampuni za kitalii, ambazo zimegaiwa mapande ya uwindaji ndani ya hifadhi ya Selous. Alipoulizwa kuhusu suala hili, meneja wa eneo la mashariki huko Kingupira alisema, wawindaji wanawinda kinyume cha sheria na kama ni kweli basi ni lazima wakamatwe. Ujangili wa meno ya tembo unasemekana kuwa bado upo, kwenye miaka ya nyuma, vijiji vilivyo pembezoni mwa Mto Rufiji vilikuwa na umaarufu wa kuwasaidia majangili wa vipusa. Pengine ujangili huu bado unaendelea, lakini la msingi ni kwamba, wanavijiji wachache kama wapo, wanaofaidika na uwindaji haramu kwenye ardhi ya kijiji.

Wakati wa ziara yetu tulikutana na mwindaji mmoja anaeitwa Krispin kutoka kampuni Intercon Hunters and Safaris Ltd ambaye alikuwa anataka apewe eneo la wazi la uwindaji la Mloka. Haijulikani, ikiwa alikuwa anataka kuanzisha kampuni yake binafsi au alikuwa anataka kufanya nini. Tulipoliangalia suala hili kwa kujadiliana na watu CITES walioko Dar es Salaam, Idara ya Wanyamapori, walithibitisha utashi wa Krispin lakini hawakutaka kuongea zaidi juu ya suala hilo. Eneo la wazi la uwindaji ni eneo lenye maelezo ya ukubwa wake lakini huwa halina mipaka. Kwa mujibu wa maelezo ya Afisa wa Wanyamapori wa Wilaya, Bw. John Eniyoye, eneo la wazi la Mloka, linaanzia kwenye mpaka na hifadhi ya Selous na kupita kwenye vijiji vilivyoko upande wa kaskazini mwa Mto Rufiji. Eneo hilo linaelekea upande wa mashariki kuelekea vijiji vya Ngulakula, Miwaga, Umbuga, na Nyatanga na linapakana na wilaya ya Kisarawe kwa upande wa kaskazini. Lakini Afisa Wanyamapori wa Wilaya hakuweza kuonyesha ramani yenye eneo hilo.

Kwenye maeneo ya delta uwindaji wa wanyamapori kwa ajili ya nyama ni mdogo sana kwa sababu wanao wanyama wachache tu ambao wanaopendwa. Wanyama ambao huwindwa kwa nyama yao ni viboko kwenye Mto Bumba ulioko kwenye kijiji cha Twasalie na kidogo kwenye maeneo ya kilimo ya Mpendeni na King'ongo yaliyoko kwenye kijiji cha Jaja. Wanyama wingine ambao huwindwa kwa nyama yao kwenye vijiji hivi ni Tohe na Mbawala. Inatambulika kwamba mara kadhaa wanakijiji wa Jaja wanashirikiana katika kuwawinda wanyama waharibifu wanaovamia mashamba yao yalioko huko kijijini Ruma. Ijapokuwa wanakijiji wa kata ya Kiongoroni hupanga udhibiti wa wanayama waharibifu kwenye mashamba yao, lakini hawaijui idadi ya wanyama pori na kilimo cha kuhama hama kinatumika sana. Watu huhama kutoka shamba moja kwenda jengine mara tu wanapohisi kuwa uzalishaji kwenye eneo walilopo umeshuka. Uhamiaji kwenye maeneo mapya husababisha ukataji wa misitu, kitendo ambacho ni kuwanyima makaazi wanymapori. Mshauri hakuweza kufahamu kama kipindi cha kuyaacha mashamba na kuyarudia tena ni cha kutosha. Vile vile haijulikani kama kijiji cha Ruma kina mpango wa matumizi ya ardhi, ambao ungesaidia kuhakikisha kuwa uharibifu wa mazingira hautokei.

### 1.5.4 Ufuatiliaji wa wanyama pori

Kila kijiji cha mfano kimepatiwa kifaa cha GPS na Walinzi (skauti) wa maliasili wa kijiji wamefunzwa jinsi ya kukitumia kifaa hicho, ili kuweza kuyatambua maeneo waliyomo. Kwenye kila kijiji kuna daftari ya kurekodi taarifa zinazopatikana kwenye doria. Wakati wa doria, taarifa zinaandikwa kwenye kitabu kidogo na baadae huhamishiwa kwenye daftari ya rekodi. Taarifa zinazokusanywa ni aina na idadi ya wanyama, alama za miguu ya wanyama na rekodi zilizosomwa kwenye GPS. Hata hivyo wanakijiji walikuwa hawajajua jinsi ya kuzifasiri rekodi za GPS kwenda kwenye ramani.

Pamoja na mapungufu hayo vifaa vya ufuatiliaji vipo kijijini na mafunzo yametolewa na chuo cha kufundisha wananchi cha (CBTI) kilichoko Songea. Pia mafunzo yametolewa na maafisa wa wilaya wa wanayampori na wale wa kudhibiti wadudu waharibifu. Hakuna mfumo wa unaoelweka wa kufuatilia wanyamapori. Ufuatiliaji wa wanyamapori unahitaji utaratibu, ukaguzi, uangalizi na uwekaji wa kumbukumbu za hali ya rasilimali ya wanyamapori kwenye ardhi ya kijiji.

### 1.5.5 Rasilimali za kwenye maji

Samaki, mamba, viboko na kasa ni rasilimali zilizo kwenye maji ambazo ni muhimu kwa vijiji vyote. Maziwa ya Mtanza, Uba na Ruwe, na Mto Rufiji pamoja na vijito vinavyomwaga maji kwenye mto huo ni rasilimali kuu za maji ziliomo kwenye vijiji vya Mtanza/Msona na Mbunju/Mvuleni (vijiji vilivyoko kwenye tambarare la mafuriko). Kwenye vijiji vya delta yaani Twasalie na Jaja rasilimali kuu za maji ni mito Bomba, Tarachu na Mkongo. Kijiji cha Jaja kinapakana na Bahari ya Hindi kwa upande wa mashariki. Vilevile kuna maziwa madogo madogo mengi pamoja na Mto Ruhoi, ambao uko nje ya eneo la kijiji. Vijiji vimeweka kanuni za kudhibit matumizi ya maji na rasilimali zilizomo kwenye maji, ambapo mbali na uvuvi kwa kutumia kibali na kudhibiti zana zinazotumika kwa uvuvi, vile vile wameweka utaratibu wa kuyafunga maeneo ya uvuvi ili kuwaruhusu samaki wakuwe. Wakati maeneo hayo yanapofunguliwa kwa ajili ya matumizi wanakijiji wa Mtanza/Msona hutoza Shilingi 100/= kwa siku kwa kila mvuvi, wakati vijiji vilivyo delta vinatoza Shilingi 1000/= kwa kila kipindi cha maji makuu, vipindi hivi viko mara mbili kwa mwezi. Mpango kama huu bado hujakubaliwa au umechelewa kutekelezwa kwenye kijiji cha Mbunju/Mvuleni. Kuna madai kwamba baraza la kijiji halijapitisha wala kuzikubali kanuni za uvuvi. Baadhi ya viongozi wa kijiji wanadai kwamba, mwaka huu kuna njaa na pia mgogoro wa mpaka wa mashariki haujapatiwa ufumbuzi hivyo haitowezekana kutekeleza kanuni za uvuvi wala sheria ndogo uvuvi. Kwa hiyo, rasilimali za uvuvi za Mbunju/Mvuleni bado zimeachwa kwenye hali ya uvuvi huria.

Kwenye vijiji vya Twasalie, Jaja na Mtanza/Msona kanuni za uvuvi zinafuatwa na walinzi wa kijiji hufanya doria ili kuwakamata wanaokiuka amri hizi. Utaratibu huu unaojaribu kudhibiti utumiaji huria wa rasilimali za uvuvi ni mzuri. Ziara yetu na doria kijijini Jaja ilithibitisha haya, kwa kuwa wakati tunasafiri kwenye Mto Mkongo, ambao kwa wakati huo ulikuwa umefungwa hakukuonekana hata mvuvi mmoja aliyekuwa kwenye mto.

Baadhi ya wakati mamba na viboko huwa ni wanyama hatari na mwaka huu mtu mmoja ameuwawa na mamba. Kijijini Twasalie, mamba huwa wanachukua watu kadhaa kila mwaka, baadhi ya watu hutolewa kwenye mitumbwi na mamba. Ikiangaliwa kwa misingi ya idadi, mamba wanaweza kuvuliwa na kuuzwa ili kusaidia kuwaendeleza watu, lakini viboko ni wachache.
Miaka kadhaa nyuma, wanasema wanakijiji wa Mbunju/Mvuleni, kulikuwa na mtu ambaye alitaka kuanzisha ufugaji wa mamba lakini hakuweza kufikia makubaliano na mkurugenzi mtendaji wa wilaya.

Uvuvi wa mamba ni shughuli ifanyikayo mara chache sana kwenye maeneo ya vijiji, ijapokuwa Mkurugenzi wa Wanyamapori hutoa vibali vya uvuvi huo. Hili ndilo jawabu la Mkurugenzi wa Wanyamapori, kufuatia maombi kadhaa ya msaada dhidi ya vitisho na hasara kwa wanavijiji. Mwaka huu (2002) kikundi cha wawindji wenye leseni walifanikiwa kumuua mamba mmoja kwenye Ziwa Uba na wakadai kwamba kuna mamba wengi kwenye ziwa lile lakini ni wachanga mno kwa haja zao. Wanakijiji wanafikiri kwamba mbinu za uvuvi zilizotumika, aina ya chambo na haraka ndio zimesabisha kutokupatikana kwa mamba wakubwa, na sio kwa sababu hawapo. Wanakijiji hawashirki katika uvuvi wa mamba na wala hawapati faida yoyote ya moja kwa moja, lakini kwa uvuvi wa kitalii halmashauri ya wilaya inatarajiwa kupokea asilimia 25% ya mapato. Kijiji kinahitaji kuwa na sheria ndogo ambayo itwalazimisha wawindaji kwenye eneo la kijiji kulipa chochote. Hili linaweza kujadiliwa kwenye mikutano ya kijiji na mapendekezo yakapelekwa kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Popote pale panapokusanywa mapato kutokana na mauzo na leseni kunakuwa na pande mbili upande mmoja unaofanya ukusanyaji na upande mwingine unaoamua matumizi. Utaratibu huu upo kwenye vijiji vyote, lakini kwenye kijiji cha Mtanza/Msona kuliripotiwa ubadhirifu. Bi. Pili Mwambeso ambaye ni mwezeshaji wa mpango wa usimamizi wa mazingira wa kijiji aliripoti kwamba matumizi mabaya ya fedha yameelezwa kutokea mara kwa mara na wanakijiji huwabidi kubadilisha wakusanyaji wakitumaini kwamba hatua hiyo itaondosha hali ya ubadhirifu.

### 1.5.6 Utekelezaji wa doria kijijini

Doria za maliasili zinakwamishwa na matatizo mengi. Hata hivyo, nafikiri kwamba kutokuthaminiwa na kutambuliwa na mamlaka husika - yaani idara zinazohusika na maliasili kwenye ngazi ya wilaya na uongozi wa Hifadhi ya Wanyamapori ya Selous - kuwa ndio kikwazo kikuu. Walinzi wanahitaji kuratibiwa na viongozi wa sekta husika kwenye idara za maliasili na wasidiwe kufanya kazi kwa pamoja kama walivyo wenzao wingine kijijini. Kwa uwezeshaji wa Afisa wa Wanyamapori wa Wilaya, walinzi wa kijiji na wale wa hifadhi ya Selous wanaweza kufanya kazi kwa pamoja. Jukumu la uongozi wa wilaya ni kuratibu wale watendaji katika ngazi ya kijiji, hii ni shughuli muhimu kwenye utekelezaji wa mradi wa usimamizi wa mazingira wa kijiji. Kwa mfano, bila ya msaada wa afisa uvuvi wa wilaya, walinzi wa kijiji cha Jaja hawawezi kuzishinda meli kubwa za uvuvi hata baada ya kupatiwa boti yenye mashine.

Kikwazo kikuu kwa watekelezaji wa doria wa kijijini ni uwezo mdogo wa wanakijiji wa kupambana na majangili wanaotumia vyombo vya moto na kwamba miradi yao bado ni michanga na haiwezi kuwezesha ufanyaji wa doria kubwa. Hii ndio sababu kubwa inayotolewa ili kufanya doria karibu na maeneo ya kijiji tu. Siku za doria kwenye kijiji cha Mtanza/Msona doria imepangwa kuwa ni siku moja hadi mbili kwa mwezi na kwenye kijiji cha Mbunju/Mvuleni ni mara moja kwa wiki na kwa Twasalie watu wameondoka kijijini na kwa hiyo hawatekelezi majukumu yao kama ilivyopangwa. Wakati wa kuruhusu uvuvi, ratiba ya doria hubadilika kwa kuwa baadhi ya walinzi hutumika kukusanya maduhuli, kwa mfano kwenye kijiji cha Mtanza/Msona.

Mpambano na majangili wenye silaha umeweka kumbukumbu kwenye akili za walinzi. Kwa mfano walinzi wa kijiji cha Mbunju/Mvuleni mara zote watazungumzia jangili waliemfukuza wakati wakiwa kwenye doria. Jangili huyo alikimbia pamoja na kwamba alikuwa na bunduki, pengine kwa sababu walinzi walikuwa karibu nae au alifikiri kwamba walikuwa na walinzi wenye bunduki kutoka wilayani. Walinzi wa Mbunju/Mvuleni na wale wa Mtanza/Msona mara zote huwa kwenye doria. Na wamesema kwamba wanapokutana na majangili wenye bunduki, hasa wale wanaotoka jeshini, inakuwa kazi ngumu kwa sababu watu hao huwa hawataki kuulizwa maswali yoyote. Na kwa kuwa wanakijiji wanakuwa hawana silaha basi wanakuwa hawana uwezo wa kulazimaisha kupatiwa majawabu.

Vijiji vya Jaja na Twasalie hufanya doria kwa sababu mbalimbali, lakini kubwa zaidi ni kuwakamata wavunaji mikoko kinyume cha sheria na wale wanaovunja kanuni zilizowekwa na kijiji kudhibiti matumizi ya maliasili. Hata hivyo, wameelekezwa kutoa ripoti kwa ofisi ya mikoko ya idara ya misitu pale wanapowakamata wavunaji haramu wa mikoko ambao wamevunja sheria. Wanasema kwamba vijiji havijapewa mamlaka ya kuwaadhibu moja kwa moja watu wanaovunja sheria kwenye hifadhi ya mikoko. Ratiba ya doria hupangwa kila wiki kwenye vijiji vyote viwili. Tofauti na vijiji vya Mtanza/Msona na Mbunju/Mvuleni, walinzi ambao wapo kwenye mafunzo kijijini Twasalie huwa hawashiriki kwenye doria. Wakati huo huo mlinzi mmoja aliefunzwa wa kijiji cha Twasalie amehama, hivyo kuifanya kazi ya ulinzi kuwa ngumu kwa wale waliobakia. Walinzi hao pia walilalamika kwamba hawawezeshwi kufanya doria na hawana vitambulisho vitakavyo watambulisha kwa watu wanaotoka nje ya kijiji wakati wakiwa kwenye kazi zao. Hivyo udhaifu kwenye ulinzi kijijini Twasalie umesabisha kuendelea kwa uwindaji wa viboko na uuzaji wa nyama zake kijijini mbele ya macho ya mwenyekiti wa kijiji, walinzi na viongozi wingine wa kijiji. Kwenye kijiji cha Jaja, kazi ya doria imekuwa ngumu hasa kwenye eneo la Kipwa Mtumbuka lililoko kwenye bahari ya Hindi.

Mafanikio ya wanakijiji kwenye vijiji vya mfano ni pamoja na kukamatwa wavunaji wa maliasili kinyume cha sheria. Kwa mfano, kwenye tukio moja walinzi wa Mbunju/Mvuleni walifanikiwa kumkamta mwindaji. Kwenye kijiji cha Mtanza/Msona wanakijiji waliwakamata wavunaji haramu wa misitu kwenye kijiji chao na wanatarajia kulipwa sehemu ya mapato ya iliyoingia kwenye halmashauri kutokana na magogo yaliyokamatwa. Wanakijiji wa Twasalie wameweka kumbukumbu za uvunaji

haramu wa nguzo na fito za mikoko iliyo kwenye ardhi ya kijiji bila ya leseni au kibali cha kijiji kwenye misitu ya matumizi na kwenye misitu ya hifadhi.

### 1.5.7 Uratibu wa wadau

Kwa ujumla uratibu baina ya wadau ni mbovu na hata ikiwa kuna uwazi wa majukumu kwa kila mdau, majukumu hayo huwa ama hayatekelezwi vyema au hayatekelezwi kabisa. Kwa mfano, jukumu la halmashauri ya wilaya katika kuwezesha usimamizi wa misitu halieleweki sawa sawa. Hali hii imesabisha ujumbe unaopelekwa na halmashauri kijijini kutofautiana na ujumbe unaopelekwa kwenye mamlaka nyingine. Mfano ni maelekezo tofauti kuhusu hali ya misitu ya asili ya kwenye vijiji vya Mtanza/Msona na Mbunju/Mvuleni.

Ni jambo linalofahamika vyema kwenye vijiji kwamba migogoro ya mipaka ilianza baada ya kuanza utekelezaji wa mipango ya mazingira ya kijiji, ambayo ilijumuisha kanuni na taratibu za kuzuia na kutumia misitu. Pamoja na ukweli huu, mshauri hakuweza kuhakisha kwamba migogoro ilizuka kwa sababu taratibu za kiasili zimebadilishwa au kwa sababu vijiji vya mfano vinahifadhi maliasili zao. Haki za watumiaji wa maliasili kutoka nje ya kijiji zinahitaji zishughulikiwe ipasavyo kwenye mipango ya usimamizi kwa kuwashirikisha watumiaji kwenye mipango na ikibidi basi mipango ya pamoja ya matumizi ardhi inabidi ifanyike.

Utekelezaji uliofanikiwa wa usimamizi unaoshirikisha jamii kwenye usimamizi wa maliasili unakubaliana na kutofautisha uwezo lakini vile vile inatambua haki za asili za utumiaji wa maliasili. Hii ina maana kwamba kwa yeyote atakaeathirika na kanuni za utekelezaji wa usimamizi wa maliasili kwa kushirikisha jamii ni lazima apewe nafasi ya kushiriki kwenye kuzirekebisha kanuni, kiasi kwamba kanuni ziwe zimekubaliwa na wote.

### 1.5.8 Misitu ya hifadhi ya kijiji

Kuanzishwa kwa misitu ya hifadhi ya kijiji ni jambo linalokubaliana na sera mpya ya Misitu. Mabaraza ya vijiji vyote vinne yamekubali kuwa sehemu ya ardhi ya vijiji iwe msitu wa hifadhi wa kijiji. Vijiji cha Mtanza/Msona na Mbunju/Mvuleni vimeamua kuchukua mbinu ya misitu ya jamii na vijiji vya Twasalie na Jaja wameamua kutumia mbinu ya usimamizi wa pamoja na idara ya misitu na nyuki. Misitu iliyohifadhiwa kwa kila kijiji ni kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali ifuatayo:

| Kijiji | Mbinu ya usimamizi waliyoichagua | Ukubwa wa msitu uliohifadhiwa |
|---|---|---|
| Mtanza/Msona | Msitu wa jamii | 10,713 ha (107.13 $km^2$) |
| Mbunju/Mvuleni | Msitu wa jamii | 1,222 ha (12.22 $km^2$) |
| Twasalie | Usimamizi wa pamoja | 16,987 ha (169.87 $km^2$) |
| Jaja | Usimamizi wa pamoja | 1,318 ha (13.18 $km^2$) |

Msitu wa Mtanza/Msona ni sehemu ya eneo la wazi la Mloka ambako wanyama wanaohama huwa wanapita wakati wakienda au wakirudi kutoka hifadhi ya Selous. Halmashauri ya wilaya pia inadai kwamba eneo hilo ni sehemu ya msitu wa hifadhi wa halmashauri. Hali kama hiyo imejitokeza huko Mbunju/Mvuleni ambako halmashauri ya wilaya inadai kwamba msitu wa Ruhoi ni wao. Hata hivyo kumbukumbu za serikali kuu hazithibitishi kuwepo kwa misitu hiyo ya halmashauri. Tofauti ya maoni ya hali na hadhi ya misitu ya vijiji vya Mtanza/Msona na Mbunju/Mvuleni ilisababisha Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki kusimamisha uvunaji kwenye maeneo hayo, kwa muda mfupi hadi kijiji na halmashauri watakapotatua mgogoro uliotokea. Maelekezo hayo, bado yanatekelezwa hadi sasa. Mbali na haya kuna tatizo la eneo la kambi ya Msigani kwenye kijiji cha Mtanza/Msona. Mwenye kambi na uhalali wa kambi hiyo bado haueleweki.

Wakati huo huo msitu wa hifadhi wa kijiji cha Mbunju/Mvuleni ni mdogo (12.22 $km^2$) na eneo la msitu mpevu wenye miti mikubwa na mbega lipo nje ya eneo lilochaguliwa kuwa ni msitu wa hifadhi. Kwa maoni ya mwenyekiti wa kijiji, eneo hilo lililoachwa pamoja na lile lilochaguliwa yapo kama yalivyo kwa sababu makubaliano ya mpaka wa msitu wa hifadhi yaliyofikiwa na kitongoji cha Mpima hayakufuatwa. Wanafikiri pengine ingefaa mipaka ikarekebishwa, lakini hilo litakuwa gumu kwa sababu ramani imeshachorwa.

Msitu wa Mbunju/Mvuleni unaowanyama wakaazi kama vile nyani. Mbega, nguruwe mwitu, na mbawala. Vilevile maeneo haya yanatumiwa na wanyama wanaohama kati ya eneo hilo na hifadhi ya Selous. Idadi na aina ya wanyama hao na maisha yao kwenye msitu wa hifadhi wa kijiji haieleweki.

Misitu mingi iliyohifadhiwa kwenye kijiji cha Twasalie na Jaja ni mikoko, ambayo imehifadhiwa kisheria na usimamizi wake upo chini ya mkurugenzi wa idara ya misitu na nyuki. Kutokana na sera mpya ya misitu, misitu hii inahitaji kusimamiwa kwa mpango wa pamoja kati ya idara ya misitu na wananchi ama ndani ya kijiji au baina ya vijiji kadhaa vyenye kuwa na sababu kupenda kushiriki kwenye usimamizi au wanahisi kuwa wanazo haki za kiasili za kutumia misitu kama hiyo. Mradi wa usimamizi wa mikoko umefanya mikutano na kila kijiji, ambapo kila kijiji kiliunda kamati ya usimamizi wa mikoko. Kwenye vijiji vya Twasalie na Jaja kamati ya usimamizi wa mikoko zilipewa majukumu makubwa zaidi na jina la kamati likabadilika kuwa kamati ya mazingira ya kijiji.

Kila kijiji kimeandika mapendekezo ya mpango wa usimamizi wa kushirikiana kati ya kijiji na idara ya misitu na nyuki. Majibu hayajarudi kutoka kwa mkurugenzi idara ya misitu na nyuki na mipaka kwa ajili ya usimamizi ya kila kijiji haijawekwa, vilevile vijiji havijakutana kwenye mkutano wa pamoja. Hata hivyo wanakijiji wa Jaja na Twasalie wameshatengeneza sheria ndogo za usimamizi wa maliasili na wameziwasilisha kwenye halmashauri ya wilaya. Kwenye kijiji cha Jaja, msitu wa hifadhi ndio makazi makuu ya kima na nyani.

### 1.5.9 Umuhimu wa maeneo ya vijiji

Wanakijiji kwenye vijiji vyote vya mfano hawajaanza kutathmini rasilimali za vijiji vyao, ijapokuwa ilikuwa imepangwa kutekelezwa. Wanakijiji wa kijiji cha Mbunju/Mvuleni waliofunzwa kazi ya kutathmini mimea wamehama na kwa hiyo mipango ya kufanya tathmini itakosa huduma zao. Kule Twasalie na Jaja hawakuwa na watu kama hawa, hata hivyo wanakijiji wa Jaja walisema kwamba wanaweza kufanya tathmini kwa kuitisha mikutano kijijini.

Pamoja na hayo vijiji vyote vya mfano vina uwezo wa usimamizi wa wanyamapori na mali asili kwa ujumla. Aina na idadi ya wanyama, pamoja na mienendo ya idadi zao bado haifahamiki vyema, lakini kwa kufuatana na takwimu na taarifa zilizopo umuhimu wa wanyamapori unatofautiana kwenye vijiji vyote vinne. Umuhimu wa wanyamapori kwenye kijiji cha Mtanza/Msona ni mkubwa zaidi kwa sababu kina eneo kubwa la kijiji na msitu, kina aina nyingi ya mimea na uoto, na kipo karibu sana na Hifadhi ya Wanyamapori ya Selous.
Kivutio kubwa kijijini Mtanza/Msona ni idadi kubwa ya twiga, nyati, na tembo wanaokuja kijijini kila mwaka kuanzia mwezi wa Agosti hadi Desemba. Kwenye kipindi hicho wengi wa wanyama hao na wingine wa aina nyinginezo huja kijijini wakitokea Hifadhi ya Wanyamapori ya Selous, wakifuata maji na malisho.

Kwa upande wa kijiji cha Mbunju/Mvuleni kivutio kikubwa ni msitu mkubwa wa asili. Sehemu ya msitu huo imo ndani msitu wa hifadhi na maeneo mingine yameachwa au yameingia kwenye vijiji vya jirani. Baadhi ya wanyamapori huja kuanzia mwezi wa Agosti hadi Desemba kila mwaka. Mkusanyiko mkubwa wa wanyama wa aina moja waliowahi kuonekana kijijini, ukiacha nyani, ni mbalapi 20 walioonekana mwaka Jana. Kwa ujumla idadi ya wanyamapori hapa ni ndogo na kwa hiyo uwezo wa kuvutia utalii wa kuangalia wanyamapori ni mdogo.

Majira ya mvua yanapoanza wanyama wanaohamahama hurudi tena Selous. Inasemwa kwamba sababu kubwa ya kurudi huku kwa haraka ni mvua na kupatikana kwa maji ndani ya maeneo, lakini pia kuna ushahidi wa ujangili. Kwa sababu ya ujangili wanyama hutumia muda mfupi iwezekanavyo nje ya hifadhi na hurudi tena mara tu kiwango cha mahitaji ya malisho na maji vimefikia kiwango cha kutosheleza.

Kwenye maeneo ya delta kivutio kikubwa ni uasili wa misitu ya mikoko. Kwa mfano, inasemekana kwamba, kwenye eneo la Makao lililopo Jaja kuna idadi kubwa ya aina mbali mbali za miti na kuna kiasi cha aina 8 za miti ya mikoko. Uoto huu una wanyama, ijapokuwa kidogo hasa kima, ngedere, nyani, ngiri na nguruwe mwitu. Vilevile kuna ndege wanaohamahama kama vile korongo na yangenyange ambao huja kila mwaka baina ya Desemba na February. Kijiji cha Twasalie kimetenga eneo ambalo ni mahsusi kwa usimamizi wa wanyama pori. Ngiri wa Twasalie ni wanyama wanaokula na kuzurura kwenye maeneo mengi hivyo umuhimu wake ni mkubwa. Umuhimu wa maeneo ya bahari ya Jaja bado haujachunguzwa. Hata hivyo umuhimu wa eneo la matumbawe la Kipwa Mtumbuka unajulikana vyema.

# 2 Warsha ya kuitaarifu EMT matokeo ya kazi

Siku ya mwisho ya kazi hii ilikuwa ni kuendesha warsha ya wanakamati wa timu ya usimamizi wa mazingira iliyoko wilayani. Warsha hii ililenga kuwapa washiriki nafasi ya kuchangia mawazo kwenye kuweka mikakati ya kutatua matatizo au masuala yanayohusu wanyamapori kwenye wilaya ya Rufiji. Ripoti iligawanywa na kuwasilishwa kwenye maeneo matatu kama ifuatavyo

- Kupitia sekta ya wanyamapori kwenye wilaya ya Rufiji.
- Hali ya sasa kwa kila kijiji.
- Masuala yanayohitaji hatua za haraka.

Utondoti wa kila suala upo kwenye ripoti ya warsha.

Majadiliano yalifanyika kila baada ya kuwasilisha suala moja, hii ilisaidia kuongeza taarifa na kuithibitisha ripoti. Maeneo ambayo yalijadiliwa sana ni

- Majukumu na kushiriki kwa wadau tofauti (madiwani, wanavijiji, viongozi wa vijiji, wafanyakazi wa ugani, watendaji kata na watendaji wa vijiji) kwenye usimamizi wa mazingira.
- Majukumu ya na ushiriki wa kamati mbalimbali (baraza la kijiji, halmashauri ya kijiji, kamati ya usimamizi wa mazingira, kamati za mazingira, kamati za maendeleo za kata, halmashauri ya wilaya) kwenye usimamizi wa mazingira.
- Uwezo wa sekta ya wanyamapori kwenye halmashauri ya wilaya ya Rufiji na halmashauri za vijiji kwenye kudhibiti wanyama waharibifu.
- Ada za kuwindia na haja ya kushirikisha wana kijiji kwenye matumizi yake kwenye kuimarisha utaratibu wa kushirikisha wananchi kwenye utengenezaji mipango.
- Ushiriki wa wote kwenye utayarishaji na utekelezaji wa sheria ndogo za usimamizi wa mazingira.
- Uvuvi unaofanywa na meli na uharibifu wa mazingira unaotokana nazo.
- Kushiriki kwenye warsha za kutayarisha mipango ya usimamizi wa mazingira kwa wanavijiji kutoka kwenye vijiji ambavyo si vya mfano.
- Tathmini ya maliasili za kijiji
- Kuwakamata majangili na msaada kutoka mamlaka husika.
- Mivutano ya mipaka, uwekaji wa kumbukumbu kuhusu masuala ya mipaka na msaada wa wilaya katika kutatua migogoro hiyo.
- Mioto ya misitu na jinsi ya kuisimamia na kuizuwia.

Baadae wanawarsha waligawanywa kwenye makundi saba na kila kundi lilipewa suala moja amabalo linahitaji kujadiliwa na walitakiwa watoe mapendekezo yao ya ipi ni njia bora ya kulishughulikia na nani alishughulikie. Masuala yaliyojadiliwa ni:

- Uwezo mdogo wa vijiji vya mfano kupambana na wanyamapori na ukosefu wa kiwango na thamani ya uharibifu au hasara iliyopatikana.
- Kuongezeka kwa ujangili na udhaifu wa doria kwenye vijiji.
- Kuelezea kinaganaga maeneo ya kijiji na masuala ya mipaka.
- Uwezo mdogo wa sekta ya wanyamapori katika kupambana na wanyama waharibifu.
- Ukosefu wa taarifa za tathmini na thamani ya maliasili za vijiji na wilaya na mdogo wa kutayarisha na kutekeleza mipango endelevu.
- Uvuvi wa kamba kwa meli kwenye maeneo ya vijiji yaliyomo ndani ya Bahari ya Hindi.
- Mioto ya mapori na kilimo kwenye misitu ya asili.

Matokeo ya majadiliano ya vikundi yaliwasilishwa na kujadiliwa kwa pamoja. Hatua zilizokubaliwa zimo kwenye ripoti ya warsha.

# 3 Hitimisho

## 3.1 Suala la mipaka ya kijiji

Kwenye vijiji vyote vinne vya mfano utekelezaji wa mpango wa usimamizsi wa mazingira wa kijiji unakwamishwa na migogoro na kukosekana kwa uhakika wa mipaka ya kijiji. MUMARU imesaidia kuwezesha mawasiliano baina ya vijiji na majirani zao. Kuna baadhi ya mipaka ambapo vijiji vimefanikiwa kuondosha migogoro ya mipaka, ambalo ni jambo muhimu katika kuboresha usimamizi wa wanyamapori pamoja na maliasili nyingine kwenye maeneo yao.

Kifungu 4.2.2.7 cha Sera ya Ardhi ya mwaka 1995 inasema kwamba 'ili kuweza kudhibiti ardhi za vijiji… halmashauri za vijiji zitapewa nyaraka zinazooonyesha mipaka ya kijiji…' hili linapewa uzito wa kisheria kwenye Sheria ya Ardhi nambari tano (5) ya mwaka 1999 chini ya kifungu 7 (7) amabayo inaruhusu kijiji kupewa cheti cha umiliki wa ardhi ya kijiji. Suala la ardhi ya kijiji halijashughulikiwa na vijiji vya mfano na pengine vijiji vyengine vya wilaya ya Rufiji vilevile havijalishughulikia kama ambavyo halijashughulikiwa na vijiji vingi nchini.

Matatizo ambayo wanakijiji wanakumbana nayo kwenye utekelezaji wa mpango wa matumizi ya ardhi vijijini pengine ni kwa sababu kila kijiji kinajifanyia mipango yake peke yake. Uzoefu unaonyesha kwamba, ikiwa vijiji vyote vitashirikishwa kwenye mipango ya matumizi ya ardhi migogoro ya mipaka itapunguzwa. Utayarishaji wa mipango ya matumizi ya ardhi huanza na makubaliano ya mipaka ya vijiji. Kwa mfano kama ingelikuwa ni maelekezo ya Kamati ya Ujenzi, Uchumi na Mazingira ya wilaya ili kutayarisha mipango hiyo basi vijiji vingi vingefikia muafaka kuhusiana na mipaka yao ya asili. Kazi hii hata hivyo hubidi kufanywa kwa uangalifu ili kuepuka kuchanganya mipaka ya kiasili ya kijiji na mipaka ya kata, tarafa au wilaya. Mipaka ya kiasili ya kijiji inaweza kwenda nje ya mipaka hiyo au huweza kuacha maeneo baina ya vijiji ili kuwa eneo la pamoja ambalo linakuwa chini ya Kamishna wa Ardhi.

## 3.2 Migogoro ya binadamu na wanyamapori

Wanyamapori ni rasilimali ya wote ambayo huwa ina uwezo wa kutembea na kwa hiyo uhuru wake huwa hauna kikomo. Itaonekana kwamba, kupungua kwa shughuli za binadamu kwenye maeneo yaliyohifadhiwa hupelekea kuongezeka kwa idadi ya wanyama pori. Kwenye hali kama hiyo watu wanoishi kwenye maeneo haya huwa daima wamo katika ushindani na wanyama pori kwa sababu wote huwa wanatumia makazi yale yale. Kutokana na kuwa karibu basi wanyama huvamia mashamba na hiki kimekuwa kilio cha wakulima wengi kwenye vijiji vya mfano na wilaya nzima kwa ujumla.

Bado haijawa rahisi kuweza kujua kiwango cha hasara zinazopatikana kwa watu kupoteza maisha na mali zao, lakini hasara hii ni maradufu. Tathmini ya haraka iliyofanywa na mshauri inaonyesha kwamba kwa miongo kadhaa mashamba huharibiwa kabisa. Kwa wastani, mashamba yanayolindwa vyema hupata hasara ya asilimia 25% na yale ambayo hayakulindwa hupoteza asilimia mia moja 100%. Nyati, tembo, viboko, nyani, kima na nguruwe mwitu ni kati ya wanyama waharibifu waliorikodiwa hadi sasa. Nyati na tembo wapo Mtanza/Msona na Mbunju/Mvuleni, ijapokuwa kuna baadhi ya wakati ambapo nyati wameripotiwa kuonekana huko Twasalie. Mamba ni tishio kwenye vijiji vya Mtanza/Msona, Mbunju/Mvuleni na Twasalie kwa sababu huwadhuru watu kadhaa kila msimu. Watu hujishughulisha na uvuvi wa samaki au hata uwindaji pale ili waweze kumudu maisha, wakati mashamba yao yanapoharibiwa na wanyamapori.

Ni jukumu la halmashauri ya wilaya kupambana na wanyama hatari, kuwaelekeza wananchi kutumia mbinu za kuwafukuza wanyama bila ya kuwauwa na kuwasaidia wakulima kulinda mazao yao. Tatizo ni kwamba halmashauri ya wilaya ya Rufiji haina vifaa wala wafanyakazi wa kutosha. Uwezo mdogo wa halmashauri na serikali kutokulipa fidia kwa uharibifu au hasara zitokanazo na wanyamapori

kimekuwa chanzo cha migogoro kati ya wahifadhi na jamii imbayo inapelekea uvunaji haramu wa maliasili. Hali hii inawatanza wanavijiji na huwafanya wasiwe na ari, na wagawanyike kimawazo kuhusu suala la uhifadhi wa wanyamapori kwenye ardhi zao.

## 3.3 Uwindaji wa wanyamapori kwenye ardhi za kijiji

Wanyamapori waliomo kwenye vijiji, kama zilivyo rasilimali nyingine za pamoja, wanaathiriwa na kutumiwa kwa pamoja na watu wote. Watu kutoka nje ya kijiji na mara nyingine kutoka nje ya wilaya huja kuwinda. Wanavijiji huwa hawafaidiki na uwindaji haramu ambao hufanyika kwenye ardhi yao ndani na nje ya msimu wa uwindaji. Halmashauri ya wilaya na hata Mkurugenzi wa Wanyamapori hawana uwezo wa kuzuwia uwindaji haramu vijijini.

Hii ndio sababu ya kuwa na sera mpya ya wanyama pori ambapo maeneo ya wazi ya uwindaji na maeneo yaliyodhibitiwa yanageuzwa kuwa hifadhi za kijiji ambazo zinaitwa Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori (WMA). MUMARU wanatumia sera ya taifa ya misitu na miongozo ya usimamizi wa misitu ya jamii ili kuwasaidia wafanyakazi wa halmashauri kuviwezesha vijiji kuweka mipaka yao wakati wa kutenga misitu ya hifadhi ya kijiji. Sasa hivi mradi umo kwenye jitihada za kuwezesha wilaya kuitumia sera ya wanyamapori ili wilaya iwawezeshe wanakijiji kuitumia sera kuzifikia haki zao za kutumia rasilimali ya wanyamapori. Vijiji vya mfano vinachukua juhudi ili kudhibiti uwindaji haramu na kuweza kupata haki zao za kutumia wanyamapori.

## 3.4 Ufuatiliaji wa wanyamapori

Kimsingi ufuatiliaji ni lazima ufuatane na malengo ya usimamizi (uendeshaji) na hutumia taarifa zinazokusanywa kila siku au kadiri iwezekanavyo. Kwenye vijiji vya mfano tayari kuna mfumo ambapo taarifa na takwimu zinazokusanywa huwekwa kwenye daftari ya kumbukumbu. Vijijini upo utaratibu wa kukusanya taarifa lakini wanavijiji na maafisa wa wanyamapori wa wilaya bado hawajajifunza ni vipi wazitumie taarifa hizo. Wakati kazi inayoelezwa kwenye ripoti hii inafanyika kulikuwa na mijadala mifupi juu ya kutambua na kutumia viashirio au dalili. Pamoja na yote hayo kutengeneza mfumo wa ufuatiliaji kunahitaji muda zaidi na kwa hiyo jambo hili liliachwa kwa mipango ya baadae.

Ilionekana kwamba aina ya taarifa zinazokusanywa wakati wa doria hazitoshelezi haja ya ufuatiliaji wa wanyamapori na hivyo taarifa zaidi inabidi zikusanywe. Ili kukusanya takwimu zinazohitajika, kitabu kidogo kinafaa, lakini mtu anaweza kusahau kurekodi baadhi ya taarifa muhimu zinazohitajika kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini. Hivyo, fomu yenye kusaidia kukusanya taarifa kinaganaga zilitayarishwa na kujadiliwa wakati wa mafunzo kabla ya kuunda mfumo wa ufuatiliaji. Mfumo mzuri wa ufuatiliaji haunabudi kuwezesha kukusanywa taarifa za kutosha kwa ajili ya usimamizi wa wanyamapori.

Ili kuweza kusimamia wanyamapori ipasavyo, walinzi wa vijijini wanahitaji mafunzo juu ya misingi ya kufanya tathmini, ramani, na uwekaji kumbukumbu. Walinzi wote wa vijiji vya mfano na wafanyakazi watatu wa wilayani walifunzwa jinsi ya kutumia GPS. Inaonekana kwamba walielewa vyema mafunzo hayo. Utumiaji wa GPS ni mbinu ya msingi kwenye doria na sensa ya wanyama, kwa hiyo ingefaa wanakijiji wakazidi kuelimishwa kuhusu matumizi ya chombo hicho. Kwa kuwa sasa vijiji vimepatiwa vifaa vya GPS na wanapatiwa mafunzo zaidi kutoka kwa wafanyakazi wa halmashauri, inawezekana watakuwa na uwezo wa kukitumia kifaa hicho.

## 3.5 Utekelezaji wa Doria

Kwenye vijiji vyote vya mfano wanakijiji huendesha doria kwa kati ya siku moja hadi mbili kila mwezi. Mafanikio yaliyopatikana kwenye baadhi ya doria inaoonyesha uadilifu wa walinzi. Hata hivyo tatizo kubwa ni kutambuliwa na kuthaminiwa na wenzao wa wilayani na hifadhi ya Selous. Vilevile doria za walinzi wa kijiji hufanyika karibu na kijiji kwa sababu walinzi huwa hawana silaha na

wanagopa kushambuliwa na majangili wenye silaha. Mbali na suala la silaha, wale walinzi wa kijiji waliofunzwa tu ndio wenye sare, na hawa wanatambulika kijijini tu.

Vijiji vya mfano vinatakiwa kusaidiwa kwa kuwakamata wanaouvunja sheria za maliasili. Halmashauri ya wilaya ya Rufiji na Hifadhi ya Wanyamapori ya Selous wanatakiwa kuviunga mkono vijiji vya Mtanza/Msona na Mbunju/Mvuleni, na mradi wa mikoko pamoja na halmashauri ya wilaya ya Rufiji wanatarajiwa waviunge mkono vijiji vya Jaja na Twasalie. Vijiji vyote vimelalamika kwamba hawapewi msaada unaotakiwa na kuna baadhi ya wakati wameitwa majangili. Hali hii inawaweka njia panda kuhusiana na suala la uhifadhi wa wanyamapori.

## 3.6 Uratibu wa wadau

Kumefanyika warsha kadhaa za wadau katika ngazi ya wilaya na mkoa ambazo zimewezeshwa na MUMARU. Ni kawaida kwa wadau wengi kuhudhuria warsha kama hizo. Ijapokuwa ingetarajiwa kuwa uratibu wa wadau ungetosheleza kwenye ngazi ya kijiji, mapungufu kadhaa yamejitokeza. Baadhi ya wadau muhimu kama vile afisa misitu wa wilaya, afisa wa wanyamapori wa wilaya na wakuu wa maeneo wa Hifadhi ya Wanyamapori ya Selous huwa hawashiriki katika utekelezaji wa mipango ya usimamizi wa mazingira ya kijiji. Wanavijiji wangependa kupata msaada wa wadau hawa.

Mradi wa usimamizi wa mikoko umekuwa ukishirikiana na wanavijiji kwenye maeneo ya Delta na wamefanya mikutano kwenye vijiji vyote viwili ili kuanza mpango wa usimamizi (uendeshaji) wa misitu kwa ushirikiano. Utaratibu huo umepiga hatua kubwa, kiasi kwamba meneja wa mikoko wa wilaya ya Rufiji alieko Nyamisati Bw. Frank Sima, aliwaeleza wananchi wa Twasalie kwamba, mapendekezo yao yameshawasilishwa kwa mkurugenzi wa idara ya misitu na nyuki kwa ajili ya kuidhinishwa na kuwekwa saini.

## 3.7 Kufanya biashara ya wanyamapori vijijini

Uwekezaji kwenye biashara za wanyamapori ni ghali sana. Hata hivyo, inawezekana kuwa wapo wawekezaji ambao wanataka wapate maeneo au wapate washirika wa kufanya nao biashara ya kupeleka watalii. Umuhimu wa tathmini katika kufanya shughuli kama hiyo ni mkubwa sana. Matokeo ya tathmini yanaweza kutumiwa kutafuta wafadhili au wawekezaji.

Kila mwaka mnamo mwezi wa Agosti hadi Desemba, wanyama wanaohama kutoka Selous hufika kwenye vijiji vya Mtanza/Msona na Mbunju/Mvuleni. Kwa kuwa kijiji cha Mtanza/Msona kipo karibu na hifadhi ya Selous basi hupata wanyama wengi kuliko Mbunju Mvuleni. Wanyama hawa wanakuja kunywa maji kwenye Mto Rufiji, mto Ruhoi na kwenye maziwa ya Mtanza, Uba na Ruwe. Hata hivyo uhamiaji huu hautoshi, kwasabu kufanikiwa kwa utalii wa wanyamapori kunahitaji wanyama wawe wengi na wakae kwenye eneo husika kwa muda mrefu kila mwaka.

Hata hivyo, vijiji vya Mbunju/Mvuleni na Mtanza/Msona vina nafasi nzuri ya kuendeleza uwindaji kwa ajili ya nyama na kuweza kupata mapato kutokana na kuuza nyama na kukatisha leseni za uwindaji. Kujulikana kwa idadi ya wanyama waliopo kutasaidia kuamua, idadi ya wanyama watakaowindwa kila mwaka, inafaaa kujaribu njia hii. Pamoja na kwamba kuna haja wanyama kuongezeka, kijiji cha Mtanza/Msona kinaweza kufaidika na utalii wa kupiga picha na wawindaji wa kitalii hata kwa hali ya sasa. Rasimu ya miongozo ya maeneo ya usimamizi wa wanyama pori inaelezea kuwa uwekezaji ni kuzitumia nafasi zinazotolewa kwenye maeneo ya usimamizi wa wanyamapori kwa ajili ya biashara. Hata hivyo mtu hawezi kupata nafasi ya kuwekeza kwenye maeneo hayo kabla ya haki za utumiaji kupatikana.

Kwa upande mwingine kijiji cha Mbunju/Mvuleni kina nafasi ndogo ya kuendesha utalii wa wanyamapori, kwa sababu kuu tatu: moja ni udogo wa maeneo ya kijiji na msitu wake, mbili ni idadi ndogo ya wanyama wanaofika kwenye hifadhi ya msitu wa kijiji na tatu ni aina ya mimea iliyopo (uoto

uliopo). Ijapokuwa bioanuwai ya kwenye misitu mikubwa inaweza kuwa kubwa lakini kwa kawaida inakuwa na idadi ndogo ya wanyama. Kwa hiyo kijiji cha Mbunju/Mvuleni kinaweza kuekeza kwenye utalii wa bioanuwai yaani utalii wa kiikolojia kwenye misitu.

Utalii wa kiikoloji (ecotourism) umepewa tafsiri mbalimbali, lakini kwa ujumla ni utalii ambao lengo lake kuu ni "*muingiliano na maumbile, na inajumuisha hamu ya kupunguza athari mbaya [kwenye maeneo yanayotembelewa]*". Ili kuweza kuendesha utalii wa kiikolojia kwenye eneo inahitaji tathmini ya thamani na matumizi ya maliasili za kijiji na kuzielezea umuhimu wake katika ngazi ya taifa na kimataifa. Kwa mfano sababu zilizopelekea kuhifadhiwa kwa msitu wa kijiji zinaweza kutumika kuelezea umuhimu wa msitu huo.

Kwenye maeneo ya delta misitu ya mikoko na mchanganyiko wa aina za viumbe ni kivutio kikuu. Twasalie inaweza kuwa ni moja kati ya sehemu chache kwenye ukanda wa pwani ambako kunapatikana mamba na viboko kwenye makazi ya asili karibu na bahari. Jaja ni moja ya vijiji vinavyopakana na Bahari ya Hindi na kina matumbawe kwenye eneo la Kipwa Mtumbuka. Eneo hili linaweza kuwa kivutio kikubwa lakini litahitaji usimamizi (uendeshaji). Vijiji vya pwani vina nafasi ya kuendesha biashara ya kombe (seashells).

Mambo mingine ya kuwekeza kwenye wanyamapori, yanayoweza kufanyika kwenye vijiji vya mfano ni uuzaji nyara. Nyara hizi zinaweza kutokana na wanyama hai au wanyama waliokufa. Kwa mfano kuna uwezekano wa kuendesha biashara ya kuuza ndege kwenye soko la ndani au hata kusafirisha nje ya nchi. Aina mbalimbali za nyara zimeorodheshwa kwenye fomu ya maombi ya leseni ya kuwinda nyara. Baadhi yao, kwa mfano ufugaji wa wanyama, zinaweza kujaribiwa. Kwa hiyo ufugaji wa mamba, makobe na vipepeo unaweza kuchunguzwa, vile vile utengenezaji wa kambi za watalii (campsites) ni moja ya mambo yanayoweza kufanyika.

Uombajiwa kibali cha ufugaji wa wanyama na mambo mingine yanayohusu nyara zitokanazo na wanyamapori hufanyika kwa kupeleka maombi kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori kutumia Fomu Nambari 13 (Game Form Number 13). Hii ikikubaliwa na Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori inamruhusu muombaji kupatiwa leseni ya uwindaji nyara. Baada ya hapo vibali huwa vinatolewa kufuatana na mahitaji, kwa mfano ikiwa mtu au kijiji kinajishughulisha na ufugaji wa mamba, basi itabidi mfugaji aombe kibali cha kuvuna mamba chini ya taratibu za mkataba wa kimataifa wa kulinda mimea na wanyama (CITES). Tanzania imeuridhia mkataba wa CITES kwa hivyo inawajibika kufuata taratibu zake. Taratibu za kuomba leseni ya kuwinda nyara hazihitaji kufuata rasimu ya miongozo ya maeneo ya usimamizi wa wanyamapori.

Kijiji cha Mbunju/Mvuleni kina sehemu ya msitu wa mpingo, kwa hiyo wanakijiji wanaweza kuwekeza kwenye uchongaji na utengenezaji vinyago. Mambo haya yote yanahitaji tathmini ya malisili ziliopo, na kufuatiwa na utangazaji na uwekezaji kwenye miundo mbinu. Vilevile mambo haya yanahitaji utafiti wa kina juu ya upatikanaji wa rasilimali.

## 3.8 Utekelezaji wa miongozo ya maeneo ya usimamizi wa wanyamapori

Nyaraka za mpango wa usimamizi wa mazingira wa vijiji zimeelezea haja ya vijiji kuanzisha utumiaji wa wanyama pori walio kwenye vijiji vyao. Hata hivyo, tatizo kubwa lililopo ni eneo la kisheria la kijiji bado halijafahamika vyema. Hadi sasa ni vigumu kuzungumzia uhalali wa kutumia wanyamapori kwa kufuata miongozo ya maeneo ya usimamizi wa wanyama pori.

Ili kuweza kuomba kubadilisha haki za matumizi kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori, kijiji kinahitaji kuwa na mpango wa matumizi ya ardhi ambao unaonyesha hali halisi ya sasa. Chini ya sheria ya ardhi, kijiji hakiwezi kutayarisha mpango wa matumizi ya ardhi wakati kikiwa na mgogoro wa mipaka. Hata hivyo kuna sababu ya msingi ya kuanza kuweka msingi kuelekea kwenye mpango huo kwa kuanza hatua za mwanzo kama ilivyoelezwa kwenye miongozo ya maeneo ya usimamizi wa

wanyamapori. Baadae hii itakuwa hatua muhimu kwa kijiji cha Mtanza/Msona, ambacho kina eneo kubwa ambalo halijahifadhiwa. Ni lazima itarajiwe kwamba kutakuwa na mipango tofauti ya kutumia wanyamapori kwenye misitu ya hifadhi ya chini ya miongozo ya maeneo ya usimamizi wa wanyamapori inayotarajiwa kutolewa siku za karibuni.

Maeneo yaliyokwenye mipaka ya vijiji si mfumo kamili wa kiikolojia kwa ajili ya wanyama wanaohama hama, vilevile vijiji havijui mipaka yao. Hali hii inautanza utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa mazingira, hivyo uchambuzi wa hali ya maliasili inaweza kuwa ni muhimu kufanyika.

## 3.9 Rasilimali za maji za kijiji

Vijiji bado havijafikiria usimamizi wa wanyamapori wanaoishi kwenye maji. Hata hivyo, kwenye vijiji vya Mtanza/Msona, Mbunju/Mvuleni na Twasalie, inawezekana kukafanyika ufugaji wa mamba. Hadi sasa vijiji vimeshughulika na ufugaji wa samaki tu, ambao unaweza kuathiriwa na utumiaji wa pamoja. Hali ya uvuvi wa sasa, hasa kwenye kijiji cha Mbunju/Mvuleni si endelevu na kuna haja ya kuidhibiti hali hiyo.

## 3.10 Rasilimali ya misitu ya vijiji

Misitu ya hifadhi ni makazi ya wanyamapori na kwa hiyo usimamizi wa maeneo haya utaongeza usimamizi wa wanyamapori. Sheria ya Misitu ya mwaka 2002 inatoa nafasi ya usimamizi shirikishi katika mipango kama vile misitu ya hifadhi ya vijiji, usimamizi wa pamoja na kadhalika. Kwenye mipango hii haki za watumiaji wa miti iliyomo kwenye misitu ya hifadhi huwa inakuwa ni ya taasisi au mtu anaechukua jukumu la kusimamia misitu hiyo. Vilevile, na ijapokuwa inahitaji utaratibu wa ziada, haki ya utumiaji wa maliasili ya wanyamapori, huwa inamilikiwa na wasimamiaji wa msitu. Katika kupata haki hizi, vijiji vya mfano vimefuata taratibu kadhaa na inaweza kusemwa kuwa walau wameanza hatua za awali.

Katika kufuata taratibu hizo, vijiji viwili vimetenga sehemu ya kijiji kuwa msitu wa asili ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa mazingira wa kijiji. Lakini wakati wa kuthibitisha wawakilishi wa halmashauri walisema kwamba maeneo hayo ni hifadhi za halmashauri ya wilaya. Ukweli ni kwamba, kwa muda mrefu halmashauri ya wilaya imekuwa ikitoa leseni za kukata magogo ndani ya msitu wa Mtanza/Msona na Mbunju/Mvuleni pamoja na kwamba halmashauri haifanyi usimamizi. Halmashauri imekuwa ikikusanya maduhuli na wala haijawahi kutumia fedha hizo kuendeleza misitu.

Kwa hiyo, haikuwa rahisi kupitisha mpango wa msitu wa jamii ulioanzishwa na kijiji. Hatua hiyo ilisababisha malumbano baina ya wanavijiji na halmashauri ya wilaya ya Rufiji. Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki, akiwa kama msuluhishi, alielekeza kwa makusudi kabisa kusimamisha uvunaji wa misitu hiyo ili kutoa nafasi kwa pande mbili zinazopingana kutafutia ufumbuzi tatizo hili.

Hadi sasa uvunaji haujasimama kama ilivyotarajiwa na kumekuwa na ucheleweshaji wa kutafutia ufumbuzi tatizo lillilojitokeza. Kifungu Nambari 40 (hatua za awali) cha Sheria ya Misitu ya mwaka 2002 kinauelezea msitu wa hifadhi kama ni msitu uliotangazwa na baraza la kijiji kuwa ni msitu wa hifadhi. Hii ina maana kwamba mara tu baada ya uamuzi wa baraza la kijiji msitu unakuwa umehifadhiwa. Vilevile, miongozo ya usimamizi wa misitu ya jamii unazitaka halmashauri za wilaya kuanzisha na kuliendeleza daftari la kumbukumu za misitu ya hifadhi. Jambo hili bado halijafanyika kwenye halmashauri ya wilaya ya Rufiji. Labda hii ni kwa sababu sera ya taifa ya misitu na miongozo ya utekelezaji bado ni mpya na zinahitaji ujuzi wa kuzifasiri. Hata hivyo kwenye vijiji vyote utaratibu unatayarishwa ili kuitambua misitu ya hifadhi ya vijiji.

Kwenye maeneo ya delta mpango wa usimamizi wa misitu kwa pamoja kati ya wanakijiji na idara ya misitu na nyuki umo kwenye matayarisho kwa ajili ya kuifanya halmashauri ya wilaya kuitambua rasmi misitu ya hifadhi ya kijiji.

# 4 Mapendekezo

Kwenye ngazi ya wilaya kuna Timu ya Usimaizi wa Mazingira (EMT), ambayo kimsingi ni sehemu ambapo masuala ya usimamizi wa mazingira huwa yanajadiliwa. Timu hiyo haijaundwa kisheria lakini huwa inajadili masuala ambayo yanahitaji ufumbuzi wenye nguvu za kisheria, lakini kwa bahati mbaya timu hiyo haiwezi kufanya maamuzi kama hayo. Kwa hiyo pamoja na kuanzishwa kwake mnamo mwaka 1998 na kuwa imeshafanya vikao zaidi ya 50 bado uratibu wa juhudi zake hautoshelezi. Uzoefu sehemu nyingine unaonyesha kwamba, kamati zenye nguvu za kisheria ambazo ziko chini ya uenyekiti wa Mkuu wa Wilaya zimesaidia kuboresha uratibu. Mkurugenzi Mtendaji wa wilaya ya Rufiji Bw. F. Q. M Fissoo na Afisa wa Ardhi, Maliasili na Mazingira Bw. M. S. Chande walisema kwamba, halmashauri ya wilaya Rufiji imetakiwa na ofisi ya waziri mkuu, kuanzisha Kamati za mazingira zenye nguvu ya kisheria kwenye ngazi ya wilaya, kata na kijiji. Hata hivyo hawajapewa maelekezo ya jinsi ya kuziunda kamati hizo. Kwa kuwa haijulikani ni lini maelekezo hayo yatatolewa, mshauri anapendekeza kwamba walau kwa sasa wilaya ingeunda kamati ya wilaya ya ushauri wa maliasili.

## 4.1 Suala la mipaka ya kijiji

MUMARU umeviwezesha vijiji kuongeza uwezo wao kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo upangaji wa matumizi ya ardhi. Mafanikio haya yanahitaji kuimarishwa na juhudi ziendelee kuziimarisha zaidi. Mshauri anapendekeza kwamba:

- Afisa Ardhi na Mpimaji Ardhi wa Wilaya wavisaidie vijiji vya mfano kukamilisha mijadala ya kutatua migogoro ya mipaka kama ambavyo imeainishwa kwenye kifungu 7(2) cha Sheria ya Ardhi ya vijiji nambari 5 ya mwaka 1999. Hii inatumika pale ambapo vijiji vimeshindwa kufikia muafaka kwa kupitia juhudi zao binafsi kwenye mikutano ya uhusiano mwema.
- Wataalaam hao wawezeshe uchorwaji wa ramani ya mipaka ya kijiji na kuvisajili vijiji vya mfano kama ambavyo imeelekezwa kwenye Kifungu 7 (7) cha Sheria ya Ardhi Nambari 5 ya mwaka 1999. Ramani itahitajika wakati wa kuomba cheti cha usajili wa kijiji.
- Kwenye baadhi ya maeneo, mbinu ya usimamizi wa ardhi kwa pamoja unaweza kuwa ni wa lazima kama ambavyo imeelekezwa kwenye Kifungu Nambari 11 cha Sheria ya Ardhi Nambari 5 ya Mwaka 1999.

## 4.2 Migogoro ya wanyamapori na binaadamu

MUMARU umewafunza walinzi (skauti) wa maliasili wa vijiji na watu wingine wamejifunza kutoka kwa wale waliofunzwa na kutoka kwa afisa wanyama pori wa wilaya. Haya ni mafanikio makubwa katika kudhibiti wanyama waharibifu. Sheria ya Kumiliki Silaha ya Mwaka 1991 na ile ya uhifadhi wa wanyamapori nambari 12 ya mwaka 1974 zinaruhuzu mtu kujilinda yeye na mali zake. Inapendekezwa kutumia wanakijiji hawa wenye ujuzi kupunguza matatizo ya wanyama waharibifu kwenye mashamba.

- Inapendekezwa kwamba vijiji visaidiwe kupata bunduki na nyavu na kuifanya shughuli ya kuondoa wanyama waharibifu kuwa ni jukumu la halmashauri ya kijiji.
- Kuongeza uwezo ni jambo moja lakini kuutumia uwezo uliopatikana ni jambo jengine tofauti. Sasa ni lazima kwa halmashauri ya wilaya kutumia uwezo wa wanavijiji katika kuondoa tatizo la wanyama waharibifu. Wilaya inaweza ikaiga mfano wa kijiji cha Ngarambe, ambako skauti wa wanyamapori wa kijiji wameisaidia sana halmashauri katika kutatua tatizo la wanyama waharibifu.
- Kama hatua ya awali, halmashauri itumie asilimia 25% ya mapato kutokana na watalii wawindaji kununua marisao na risasi na kuwapatia walinzi wa wanyamapori wa kata na vijiji.
- Mipango lazima ifanywe kuziboresha mbinu za ulinzi za kienyeji kama vile utumiaji wa ndoana kwa mamba, matumizi ya moto, kupiga kelele na nyavu kwa wanyama wingine. Halmashauri ya wilaya/afisa wa wanyamapori, na afisa wa kilimo na mifugo wa wanaweza kuendesha mpango huu.

## 4.3 Uwindaji wa wanyamapori kwenye ardhi ya kijiji

MUMARU umesaidia kuongeza uwezo wa vijiji katika kutambua haki na wajibu wao, vilevile umetoa mafunzo rasmi ya ulinzi wa wanyamapori na mafunzo ya uongozi. Pia mradi umeongeza uwezo wa wanavijiji katika usimamizi na umevifanya vijiji kuchukulia suala la usimamizi wa mazingira kuwa ni sehemu ya wajibu na majukumu ya halmashauri ya kijiji. Hii inakubaliana na sera ya taifa ya kupeleka madaraka na usimamizi wa maliasili kwa wananchi. Uwezo uliojengwa inafaa ukatumika ili kuharakisha upatikanaji wa haki za utumiaji rasilimali ya wanyamapori kwenye vijiji vya mfano.

Mapendekezo yafuatayo yanatolewa kuharakisha utaratibu huo:

- Halmashauri ya Wilaya na hasa Idara ya Maliasili inahitaji kuzithamini na kuziheshimu juhudi za wanakijiji na kuwasaidia kupata haki zao za kisheria kwenye kutumia rasilimali ya wanyamapori. Ili kuharakisha maamuzi, ushauri, na kuungwa mkono kutoka idara ya wanyamapori, kuna haja kwa Halmashauri ya wilaya kumpa jukumu la uwezeshaji mmoja kati ya maofisa wa Idara ya Maliasili. Ofisa huyo anatakiwa awe na uwezo wa kuzifasiri sheria na sera za maliasili au aweze kujifunza mambo hayo kutoka kwa washauri.
- Ujangili kwenye maeneo ya kijiji unaweza kudhibitiwa ikiwa wananchi watashirikishwa ipasavyo. Vijiji vina walinzi waliofunzwa na halmashauri ya wilaya inashauriwa kuwatumia uwezo huu ili kuiga mifano ya wilaya nyingine kama Songea, Ruvuma na Hifadhi ya Wanyamapori ya Selous ambao wanatumia walinzi waliofunzwa kwa kazi rasmi ambazo pengine ingebidi zifanywe na walinzi walioajiriwa na serikali.
- Ingefaa kukaanzishwa ushirikiano wa mafunzo na uendeshaji doria kati ya hifadhi ya Selous, walinzi (skauti) wa maliasili wa wilaya na wale wa kijiji. Ili kupunguza ujangili kwenye maeneo ya kijiji.

## 4.4 Ufuatiliaji wa wanyamapori

Kwa ujumla ufuatiliaji ni upimaji wa kudumu wa shughuli na sehemu ya kazi za kila siku ya usimamizi na uendeshaji. Tunapofanya ufuatiliaji wa wanyamapori tungependa kupima mabadiliko kwenye maeneo na mambo yote husika ili kuweza kuelewa vyema hali iliyopo na kujenga hali mpya inayotarajiwa. MUMARU umenyanyua uwezo wa wanavijiji katika kufanya ufuatiliaji. Mradi umewafunza walinzi, viongozi na wananchi kuitambua mimea mbalimbali kwenye kila kijiji cha mfano. Kinachohitajika sasa hivi ni kuweka mfumo wa ufuatiliaji, ambao utatoa mwongozo wa kitu gani, kinafanyika lini, na kinafanywa na nani. Utekelezaji wa mfumo huo utahitaji Afisa wa Wanyamapori wa Wilaya kufanya ufuatiliaji ikiwa ni sehemu za shughuli zake za kawaida.
Kutayarisha mfumo mzuri wa ufuatiliaji kunahitaji kutayarishwa warsha ya wadau ambapo kutawezeshwa kuyapitia malengo na vigezo vya mfumo wa ufuatiliaji. Kwa hiyo inapendekezwa:

- Kuendesha warsha ya kujadili na kuutengeneza mfumo wa ufuatiliaji kwa kila kijiji.
- Kutumia fomu ya ufuatiliaji yenye nafasi za kujaza ili kuweza kupata taarifa zaidi ya zile zinazokusanywa kwa kutumia daftari za doria.
- Kufuata mapendekezo yaliyotolewa na Jane K. Turpie (2000) na kuanzisha taarifa za msingi za kila kijiji (kuchambua hali iliyopo, na hali ya wanyama na makazi yao) na matumizi na thamani ya maliasili ya maeneo ya delta na kwenye bonde la Mto Rufiji.
- Kuwapa wanavijiji mafunzo zaidi ya vitendo juu ya jinsi ya kutumia GPS na kutafsiri vipimo vyake na kulinganisha vipimo hivyo na ile vya kwenye ramani. Vilevile wanakijiji wangeongezewa ujuzi wa kuweka kumbukumbu na taarifa.

## 4.5 Utekelezaji wa doria

Ushiriki wa wadau kwenye mipango vijiji ni jambo la muhimu ili kuweza kutafuta mbinu za kutatua matatizo yanayokabili mradi. Walinzi (skauti) wa maliasili na viongozi waliopatiwa mafunzo wanahitaji kuungwa mkono na Afisa wa Wanyamapori wa wilaya na/au Afisa wa Ardhi, Maliasili na Mazingira. Inapendekezwa kwamba:

- Kuna haja ya kuutambua msaada ambao wanakijiji wanauhitaji kwa ajili ya kuwawezesha kuchukua wajibu wao kwenye doria. Hili linaweza kufanyika kwenye warsha ya wadau ambako wadau wote watatakiwa kujadili na kukubaliana na mpango wa pamoja wenye kuonyesha majukumu ya kila mmoja.
- Masuala ya vifaa kama sare, kadi za utambulisho na haja ya kuwa na silaha hayawezi kuendelea kupuuzwa.
- Mambo kadhaa ambayo yamefikiwa hadi sasa yanaonekana kuwa yamefikia hatua ya kutosheleza, mambo hayo ni pamoja na mafunzo ya vitendo ya utekelezaji wa sheria ndogo ndogo, kuwakamata wahalifu na mambo ya kisheria yanayohusu hilo, pamoja na mafunzo ya ukusanyaji wa taarifa za doria. Mafunzo haya yanaweza kuimarishwa kwa kuendeshwa na mlinzi wa wanyampori yeyote aliyepata mafunzo wanyamapori huko Pasiansi.
- Watu watakaochaguliwa kuwa walinzi ni lazima wafunzwe ili wafanane na wenzao waliowatangulia. Mafunzo yanaweza kufanyika huko huko Rufiji na kusimamiwa na Afisa Wanyamapori wa Wilaya ambaye anaweza kufanya mipango mafunzo hayo yakafanyika kwenye hifadhi ya Selous. Hii inaweza kusaidia kujenga uhusiano zaidi kati ya vijiji na hifadhi ya Selous.

## 4.6 Uratibu wa wadau

Utambuzi wa wadau mara zote hufanyika wakati wa kufanya mpango wa usimamizi kwenye ngazi ya wilaya. Warsha za kutayarisha mpango huwa fupi lakini ni muhimu sana kwa kuufanya mradi uwe endelevu. Kwa hiyo ni jambo la muhimu kuipitia mipango ya usimamizi wa mazingira ya vijiji kila mwaka na kuhakikisha kuwa wadau wote wanashirikishwa hasa wale muhimu, ambao watahusika kwa njia moja au nyingine na utekelezaji wa mpango wa mazingira wa kijiji. Kwa hiyo inapendekezwa

- Kuwaorodhesha na kuwachambua wadau wote wanaojulikana na wale wanaotarajiwa ili kuweza kufahamu umuhimu wa kila mmoja wao katika utekelezaji wa mipango ya kijiji.
- Kuwajumuisha wadau wote wakati wa upangaji wa mpango wa kijiji.

## 4.7 Umuhimu wanyamapori kwa vijiji na biashara ya wanyamapori

Vijiji vyote vya mfano vina nafasi ya kujiingiza kwenye biashara za wanyamapori, lakini jambo hili linahitaji kuendelezwa na kuimarisha maeneo ya umuhimu kwa kila kijiji. Ili kufanya hivyo kunahitajika kuwepo ufahamu wa kutosha wa idadi ya wanyama na maeneo yao. Uwezo upo wa kufanya shughuli hii kwenye ngazi ya kijiji walau kwenye upande wa wanyamapori. Kwa hiyo inapendekezwa:

- Kufuatilia idadi ya wanyamapori na mienendo yao.
- Vijiji vya mfano vivishawishi vijiji vya jirani ili kuanza uhifadhi kwenye vijiji vyao.
- Halmashauri ya Wilaya ishirikiane na wanakijiji ili kudhibiti ujangili kwenye eneo la wazi la Mloka na pia ivishawishi vijiji vilivyobaki kuiga mifano ya vijiji vya mfano.

## 4.8 Utekelezaji wa miongozo ya maeneo ya usimamizi wa wanyamapori.

Vijiji vinatakiwa vifuate miongozo iliyopo ya uendeshaji wa maeneo ya usimamizi wa wanyamapori, hali hiyo ni tofauti na vijiji kama Ngarambe ambavyo ni vijiji vya mfano vya mpango wa uhifadhi wa Selous. Wakati mambo mingine, kama vile mamlaka ya ardhi ya vijiji yameshughulikiwa kwenye mapendekezo nambari 5.1, Inapendekezwa kwamba:

- Kwanza utashi wa kutaka kuwa na maeneo ya usimamizi ya wanyamapori unawasilishwa kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori. Utaratibu ni kwa baraza la kijiji kukubali, kama ilivyotakiwa kwenye Sheria ya Ardhi ya Vijiji Nambari 5 ya mwaka 1999 na kwa kupitia halmashauri ya kijiji kumtaarifu Mkurugenzi wa Wanyamapori. Nia hiyo inabidi ielezwe kwenye barua inayoambatanishwa na kumbukumbu za kikao cha baraza la kijiji ambacho kimeidhinisha mpango huo. Taarifa zinaweza kupitishwa kwenye njia za kawaida, yaani kupitia Halmashauri ya Wilaya na Kata.

- Vijiji vinashauriwa kuanzisha mikutano ya ujirani mwema na vijiji vilivyo jirani yao na kuleta muamko na uelewa juu ya matumizi na thamani ya wanyamapori kama ni hatua kuelekea kwenye usimamizi wa pamoja wa wanyama pori. Masuala haya yanaweza kujadiliwa kwenye mikutano ya Baraza Maendeleo La Kata.

## 4.9 Rasilimali za kwenye maji vijijini

Tathmini ya jumla inahitaji kufanyika ili kufahamu thamani ya mamba na kasa kwenye maeneo ya maji vijiji vya Mtanza/Msona, Mbunju/Mvuleni na Twasalie. Tathmini hiyo itahitaji mashua maalum yenye kioo chini ili atakaefanya tathmini aweze kona vilivyomo majini. Baada ya kupata takwimu na kufahamu hali halisi, itabidi mipango mipya ya usimamizi ifanyike. Kwa hiyo inapendekezwa:

- Kujadiliana na vijiji ili kupata ridhaa yao kuhusu mpango mzima kabla ya kuanza.
- Mafanikio ya Mtanza/Msona, Jaja na Twasalie katika kudhibiti vifaa vinavyotumika kuvulia samaki na katika kukusanya mapato kutokana na rasilimali ya samaki yanafaa kuigwa na kijiji cha Mbunju/Mvuleni.

## 4.10 Rasilimali ya misitu ya kijiji

MUMARU kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji umejenga uwezo wa usimamizi wa maliasili katika ngazi ya vijiji na wilaya. Sasa ni zamu ya Halmashauri ya Wilaya kuutumia uwezo huo. Kwa hivyo inapendekezwa kwamba:

- Halmashauri ya Wilaya ivisaidie vijiji kwa kufungua Daftari la Usajili wa Misitu ya Hifadhi na kuitambua misitu ya hifadhi ya vijiji kama ambavyo inatakiwa kisheria. Kifungu cha 40 cha Sheria ya Misitu ya Mwaka 2002 inaruhusu jambo hili.
- Halmashauri ya Wilaya inawajibu wa kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya usimamizi na uendeshaji wa misitu.

# 5 Viambatisho

## 5.1 KIAMBATISHO 1: Madhumuni na Majukumu ya Ushauri Kulingana na Hadidu Rejea

**1. UTANGULIZI:**
Mradi wa usimamizi wa mazingira Rufiji (MUMARU) ofisi yake ipo Utete mjini ambako ni Makao Makuu ya Wilaya ya Rufiji. Lengo la mradi huu ni kusaidia uhifadhi wa muda mrefu ya misitu, na maeneo chepechepe ili kuhakikisha bayoanuai inahifadhiwa, mifumo muhimu ya Ikologia inatunzwa, maliasili zinatumika vyema, na maisha ya wakazi wa eneo hilo yanakuwa bora.

Madhumuni muhimu ya mradi katika kipindi cha miaka mitano ya kwanza ni kama yafuatayo:-

A. Kuinua hali ya uhifadhi wa mazingira na maendeleo endelevu kwa kutayarisha mpango wa mazingira ya bonde na delta ya Mto Rufiji.
B. Kuboresha matumizi endelevu ya maliasili na kuinua hali ya maisha ya jamiii husika kwa kutekeleza shughuli za maendeleo endelevu katika eneo la majaribio kwa kuzingatia kanuni za matumizi ya busara.
C. Kuinua kiwango cha ufahamu wa wananchi kuhusu thamani ya misitu, maeneo chepechepe na pia umuhimu wa kuzingatia matumizi bora katika ngazi za kijiji, wilaya, mkoa na serikali kuu. Pia, kutoa mchango utakaosisitiza uundaji wa sera za taifa za maliasili usiochukua sura ya kisekta na utakaokuwa kwa misingi ya uwiano.

Kazi hii ya ushauri inahusika zaidi na madhumuni (a) na (b) yaliyotajwa hapo juu, hasa kuhusu utekelezaji wa masuala yagusayo wanyamapori katika mipango ya usimamizi wa mazingira ya kijiji.

**2. <u>Utangulizi</u>**
Katika bonde la delta ya Mto Rufiji kuna vijiji hamsini na mbili vilivyo na idadi ya watu wanaokadiriwa kufikia 150,000 ambao maisha yao yanategemea zaidi kilimo na uvuvi. Eneo la mradi wa MUMARU linahusisha eneo la misitu ya mikoko ambalo ni kubwa zaidi ya yote katika eneo la magharibi ya bahari ya Hindi pamoja na misitu ya mwambao, ufukwe, maeneo chepechepe, misitu ya juu na vichaka (IUCN 1997). Pia eneo hili linapakana na Hifadhi ya Wanyamapori ya Selous ambayo ni moja ya maeneo machache katika Afrika ambako wanyamapori bado wanapatikana nje ya maeneo yanayohifadhiwa. Inafahamika kuwa maeneo muhimu ya makaazi ya wanyama na ndege katika misitu iliyopo kwenye bonde la delta ya Mto Rufiji yanapungua kwa kasi kutokana na matumizi yasiyodhibitiwa. Hali hii pia inahusisha uvunaji holela wa wanyamapori na uharibifu wa maneo yao unaosababishwa na ukosefu wa usimamizi bora. Kuna migongano kati ya watu na wanyamapori. Wakazi wa eneo hili wanadai kuwa umaskini wao unasababishwa na wanyama pori ambao wanaathiri mazao, mifugo pamoja na kutishia maisha yao. Hali hii imeathiri ushirikiano baina ya uongozi wa hifadhi na wanakijiji na hivyo kusababisha migogoro baina yao kuhusu mpaka wa hifadhi ya Selous.

MUMARU umekuwa ukifanyakazi katika ngazi za wilaya, mkoa na taifa ili kuboresha usimamizi wa mazingira pamoja na kudhibiti uvunaji wa Wanyamapori katika bonde na delta ya Mto Rufiji. Sehemu muhimu ya kazi hii inahusisha utayarishaji wa mpango wa usimamizi wa mazingira wa bonde na delta ya Mto Rufiji. Utayarishaji wa mpango huo unashirikisha wadau mbalimbali kama vile Mkurugenzi wa Wanyamapori, Shirika la misaada la Ujerumani, Hifadhi ya Selous, Kampuni za Uwindaji, Kampuni za Utalii, Idara ya Misitu na Nyuki, WCST, WWF na wingineo. MUMARU umekuwa ukifanya kazi katika vijiji vinne vya mfano viwili vikiwa kwenye maeneo ya delta (Twasalie na Jaja) na viwili viko kwenye tambarare la mafuriko (Mbunju/Mvuleni na Mtanza/Msona) mbinu hii imesaidia kutambua masuala muhimu yanayopasa kupewa vipaumbele kwenye usimamizi wa mazingira kwa ujumla. Vijiji hivi vyote vimetayarisha mipango ya usimamizi wa mazingira inayojumuisha utengaji wa maeneo ya matumizi tofauti na taratibu za usimamizi wake.

Vijiji hivyo vimeunda kamati mpya za usimamizi wa mazingira zinazojihusisha na utekelezaji wa mipango ya usimamizi wa kila kijiji. Mipango ya utekelezaji, ratiba na bajeti zimetayarishwa ili kutekeleza mipango ya usimamizi. Kanuni mbalimbali zenye kusaidia usimamizi wa ardhi/maliasili zimeainishwa. Kanuni zilizoanza kutekelezwa ni kanuni za usimamizi wa wanyamapori zinazotekelezwa na wanavijiji pamoja na walinzi wanaohusika na masuala ya maliasili ambao wamepewa mafunzo maalum. Kanuni hizo zitatekelezwa katika misitu ya hifadhi ya vijiji ambayo inaanzishwa.

Misaada hasa ya mafunzo imekuwa ikitolewa kwa wanavijiji ili waweze kuanzisha mifumo ya usimamizi wa mazingira. Maskauti wanaohusika na masuala ya maliasili pamoja na baadhi ya viongozi kutoka kila kijiji walipata mafunzo huko Likuyu Sekamaganga. Pia wawakilishi toka katika vijiji hivyo walishiriki katika ziara za mafunzo (Wami–Mbiki, Jukumu Society, Hifadhi ya Selous) yaliyohusu jinsi ya kudhibiti wanyama waharibifu pamoja na masuala ya sheria. Wahusika wa mafunzo hayo walitaja maeneo mingine ya mafunzo ambayo wanayahitaji. Hayo ni pamoja na utaalamu wa vitendo katika kufuatilia usimamizi wa maliasili, masuala ya sheria na utoaji leseni, nafasi za biashara mbalimbali, utaalamu wa biashara zinazohusiana na wanyamapori na kuanzisha mahusiano ya kibiashara baina yao na vijiji vingine pamoja na taasisi mbalimbali za biashara. Wanavijiji hao wanaelewa kwamba muongozo mpya wa Serikali ya Tanzania wa usimamizi wa wanyamapori unatoa nafasi kwa jamii katika kuthibiti wanyamapori na pia walionyesha nia ya kupata mafunzo na mazoezi ya jinsi ya kutekeleza muongozo huo.

MUMARU na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji zinakabiliwa na upungufu wa wataalamu wa huduma za ughani kuhusu wanyamapori, hivyo wanahitaji mshauri atakaesaidia kuharakisha suala la kuwaelimisha wanavijiji kuwa na mamlaka makubwa zaidi ya kuthibiti wanyamapori ili kuwasaidia kupata faida kubwa itokanayo na wanyamapori. Halmashauri ina mpango wa kumpata mtaalamu wa masuala ya usimamizi shirikishi wa wanyamapori ambaye atafanyakazi kwa vipindi vifupi kwa muda wa kiasi cha mwaka mmoja ili aweze kuwasaidia maafisa wa wilaya wa Idara mbalimbali ambao ndio wawezeshaji wa suala zima la usimamizi wa mazingira katika vijiji. Mshauri wa masuala ya Wanyamapori atafanyakazi kwa karibu na Ofisi ya Wanyamapori ya Wilaya pamoja na wawezeshaji wawili wa masuala ya mipango ya mazingira vijijini na mshauri wa masuala ya misitu ili waweze, kwa pamoja, kutoa ushauri wa kitaalamu kwa vijiji hivyo vinne. Kwa bahati fedha za kufanya shughuli hii tayari imeshatolewa na taasisi ya Hoag.

## 3. MADHUMUNI YA SHUGHULI YA USHAURI.

Madhumuni makuu ya shughuli hii ya ushauri inayopendekezwa ni kama yafuatayo:-

- Kuviwezesha vijiji vinne vya mfano kuinua kiwango cha usimamizi wa wanyamapori katika maeneo yao ya Utawala ili wanavijiji wapate faida ya moja kwa moja na pia kupunguza athari katika rasilimali.
- Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wanavijiji juu ya maendeleo na utekelezaji vipengele mbalimbali vinavyohusu wanyamapori na ndege katika mpango wa ufuatiliaji maliasili yao.
- Kuwasaidia wanavijiji kwa kuwapa mawazo na njia za kutathmini uwezekano wa kuanzisha biashara zinazohusiana na wanyamapori na kuunda mpango wa muda mrefu utakaofikia mahitaji yao ya maendeleo ya kibiashara.
- Kutoa taarifa za ujumla kuhusu wanyamapori na kutoa ushauri hasa katika kutafsiri na kutumia muongozo mpya unaohusu mpango wa usimamizi wa mazingira katika eneo la mradi ili kusaidia halmashauri ya wilaya ya Rufiji na MUMARU katika kuleta maendeleo kwa kushirikiana na wadau wingine kama vile hifadhi ya Selous, kampuni binafsi, GTZ, WWF na taasisi nyingine za maendeleo ambazo zimo kwenye mpango wa usimamizi wa mzingira wa eneo la mradi.

## 4. MAJUKUMU YA SHUGHULI HII YA USHAURI

Majukumu yanayotakiwa kutekelezwa ili kufikia malengo makuu manne ni kama yafuatavyo;-

### 4.1. **Maelezo mafupi juu ya hali halisi ya sasa**.

4.1.1

- Kupitia taarifa na nyaraka za MUMARU ili kuweza kuelewa hali halisi ya kila kijiji.

- Kuwasiliana na maafisa wa wilaya ambao wamesheriki kwenye uwezeshaji wa utayarishaji wa mipango ya usimamizi wa mazingira vijijini. Hususan wawezeshaji wawili wa mipango ya usimamizi ya mazingira ya vijiji, pamoja na mshauri wa misitu na mshauri wa udhibiti wa Wanyama waharibifu.

- Kutembelea vijiji husika ili kuona hali halisi na kuongea na wanavijiji ili kupata maelezo ya shughuli wanazoendelea nazo na kufahamu matarajio yao.

4.1.2 Kukubaliana kwa pamoja na wanavijiji na maofisi wa Wilayani na wale wa Mradi wa Usimamizi wa Mikoko juu ya mipango ya utekelezaji na pia kutayarisha ratiba itakayolenga kufanikisha kutumika kwa sheria kuhusu maeneo ya usimamizi wa Wanyamapori Vijijini na mipango mingine ya usimamizi kadri iwezekanavyo.

4.1.3 Kutekeleza mikakati iliopo kwa kushirikiana na Kamati za mazingira za vijiji, Wataalam wa Wilaya pamoja na mradi wa Mikoko na vyombo husika katika ngazi ya Taifa.

## 5. MATOKEO

Serikali za vijiji vinne, kamati za mazingira pamoja na walinzi wa maliasili watakuwa na ufahamu zaidi kuhusu haki na wajibu wao na uwezekano wa kuinua kiwango cha faida itokanayo na usimamizi wa wanyamapori.
Vijiji vinne vitakuwa vinatumia mbinu mpya za usimamizi wa Wanyamapori. Kuanzishwa na kujaribiwa kwa kwa mfumo wa ufuatiliaji wa ndege na Wanyamapori kwenye kila kijiji kati ya hivyo vinne.
Wanavijiji wawe wameinua na kujenga uwezo wa kutumia nafasi zilizopo katika kuanzisha biashara zinazohusiana na Wanyamapori kwa kutumia angalau moja ya mawazo mapya ya kuanzisha biashara kwa kila kijiji. MUMARU na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji waweze kuweka wanapata taarifa sahihi zinazohusu maendeleo katika sekta ya wanyamapori.

## 6. UTAALAMU UNAOHITAJIKA.

Mshauri anatakiwa awe ni mhitimu katika fani inayohusu usimamizi wa wanyamapori na awe na uzoefu usiopungua miaka mitatu katika masuala ya usimamizi wa wanyamapori kwa kushirikisha jamii. Ni muhimu kwa mtaalamu huyo kuwa ujuzi wa sheria na sera za Tanzania zinazohusiana na masuala usimamizi wa wanyamapori kwa kushirikisha jamii na biashara binafsi za Wanyamapori

## 7. MIPANGO NA UTOAJI RIPOTI.

Mipango ya kazi ya kila mwezi itatayarishwa na kuwasilishwa kwa mshauri wa kitaalamu katika masuala ya maendeleo ya jamii na Afisa ardhi maliasili na mazingira (DLNREO).

Taarifa za utekelezaji wa kazi zitatayarishwa katika kompyuta na kuchapishwa kwa misingi ya siku 25 za kazi. Taarifa hizi zitawasilishwa kwa mdomo na pia kuonyeshwa kwa timu inayohusika na usimamizi wa mazingira katika kila mikutano yao ya mwezi. Taarifa ya mwisho itawasilishwa katika kipindi cha mwezi mmoja baada kumalizika kwa mkataba huu.

## 8. RATIBA.

Kazi hii inapendekezwa ifanyike kwa siku 40 ambazo zitagaiwa kwenye muda wa sehemu mbili za siku ishirini (20) kila moja kwenye kipindi cha miezi sita. Tarehe ya kuanza kazi ni 1 Julai 2002, na tarehe ya kumaliza ni 31 Desemba 2002 (au mapema zaidi kulingana na kiwango cha ukamilifu wa kazi). Mapendekezo ya utendaji wa kazi ni kama yalivyoainishwa katika jedwali hapo chini.

| **KAZI** | **idadi ya siku** | **MUDA** |
|---|---|---|
| Kujizoeza mazingira, kupanga na kuanza kazi ya ugani ya kwanza | 19 | Wiki ya pili, tatu na nne za mwezi Julai na wiki ya kwanza ya mwezi Agusti |
| Kufanya mawasaliano mbalimbali na kutayarisha matokeo ya kazi ya kwanza ya ugani | 1 | Wiki ya pili ya mwezi Agusti |
| Kuwasilisha taarifa ya kazi ya kwanza ya ugani | | Mwisho wa wiki ya pili ya mwezi Agusti |
| Kazi ya ugani ya pili | 19 | Wiki ya nne ya mwezi Octoba (28.10.02) mpaka wiki ya tatu ya mwezi Novemba |
| Kupitia upya kazi iliyofanyika, kuwasilisha katika Timu ya Usimamizi wa Mazingira na kutoa taarifa | 1 | Wiki ya nne ya mwezi Agosti |
| Kuwasilisha taarifa ya kazi ya pili ya ugani | | Mwisho wa wiki ya nne ya mwezi Novemba |
| **JUMLA** | **40** | |

## 5.2 Kiambatisho 2: Utaratibu wa Safari ya Kwanza

| TAREHE | KAZI YA KUFANYA |
|---|---|
| Julai 7 | Kwenda Dar-es-salaam |
| Julai 8 | Kwenda Kibiti |
| Julai 9 | Kwenda Utete |
| Julai 10 | -Kukutana na wafanyakazi wa wilayani<br>-Kupata maelezo mafupi toka kwa Wawezeshaji wa MUMARU na Mshauri wa Udhibiti wa wadudu/wanyama waharibifu<br>-Kusoma nyaraka mbalimbali na kuandaa taarifa ya kazi ya ushauri<br>-Kukubaliana na mpangilio wa kazi ya kwanza |
| Julai 11-12 | Safari kuelekea kijiji cha Ngarambe kwaajili ya ukaguzi wa awali |
| Julai 13 | Kutembelea Kingupira- makao makuu ya sehemu ya mashariki ya Selous |
| Julai 15 | -Kwenda Utete<br>-Kupata maelezo toka kwa Mshauri wa kitalaamu wa masuala ya maendeleo ya jamii<br>-Kwenda Mtanza/Msona |
| Julai 16 | -Kujizoeza mazingira ya kijijini, kusafiri kwenda kituo cha wanyama pori cha Mtemere<br>- Kuweka kambi ng'ambo ya mto |
| Julai 17 | -Kutembelea mashamba<br>-Mafunzo kwa vitendo juu ya nidhamu ya doria, majukumu ya shughuli za doria na kunakili taarifa<br>-kutembelea mpaka mpya wa hifadhi ya Selous |
| Julai 18 | Kurudi kijijini. Mkutano kwa ajili ya kupeana taarifa ulishindikana kufanyika kutokana na shughuli za mazishi kijijini |
| Julai 19 | Mkutano ili kupeana taarifa ya maendeleo ya kazi iliyofanyika kati ya Julai 16-18 |
| Julai 20 | -Mafunzo<br>Umuhimu wa rekodi za doria<br>Sensa ya wanyama na mahesabu yake<br>Sera na sheria za ardhi na maliasili<br>Vipengele vya kisheria katika kudhibiti wanyama waharibifu<br>Kutambua maeneo muhimu ya uwekezaji kwa shughuli zinazohusiana na wanyamapori<br>Miongozo ya msingi katika kuanzisha maeneo ya usimamizi wa wanyamapori |
| Julai 21 | -Kurudia kwa ufupi mafunzo ya Julai 20<br>-Mafunzo juu ya<br>Utambuzi wa alama mbalimbali na matumizi yake katika kufuatilia maliasili ya wanyamapori<br>Sheria na taarifa za utoaji leseni za uwindaji na ukamataji wa wanyamapori |
| Julai 22 | Kwenda eneo la mpaka wa msitu wa kijiji upande wa Kaskazini na kufanya doria |
| Julai 23 | Kufanya doria katika eneo la kijiji, kutembelea mpaka wa kijiji na kijiji cha Vikumburu |
| Julai 24 | -Kutembelea msitu wa Zilizili<br>-Mazoezi ya vitendo ya sensa ya wanyama<br>-Kurudi kijijini na kufanya mkutano wa kutoa taarifa ya mwelekeo wa shughuli inayofanyika |
| Julai 25 | - Mazoezi ya kusoma ramani and kutafsiri taarifa zinazotokana na kifaa kinachorekodi eneo kilichopo na kuhusisha rekodi hizo katika usomaji ramani<br>-Kwenda Utete |
| Julai 26 | Kuandika taarifa |
| Julai 27 | Kwenda Ikwiriri |
| Julai 28 | Kwenda Mbunju/Mvuleni |

| | |
|---|---|
| Julai 29 | Kujizoeza maeneo ya kijiji, kupanga muda wa utekelezaji masuala ya kijijini |
| Julai 30 | Kutembelea mashamba |
| Julai 31 | Mkutano ili kupeana taarifa ya maendeleo ya kazi |
| Agosti 1-2 | -Kutembelea msitu na kufanya doria<br>-Mazoezi ya vitendo ya sensa ya wanyama |
| Agosti 3 | -Mafunzo<br>Umuhimu wa rekodi za doria<br>Sera na sheria za ardhi na maliasili<br>Vipengele vya kisheria katika kudhibiti wanyama waharibifu<br>Kutambua maeneo muhimu ya uwekezaji kwa shughuli zinazohusiana na wanyamapori<br>Miongozo ya msingi katika kuanzisha eneo la usimamizi wa wanyamapori<br>Vipengele vya kisheria katika usimamizi wa maliasili kwa kushirikisha jamii<br>Sheria na taarifa za utoaji leseni za uwindaji na ukamataji wa wanyamapori |
| Agosti 4 | -Kurudia kwa ufupi mafunzo ya Agosti 3<br>-Mafunzo juu ya<br>Sensa ya wanyama na mahesabu yake<br>Utambuzi wa alama mbalimbali na matumizi yake katika kufuatilia maliasili ya wanyamapori<br>Mazoezi ya kusoma ramani and kutafsiri taarifa zinazotokana na kifaa kinachorekodi eneo kilichopo na kuhusisha rekodi hizo katika usomaji ramani |
| Agosti 5 | Kutoa taarifa ya maendeleo ya kazi na kufanya tathmini ya mafunzo |
| Agosti 6-7 | Kuandika taarifa |
| Agosti 9 | Kwenda Dar-es-salaam |

## 5.3 Kiambatisho 3: Utaratibu wa Safari ya Pili

| TAREHE | KAZI YA KUFANYA |
|---|---|
| Nov 3 | Kwenda Dar-es-salaam |
| Nov 5 | Kwenda Utete |
| Nov 6 | -Mkutano na wafanyakazi wa wilayani kuzungumzia taarifa ya awali ya safari ya kwanza na Mshauri wa kitaalam katika masuala ya maendeleo ya jamii |
| Nov 7 | Kukutana na DLNRE na afisa biashara ili kuzungumzia masuala mbalimbali yaliyopewa kipaumbele katika taarifa ya awali ya safari ya kwanza |
| Nov 8 | -Kukutana na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ili kuzungumzia masuala mbalimbali yaliyopewa kipaumbele katika taarifa ya awali ya safari ya kwanza<br>-Kuzungumza na Afisa Wanyamapori wa Wilaya kuhusu masuala mbalimbali pamoja na wajibu wake katika warsha iliyopangwa kufanyika<br>-Kwenda Ikwiriri |
| Nov 9 | -Kwenda Twasalie<br>-Kukutana na viongozi wa kijiji na wanakijiji kwa utambulisho na kujizoesha mandhari ya kijiji na maliasili yake na utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa mazingira ya kijiji na kuandaa ratiba ya kazi kwa siku zote sita za kuakaa kijijini hapo |
| Nov 10 | Kufanya doria eneo la Mbalanyimbo na Ngatola ambalo lina utaratibu wa mpango shirikishi wa usimamizi wa msitu wa hifadhi |
| Nov 11 | Kutembelea mashamba kijiji kidogo cha Domwe |
| Nov 12 | Mafunzo<br>Sera na sheria za ardhi na maliasili<br>Vipengele vya kisheria katika kudhibiti wanyama waharibifu<br>Utaratibu wa sensa ya makundi ya wanyama na matumizi ya taarifa zitokanazo na sensa<br>Kutambua maeneo muhimu ya uwekezaji kwa shughuli zinazohusiana na wanyamapori<br>Mazoezi ya kusoma ramani and kutafsiri taarifa zinazotokana na kifaa kinachorekodi eneo kilichopo na kuhusisha rekodi hizo katika usomaji ramani |
| Nov 13 | -Kurudia kwa ufupi mafunzo ya Novemba 12<br>-Mafunzo juu ya:<br>Doria za kuzuia ujangili na umuhimu wa kutunza taarifa hizo, kuwa na mipango katika ngazi ya kijiji na utawala bora<br>Vipengele vya kisheria katika usimamizi wa maliasili kwa kushirikisha jamii ikihusisha sera na sheria<br>Sheria na taarifa za utoaji leseni za uwindaji na ukamataji wa wanyamapori<br>Utambuzi wa alama mbalimbali na matumizi yake katika kufuatilia maliasili ya wanyamapori |
| Nov 14 | -Mkutano na wanakijiji ili kupeana taarifa na kuzungumzia maendeleo ya kazi iliyofanyika kati kipindi chote cha siku tano<br>-Kutathmini mafunzo yaliyotolewa<br>-Kukutana na Bwana Sima na Michael Mradi wa kusimamia mikoko ili kuzungumzia masuala ya kisheria pamoja na wanakijiji katika mkutano wa kupeana taarifa ya maendeleo ya kazi |
| Nov 15 | Kwenda Jaja ili kuonana na uongozi wa kijiji na kupanga kwaajili ya Novemba 15 |
| Nov 16 | Kukutana na viongozi wa kijiji na wanakijiji kwa utambulisho na kujizoesha mandhari ya kijiji na maliasili yake na kuandaa ratiba ya kazi kwa siku zote sita za kuakaa kijijini hapo |
| Nov 17 | Kutembelea kisiwa cha Beden, Makao na Kilobani ambako kuna utaratibu wa mpango shirikishi wa usimamizi wa misitu ya hifadhi |
| Nov 18 | -Kutembelea mashamba ya King'ongo katika kijiji cha Ruma |

| | |
|---|---|
| | -Kukusanya, mtaalam mshauri wa maendeleo ya jamii, Nandi na Haji |
| Nov 19 | Mafunzo juu ya:<br>Sera na sheria za ardhi na maliasili<br>Vipengele vya kisheria katika kudhibiti wanyama waharibifu<br>Utaratibu wa sensa ya makundi ya wanyama na matumizi ya taarifa zitokanazo na sensa<br>Mazoezi ya kusoma ramani and kutafsiri taarifa zinazotokana na kifaa kinachorekodi eneo kilichopo na kuhusisha rekodi hizo katika usomaji ramani |
| Nov 20 | -Kurudia kwa ufupi mafunzo ya Novemba 19<br>-Mafunzo juu ya:<br>Mazoezi ya kuhesabu wanyama na jinsi ya kuchora matokeo hayo<br>Doria za kuzuia ujangili na umuhimu wa kutunza taarifa hizo, kuwa na mipango katika ngazi ya kijiji na utawala bora<br>Vipengele vya kisheria katika usimamizi wa maliasili kwa kushirikisha jamii ikihusisha sera na sheria<br>Sheria na taarifa za utoaji leseni za uwindaji na ukamataji wa wanyamapori<br>Utambuzi wa alama mbalimbali na matumizi yake katika kufuatilia maliasili ya wanyamapori |
| Nov 21 | -Kutathmini mafunzo yaliyofanyika na kuzungumzia matokeo ya mafunzo hayo<br>- Mkutano ili kupeana taarifa ya maendeleo ya kazi |
| Nov 22 | Kutembelea mashamba ya Mpendeni yaliyopo kijiji cha Ruma |
| Nov 23 | Kwenda Utete |
| Nov 24-25 | Kuandaa taarifa na kufanya maandalizi ya warsha |
| Nov 26 | Warsha ili kutoa taarifa kwa wajumbe wa timu ya usimamizi wa mazingira |
| Nov 27 | Kuhitimisha shughuli na kuanza safari ya kurudi Dar-es-salaam |

## 5.4 Kiambatisho 4:Mpato yatokanayo na Uwindaji wa Kujkimu Katika Kijiji Cha Ngarambe

| MWAKA | **KIASI CHA PESA (shilingi)** |
|---|---|
| 1995/96 | 526,450 |
| 1996/97 | 238,320 |
| 1997/98 | 1,504,900 |
| 1998/99 | 2,019,920 |
| 1999/00 | 2,148,500 |
| 2000/01 | 2,833,700 |
| 2001/02 | 4,766,750 |

Chanzo: Kamati ya Usimamizi wa maliasili ya ngarambe



## 5.5 Kiambatisho 5: Mfano wa Formu ya Kutunzia Taarifa ya Ufuatiliaji wa Wanyamapori

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Tarehe ya doria | | | | |
| Vipimo vya kifaa cha kutambulisha eneo uliopo | Mashariki | | | |
| | Kaskazini | | | |
| Jina la sehemu | | | | |
| Wanyamapori | Spishi/jina la kienyeji | | | |
| | Kazi | | | |
| | Wanaume | | | |
| | Wanawake | | | |
| | Watoto | | | |
| | Jumla | | | |
| Uoto | Jina la kisayansi/jina la kienyeji | | | |
| | Aina ya uoto | | | |
| | Maelezo/Wingi | | | |
| Rasilimali za maji | Jina la kisayansi/jina la kienyeji | | | |
| | Maelezo | | | |
| | Kazi | | | |
| Njia za wanyama | Jina la kisayansi/jina la kienyeji | | | |
| | Maelezo ya malisho/mwenendo wa wanyama | | | |
| Mitego | Aina | | | |
| | Idadi | | | |
| | Maelezo | | | |
| Majangili/Wawindaji haramu ambao hawakupatikana | Majina | | | |
| | Uhalifu uliofanyika | | | |
| | Hatua zilizochukuliwa | | | |
| Maoni | Ya jumla | | | |
| | Ushauri/ Mapendekezo | | | |
| Timu ya doria | Kiongozi wa safari | | | |
| | Wingine | | | |
| Anae nukuu taarifa | Jina | | | |
| | Sahihi | | | |

## 5.6 Kiambatisho 6: Orodha ya Watu Tuliokutana Nao/Waliotoa

TAARIFA

Watu tuliokutana nao wakati wa utambulisho katika ngazi ya wilaya na wanaotoka katika taasisi nyinginezo

| NaM. | jina | Cheo | Anwani | simu/anwani ya barua pepe/njia nyingine za kuwasiliana |
|---|---|---|---|---|
| 1 | R. X. Nandi | Afisa matumizi ya ardhi - ezeshaji | Box 40 Utete | |
| 2 | Haji Mkungura | Msaidizi Wanyamapori | Box 12 Utete | |
| 3 | Pili Mwambeso | Afisa kilimo - ezeshaji | Box 12 Utete | |
| 4 | Juma I. Mkungura | Afisa Msaidizi Wanyamapori | Box 12 Utete | |
| 5 | M.S. Chande | Afisa Maliasili na Mazingira Wilayani | Box 12 Utete | |
| 6 | Eniyoye J. John | Afisa Wanyamapori wa Wilaya | Box 12 Utete | |
| 7 | Brg. Jenerali S. Hemed | Mkuu wa Wilaya | Box 43 Utete | |
